SportPesa
TZS. 878,152,880
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Mjadala** waibuka ofisa wa polisi kujiua mahabusu

UKURASA 3




UKURASA 30

Nipashe
Alhamisi Januari 27, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580838
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# Rais Samia akerwa mauaji

• **Amtaka** IGP kuyakomesha haraka, aliyedaiwa kumuua mjamzito, watoto anaswa, wengine mbaroni tuhuma mauaji bibi kizee...*Endelea Uk. 2&3*

## YALIYOMO

UKURASA WA 7
**PM ATAKA WATANZANIA KUIPA HADHI TANZANITE**
WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka Watanzania kushirikiana na...

UKURASA WA 7
**LUTENI ADAI KUKUBALI KUMTAFUTIA FREEMAN MBOWE MAKOMANDOO**
SHAHIDI wa 12 katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA...

UKURASA WA 9
**JAMHURI YAPINGA KESI YA NDUGAI KUJIUZULU**
WAKILI Mkuu wa Serikali, Gabriel Malata, ameiomba Mahakama Kuu kutupilia mbali kwa gharama shauri la kikatiba...



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (kulia), akikabidhi rambirambi kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, kwa ajili ya ndugu wa familia ya Hosea Kapande aliyeuawa pamoja na familia yake ya watoto wanne Kijiji cha Zanka, wilayani Bahi. Dk. Mpango alifika kijijini hapo jana kutoa pole kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Takwimu za wagonjwa, vifo UVIKO kutangazwa

UKURASA 3

## Askari mstaafu ajinyonga kwa kutumia waya wa pasi

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA SC YAPAKATWA TENA UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Rais Samia akerwa mauaji

**Na Paul Mabeja,** BAHI

RAIS Samia Suluhu Hassan ameelezea kukerwa na mauaji yanayoendelea huku akimtaka Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali Simon Sirro, kuchukua hatua kukomesha vitendo hivyo.

Pia ametoa siku saba kwa Jeshi la Polisi Mkoa wa Dodoma kuwakamata watu wote waliohusika na mauaji ya kikatili ya watu watano wa familia moja katika kijiji cha Zanka, Bahi mkoani hapo.

"Tukio hili la watu watano wa familia moja kuuawa na watu wasiojulikana na kutelekezwa ndani ya nyumba halikubariki na linaumiza sana. Hivyo basi, Rais Samia amenituma nije kutoa pole. Natoa siku saba kwa Jeshi la Polisi kuanzia leo (jana) kuhakikisha watu wote bila kuachwa hata mmoja, wanakamatwa na taarifa iletwe kwa Rais," alisisitiza Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango kwa niaba ya Rais.

Alisema watu wote waliohusika katika tukio hilo la kinyama polisi iwasake popote walipo bila kuacha mtu.

"Mkuu wa Mkoa pamoja na kamati yako ya ulinzi na usalama naagiza ndani ya hizo siku saba watu wote wawe wamekamatwa na kupata stahiki ya kufikishwa mahakamani, nawataka mhamie katika kijiji hiki hadi hapo mtakapo wakamata watu wote waliohusika na tukio hili," alisema Dk. Mpango.

Pia aliiagiza Idara ya Upelelezi kuongeza nguvu katika eneo hilo na kufanya kazi usiku na mchana ili kukamilisha uchunguzi wa tukio hilo ndani ya muda alioutoa.

"Inashangaza sana nyumba ipo hapa, lakini kuna majirani kweli walishindwa hata kusikia sauti au kushtuka kwanini wenzao hawaonekani kwa siku tatu na hapa kuna zizi la mifugo na ilikuwa inakwenda kuchungwa na watu wanakamua maziwa mpaka miili ya wenzao inaharibika na kutoa harufu ndipo wanashtuka, natumaini vyombo vya usalama hawa watu pia wanaisaidia polisi hata kama ni ndugu," alisema.

Akizungumzia mauaji mengine ya kikatili yanayoendelea kuripotiwa katika maeneo mbalimbali ya nchini, alimwagiza Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Sirro kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama wanayakomesha.

"IGP yupo hapa, kama hayupo nakuagiza RPC umfikishie maagizo haya nataka kuanzia leo matukio ya mauaji ya kikatili yanayoendelea kuripotiwa katika maeneo mbalimbali ya nchi yanakomeshwa, tumechoka kuendelea kuongoza nchi ambayo kila siku kuna taarifa za watu kuuana na vyombo vya usalama vipo.

"Leo mchana tu nilikuwa nasikiliza taarifa ya habari nimesikia mauaji yamefanyika Mtwara na watuhumiwa ni askari polisi, lakini Mbeya baba kauawa, mtuhumiwa ni mwanawe mwanajeshi na kule Moshi mama kauawa mtuhumiwa binti yake, Jeshi la Polisi mnayo kazi ya kufanya, Rais amechoka mimi nimechoka, hatuwezi kuendesha nchi namna hii," alisisitiza Dk. Mpango.

Aliwataka Watanzania kupendana na kuacha chuki zinazosababisha matukio ya mauaji ya kinyama.

"Viongozi wa dini nawaomba mtumie nyumba za ibada kuongea na waumini, hakuna mtu mwenye haki ya kuondoa uhai wa mwenzake leo hii hata simba wenyewe hawauani, lakini sisi tunafanya mambo ya wanyama," alisema Dk. Mpango kwa masikitiko.

Pia alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Mnkunda, kuitisha mkutano wa hadhara na wanakijiji wa eneo hilo ili kujadiliana masuala ya ulinzi na usalama.

"Wana Zanka mmenisikitisha sana mimi, hivi hamfahamu kuwa ni mkazi wa kata hii naogopa hata kusema nina shamba hapa, nchi nzima wameifahamu Zanka, lakini kwa sifa ya mauaji, inatishia sana hasa kwa nchi yetu ambayo inasifika kwa amani na utulivu sasa watu wataogopa hata kulala ndani ya nyumba zao."

Miili ya familia hiyo iliyouawa, ilikutwa ndani ya nyumba yao Januari 22, mwaka huu, ikiwa imeanza kutoa harufu baada ya kuanza kuharibika.



Mhariri Mtendaji wa gazeti la The Guardian, Wallace Mauggo (kushoto), akitoa ufafanuzi kwa wanafunzi wa Shule ya Genesis, walipofanya ziara kwenye chumba cha habari cha Kampuni ya The Guardian Ltd, Mikocheni, Dar es Salaam jana. Kushoto kwake ni Mhariri Mwandamizi wa gazeti la Nipashe, Epson Luhwago. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ofisa mstaafu polisi ajinyonga

**Na Mwandishi Wetu**

OFISA mstaafu wa Jeshi la Polisi, Omary Msangi (58), amekutwa amekufa chooni nyumbani kwake, huku akidaiwa kujinyonga kwa kutumia waya wa pasi.

Taarifa zinaeleza kuwa kabla ya kutekeleza kitendo hicho, Msangi alijaribu kujiua kwa kumeza dawa, kitendo ambacho hakufanikiwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Simon Maigwa, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo.

Tukio la kujinyonga kwa mstaafu huyo lilitokea usiku wa kuamkia Januari 25 akiwa kwenye nyumba aliyokuwa akiishi eneo la Kiboriloni Manispaa ya Moshi, ikidaiwa alikuwa na mgogoro wa kifamilia na mmoja wa wanafamilia.

Kwa mujibu wa jirani, Rashid Hamza, tukio hilo lilitokea katika eneo la Mbwa Haruki, Kata ya Kibolroni, Manispaa ya Moshi.

"Tulipofika nyumbani kwake, mkewe Halima Daud alituambia mumewe amejinyonga kwa waya wa pasi uliokuwa umefungwa kwenye dirisha la chooni chumbani kwao, wakati alipotoka kwenda kutafuta maziwa baada ya mumewe huyo kumeza dawa nyingi kwa jaribio la kujiua," alisema jirani huyo na kuongeza:

"Ila kunatetesi kuwa marehemu alikuwa na ugomvi wa kifamilia na mmoja wa wanafamilia (anamtaja), tangu alipostaafu hawakuwa na maelewano mazuri, pia Msangi kabla ya kustaafu alipata ugonjwa wa moyo na inasemekana alitapeliwa na kununua kiwanja feki na kutoa fedha za ujenzi na ujenzi haukufanyika, hali iliyosababisha malumbano kati yao.

Hamza alisema majira ya saa nne usiku Januari 24 kulitokea ugomvi kati ya Msangi na mwanafamilia huyo, na kumtaka wakwe wa kiume kufika nyumbani hapo.

"Tulivyosikia ni baada ya marehemu kumtaka mtoto wake kufika alishindwa kutokana na hali ya usiku, Januari 25 Msangi alichukua dawa mbalimbali na kumeza, ndipo mkewe alipoiga simu kuomba msaada kwa ndugu zake (Msangi) na kwenda kutafuta maziwa, ndipo alipojifungia ndani na kujinyonga,"alisema jirani huyo.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu Kamanda Maigwa alisema wanaendelea na uchunguzi ili kubaini chanzo cha tukio hilo.

Alisema: "Kwa sasa nipo kwenye msafara, ila ni kweli tukio hilo limetokea la mstaafu kujinyonga nyumbani kwake alipokuwa akiishi maeneo ya Kiboliron, hatujui chanzo ila tunafuatilia ili kubaini chanzo."

Mmoja wa ndugu wa familia hiyo alidai kuwa wakati Msangi akiwa Dar es Salaam anapatiwa matibabu ya moyo, mwanafamilia huyo alitumia nafasi hiyo kuuza mali zake zote ikiwamo nyumba, mashamba na mali nyingine.

## Mbaroni tuhuma mauaji mjamzito

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

JESHI la Polisi mkoani Rukwa limemkamata na kumnasa Philipo Vincent (22) kwa tuhuma za kumuua kwa kumkata mapanga mjamzito na watoto wake wawili.

Jeshi hilo limesema wakati wa kumhoji, mtuhumiwa huyo alidai kuwa alikuwa anamdai mjamzito huyo gunia mbili za mahindi.

Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Rukwa, Theopista Mallya, alisema kuwa polisi walifanikiwa kumkamata mtuhumiwa huyo kwa kuwa alijaribu kujinyonga ndipo walimkamata, na walipomuhoji alisema kuwa anataka kujiua kwa kuwa hana amani baada ya kufanya mauaji hayo.

Mallya alisema walipomuhoji zaidi, alikiri kufanya mauaji hayo kwa kuwa alikuwa amemkopesha gunia mbili za mahindi na alipomdai alionekana kufanya ukaidi wa kumlipa.

Alisema kuwa mtuhumiwa huyo alipokuwa akienda kwa mwanamke huyo kudai fedha Sh. 100,000 alimjibu kuwa asimdai kwa nguvu kwa kuwa hakumlazimisha amkopeshe, kauli iliyomuudhi mtuhumiwa na kuamua kufanya mauaji hayo.

"Mtuhumiwa huyo alinunua panga jipya na kulinoa vizuri, na siku ya Januari 14 usiku alikwenda nyumbani kwa marehemu na kisha kufanya mauaji hayo na kutokomea," alisema Mallya.

Alisema polisi walipomuhoji sababu za kuwaua na watoto, alijibu kuwa aliamua kuwachinja kwa kuwa watoto hao walimuona wakati anamuua mama yao na pia wanamfahamu kwa kuwa mekuwa akienda katika nyumba hiyo mara kwa mara kudai fedha, hivyo wangemtaja.

Mapema wiki hii, jeshi hilo lilisema tukio hilo linadhaniwa kutokea usiku wakati mama huyo na watoto wake wakiwa ndani ya nyumba yao, kisha watu waliotekeleza mauaji hayo kuingia ndani.

Mallya alisema mume wa mwanamke huyo ambaye yuko Dar es Salaam alianza kumtafuta mkewe kwa kumpigia simu, lakini ilikuwa inaita bila kupokelewa.

Alisema alipopiga kwa muda mrefu simu hiyo ilizima, hali inayoonyesha kuwa ilizima kwa kuishiwa chaji na kila alipojitahidi kupiga haikupatikana.

Baada ya hapo alimpigia rafiki yake, Paul Leonard, na kumwagiza aende akaione familia yake na alifika nyumbani hapo saa 2:30 usiku na alishangaa kukuta mlango umefungwa nje kwa kufuli, hivyo aliamua kuwaita viongozi wa kijiji na walipofika na kubomoa mlango na kuingia ndani walikuta mwanamke huyo aliyekuwa na ujauzito wa miezi minane akiwa amechinjwa pamoja na watoto wake Milliam (8) na William (4).

## HABARI KITAIFA

## Washikiliwa tuhuma za kumuua bibi kizee

**Na Richard Makore,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mara linawashikilia watu sita kwa tuhuma za mauaji ya bibi kizee, mkazi wa Kijiji cha Rigicha, wilayani Serengeti na chanzo cha mauaji hayo kikidaiwa kuwa imani za kishirikina.

Tukio hilo lilitokea hivi karibuni na mke wa kijana wa marehemu akiwa miongoni mwa wanaoshikiliwa kwa tuhuma za mauaji hayo.

Pia katika tukio hilo waganga wawili wa kienyeji wanashikiliwa na polisi kwa kuhusishwa na mauaji hayo ya kinyama.

Kamamda wa Polisi Mkoa wa Mara, Longinus Tibushubwamu, akizungumzia tukio hilo alisema, watu hao wanatuhumiwa kumuua kwa kumkatakata kwa mapanga bibi huyo Wankuru Mwita (88), usiku wa manane.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Kija Juma (30) ambaye ni mke wa kijana wa marehemu, Mageni Itegwa (40) na Makeremo Paul (47), ambao ni waganga wa kienyeji na wakazi wa kijiji hicho.

Wengine ni Emmanuel Juma (38), Peter Masalu (45) na Manoni Sumaku (38), wote wakazi wa Rigicha na chanzo cha mauaji hayo ni bibi huyo kutuhumiwa kuwaroga wajukuu zake (watoto wa Kija) ambao wanadaiwa kuugua mara kwa mara.

"Huyu Kija ni mke wa kijana wa marehemu na mume wake yupo jela anatumikia kifungo cha miaka 20 kwa kosa la ujangili, sasa huyu binti ana watoto wanne ambao wamekuwa wakiugua mara kwa mara, huyu mtuhumiwa alikwenda kwa waganga wawili ambao wote walimwambia kuwa watoto hao wanarogwa na mama mkwe wake na anataka kuwaua," alisema Kamanda Tibushubwamu.

Alisema baada ya mtuhumiwa kuambiwa na waganga wote wawili, alikubaliana na mganga Itegwa kufanya mpango wa kutafuta watu wa kumuua bibi huyo na kwamba bila kufa lazima angewaua wajukuu zake.

"Mganga huyu ndiye aliyewatafuta hawa vijana watatu kisha kuwaosha na dawa kabla ya kwenda kuua na baada ya kuua walirudi tena kwake na kuwaosha na dawa ili wasiweze kukamatwa na polisi," alisema.

Kabla ya kufanya tukio hilo watuhumiwa hao walikubaliana kutekeleza jukumu hilo kwa malipo ya Sh. 500,000 wote kwa pamoja na kwamba walipewa Sh. 50,000 ili kuanza kazi hiyo.

Kamanda alisema, fedha hizo zilikuwa ni ruzuku aliyopewa mtuhumiwa Kija kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaotekelezwa na TASAF huku wakiahidiwa kumaliziwa kiasi kilichobaki cha Sh. 450,000, wakimaliza kazi hiyo.

Kamanda Tibushubwamu alisema kuwa watuhumiwa wote wamekiri kutenda kosa hilo na taratibu za kuwafikisha mahakamani zinaendelea.

Katika tukio lingine, mkazi wa kitongoji cha Burunga wilayani Serengeti, mkoani Mara, Daud Samuel amejinyonga hadi kufa baada ya wananchi kumdhibiti asiende nyumbani kwake kuchinja watoto wake wanne kwa madai ya kukimbiwa na mke wake.

# Takwimu za wagonjwa, vifo vya UVIKO sasa kutangazwa

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema kuanzia sasa itakuwa inatoa takwimu za wagonjwa wanaougua na vifo vinavyotokana na ugonjwa wa UVIKO-19 ili taarifa hizo zipimwe na jamii na kutambua umuhimu wa chanjo, ingawa ni hiari.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema hayo jana wakati serikali ilipopokea chanjo 800,000 kutoka Serikali ya China, aina ya Sinopham ambayo itatumika kuchanja watu 400,000 dozi mbili.

Alisema hadi sasa chanjo zilizokwishapokelewa ni 8, 821,210 ambazo zinatosha kuchanja Watanzania, 5,082,380 na kwamba hadi jana waliochanjwa ni 1,922,019 sawa na asilimia 3.33, tangu zilipoanza kutolewa mwaka huu aina ya Moderna, Jansen, Pfizer na Sinopham.

Waziri Ummy, alipokea chanjo hizo zilizokabidhiwa na Balozi wa China nchini, Chen Minjiang kwa niaba ya Serikali ya China.

"Hii ni awamu ya pili kupokea chanjo kutoka China, awali ilipokewa chanjo 500,000 aina ya Synopham iliyotumika kuchanja watu 250,000 kwa kuwa inachanjwa mara mbili. Mwitikio wa kuchanja bado ni mdogo nchini, matarajio ni kufikia asilimia 60 hadi mwishoni mwa mwaka huu.

"Chanjo ni salama na ni muhimu. Ninatoa wito kwa viongozi wa serikali, taasisi, dini kuendelea kutoa hamasa kwa Watanzania kuchanja, ili kujikinga na ugonjwa wa UVIKO-19," alisema Ummy.

Alisema ili kuongeza hamasa, kuanzia sasa serikali itakuwa inatoa takwimu za wagonjwa wanaougua, vifo kutokana na ugonjwa huo, ili taarifa hizo zipimwe na jamii na kutambua umuhimu wa chanjo, ingawa bado serikali inasisitiza ni suala hiari.

Awali Balozi wa China nchini, Chen Mingjian, alisema kwamba serikali yake itaendelea kuhakikisha chanjo zinafika barani Afrika ikiwamo Tanzania, ikiwa ni mkakati wa kukabiliana na ugonjwa wa UVIKO-19.

"Chanjo ndiyo silaha ya kukabiliana na ugonjwa huu ambao virusi vyake husambaa na kusababisha athari kiuchumi, dunia imeathiriwa. China itahakikisha nchi zinazoendelea zinapata chanjo," alisema Mingjian.

"Hii ni awamu ya pili kutoa chanjo kwa Tanzania baada ya ile ya kwanza 500,000. Tunatarajia hivi karibuni China kujipatia Tanzania chanjo milioni moja, pia tutaendelea kutoa uzoefu na ushirikiano namna ya kuikabili corona, ikumbukwe ripoti ya kwanza ya UVIKO-19 ilitokea China," alisema Mingjian.

Kadhalika, Mkurugenzi wa Idara ya Kinga, Wizara ya Afya, Dk. Beatrice Mutayoba, alisema Watanzania waondoe hofu kuhusu chanjo hizo, akisema usalama upo na muda wa matumizi kuisha ni kati ya miaka miwili na miezi nane kulingana na aina ya chanjo.

"Chanjo aina ya Synopham muda wake wa ku-expire ni miaka miwili, pia Pfizer muda wake ni wa miezi nane, hivyo hofu isiwepo watu wachanje," alisema Dk. Mutayoba.



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (kushoto), akipeana mikono na Balozi wa China hapa nchini, Chen Mingjian, wakati akipokea shehena ya chanjo 800,000 ya UVIKO-19 aina ya Sinopharm, baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

## Mjadala waibuka ofisa polisi kujiua mahabusu

**Na Mwandishi Wetu**

MJADALA umeibuka Ofisa wa Jeshi la Polisi mkoani Mtwara, Mrakibu Msaidizi wa Polisi Grayson Mahembe, aliyedaiwa kujinyonga kwa kutumia tambala la kudekia akiwa mahabusu ya kituo cha polisi.

Mahembe ni miongoni mwa maofisa wa polisi waliokuwa wakishikiliwa kwa tuhuma za mauaji ya mfanyabiashara wa madini, Mussa Hamisi (25), mkazi wa Kijiji cha Ruponda, Nachingwea mkoani Lindi yaliyotekelezwa Januari 5, mwaka huu.

Inadaiwa kuwa askari hao walimpora mfanyabiashara huyo wa madini Sh. milioni 70 kisha kumuua kwa kumchoma kwa sindano ya sumu na kumtupa katika kitongoji cha Majengo Kijiji cha Hiari wilayani Mtwara.

Baada ya mauaji hayo, Januari 22, mwaka huu, inadaiwa ofisa huyo wa polisi naye alikutwa amejinyonga akiwa mahabusu huku kitendo hicho kikizua mjadala kwenye mitandao ya kijamii na kuibuka maswali kadhaa.

Jana, kupitia mitandao ya kijamii, wananchi waliibua mjadala wakihoji kitendo cha mahabusu huyo kuwekwa tambala la kudekia.

Mwananchi mmoja katika mtandao wa Instagram alilitaka Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina kuhusiana na tukio hilo pamoja na aliyesababisha uzembe huo ndani ya mahabusu awajibishwe.

Mwananchi mwingine aliandika: "Chumba cha mahabusu hakitakiwi kuwa na kitu chochote ambacho kinaweza kusababisha mtuhumiwa kukitumia kama silaha ya kujidhuru. Iweje dekio hilo kuachwa humo?"

Mwingine alihoji nafasi aliyokuwa nayo askari huyo kituoni hapo na kitendo cha kuwekwa mahabusu ya kituo chake cha kazi huku mtumiaji mwingine katika mtandao wa tweeter akihoji wakati mahabusu huyo akiwa ndani ya chumba hicho, je, hakukuwa na watu wengine?

"Tunaomba kwa tukio hili tume huru ya uchunguzi iundwe kuchunguza kifo cha askari huyu. Kuna maswali mengi ya kujiuliza, tambara la kudekia mahabusu? Mazingira ya mahabusu yenyewe hakukuwa na watu wengine, kama kweli amejinyonga kuna siri gani nzito.

"Je, hakuna mazingira yanayoonyesha kunyongwa? Kama yapo nini kimejificha nyuma yake?" mwananchi mwingine aliandika mtandaoni.

Wakati huo huo, jana Jeshi la Polisi nchini kupitia msemaji wake, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) David Misime liliwataka watu wenye ushahidi wa ziada ambao utathibitisha kuwa kuna uhalifu mwingine watuhumiwa hao wameufanya, wafike kwa timu iliyoundwa kufanya uchunguzi wa mauaji ya mfanyabiashara huyo ili ushahidi uweze kuchukuliwa.

Misime alisema timu hiyo inaendelea kukamilisha uchunguzi chini ya usimamizi wa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) ili haki iweze kutendeka.

"Tunataka haki itendeke kwani yaliyodaiwa kufanywa na maofisa na askari hao si maelekezo ya Jeshi la Polisi bali ni matendo yao binafsi na tamaa zao za kutaka kujipatia fedha kinyume cha sheria, kanuni na taratibu za nchi," alisema Misime.

# TANGAZO

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

www.tcbbank.co.tz

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA(HESABU AMBAZO HAZIJAKAGULIWA)

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

## TANZANIA COMMERCIAL BANK PLC

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA, 2021

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | | Robo Mwaka /Mwaka wa 31/12/2021 | Robo Mwaka/Mwaka 30/09/2021 |
|---|---|---|---|---|
| A. | | **MALI** | | |
| | 1 | Fedha Taslimu | 49,972 | 41,873 |
| | 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 16,534 | 64,413 |
| | 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 133,175 | 112,814 |
| | 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 73,818 | 78,327 |
| | 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 284 | 435 |
| | 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| | 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| | 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| | 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 124,636 | 85,297 |
| | 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| | 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 718,600 | 681,988 |
| | 12 | Mali Nyingine | 44,907 | 46,632 |
| | 13 | Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| | 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| | 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 22,599 | 22,522 |
| | **16** | **JUMLA YA MALI** | **1,184,525** | **1,134,301** |
| B | | **DHIMA** | | |
| | 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 0 | 0 |
| | 18 | Amana za Wateja | 729,137 | 755,420 |
| | 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| | 20 | Amana Maalumu | 178,978 | 156,088 |
| | 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 3,988 | 1,300 |
| | 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | (0) | 2 |
| | 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 17,858 | 21,005 |
| | 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| | 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| | 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine | 2,429 | 2,456 |
| | 27 | Dhima Nyingine | 28,383 | 26,208 |
| | 28 | Madeni | 108,575 | 60,724 |
| | **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **1,069,349** | **1,023,203** |
| | **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **115,176** | **111,097** |
| C. | | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 28,072 | 28,072 |
| | 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| | 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 65,433 | 66,533 |
| | 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 11,238 | 8,402 |
| | 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 10,433 | 8,090 |
| | 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| | **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **115,176** | **111,097** |
| | 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 208,231 | 171,250 |
| | 39 | Mikopo Chechefu | 80,859 | 94,680 |
| | 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 15,554 | 24,238 |
| | 41 | Mali Nyingine Chechefu | 11 | 83 |
| D. | | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 9.72% | 9.79% |
| | (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 10.94% | 13.27% |
| | (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 101.34% | 94.46% |
| | (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 60.67% | 60.12% |
| | (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 80.66% | 79.86% |
| | (vi) | Ongezeko la Amana | -3.48% | 0.08% |
| | (vii) | Ongezeko la Mali | 4.43% | -3.58% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA, 2021

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Robo Mwaka ya sasa | Robo Mwaka iliyopita | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 31-Dec-21 | 30-Sep-21 | 31-Dec-21 | 31-Dec-20 |
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 4,786 | 3,057 | 19,879 | 21,008 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | - Hasara Katika Mali | 8,083 | 5,895 | 25,816 | 10,122 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (36,612) | (23,227) | (100,786) | (199,157) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | (1) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (3,392) | (56,179) | 116,199 | 360,908 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi | - | - | - | (91,189) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 1,687 | (8,357) | (7,627) | 22,131 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 1,724 | (490) | (3,087) | (17,717) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (1,950) | (2,189) | (8,640) | (7,819) |
| | - Mengineyo (bainisha) | 7,020 | 46,995 | (41,365) | 133 |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **(18,654)** | **(34,495)** | **388** | **98,421** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (3,725) | (1,361) | (8,549) | (4,710) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | 2 |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana | - | - | (8,549) | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(3,725)** | **(1,361)** | **(17,098)** | **(4,708)** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | 612 |
| | Mengineyo (bainisha) | (1,122) | (2,694) | (6,791) | (7,545) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | ***(1,122)*** | ***(2,694)*** | ***(6,791)*** | ***(6,932)*** |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (23,501) | (38,550) | (23,501) | 86,780 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **135,177** | **173,727** | **135,177** | **33,746** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 111,676 | 135,177 | 111,676 | 120,526 |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2021

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|
| | 31-Dec-21 | 31-Dec-20 | 31-Dec-21 | 31-Dec-20 |
| 1 Mapato ya Riba | 36.106 | 29.845 | 135.181 | 122.171 |
| 2 Gharama za Riba | (11.502) | (10.179) | (40.509) | (37.359) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | **24,605** | **19.666** | **94,672** | **84,811** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | (362) | (14) | (519) | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (3.311) | (3.033) | (13.649) | (8.420) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **9.432** | **11,948** | **34,503** | **32,740** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya | 1,636 | 1,600 | 5,561 | 2,339 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 5.403 | 4.135 | 18.732 | 19.828 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 2.392 | 6.213 | 10.210 | 10.572 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(25,578)** | **(29,389)** | **(95,127)** | **(88,123)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 11.572 | 11.198 | 45.988 | 40.802 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 1.261 | 5.314 | 4.615 | 399 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 12.746 | 12.877 | 44.524 | 46.921 |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **4,786** | **(822)** | **19,879** | **21,008** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 1.950 | 7.904 | 8.640 | 15.142 |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **2.836** | **(8.726)** | **11.238** | **5.866** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | **66** |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa** | **2.836** | **(8.726)** | **11.238** | **5.932** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 1.091 | 1.039 | 1.091 | 1,039 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 101 | (311) | 400 | 211 |
| 15 **Idadi ya Matawi** | 47 | 43 | 47 | 43 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.24% | -0.87% | 1.01% | 0.70% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 2.46% | -7.34% | 10.17% | 5.84% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 56.17% | 70.32% | 56.06% | 56.89% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.58% | 2.40% | 10.68% | 10.03% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.**

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2021

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | - | **66,533** | **(0)** | **0** | **9,694** | **104,299** |
| Mabadiliko ya mpito ya IFRS 9 | - | - | - | | | | - |
| Hamisho kwenda hifadhi ya kisheria | - | - | **(739)** | **739** | - | | - |
| Faida ya mwaka | - | - | - | - | - | 11,238 | **11,238** |
| Mapato mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Hifadhi ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hamisho kwenda/kutoka mapato yaliyohifadhiwa | - | - | (361) | - | - | - | **(361)** |
| Mengineyo | - | - | - | - | | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **28,072** | - | **65,433** | **739** | **0** | **20,932** | **115,176** |
| **Mwaka uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | - | **60,601** | **(0)** | **0** | **10,220** | **98,893** |
| Hamisho kutoka hifadhi ya udhibiti | - | - | - | - | - | - | - |
| Faida ya mwaka | - | - | 5,866 | - | - | - | **5,866** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | 66 | - | - | - | **66** |
| Hisa za ziada | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hasara ya sasa ya manufaa yaliyofafanuliwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Kurudishiwa Gawio lililosimamishwa | | | - | | | | - |
| Mengeineyo | | | | | | (526) | **(526)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **28,072** | - | **66,533** | **(0)** | **0** | **9,694** | **104,299** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA, 2021

Benki ililipa faini ya shilingi 1,000,000 kwa kuwasilisha taarifa sisizo sahihi katika riport ya fedha za kigeni zilizonunuliwa na kuuzwa.

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| **SABASABA K. MOSHINGI** (Ofisa Mtendaji Mkuu) | **Imesainiwa** | **24.01.2022** |
| **REGINA E. SEMAKAFU** (Mkuu wa Fedha) | **Imesainiwa** | **24.01.2022** |
| **SOSTHENES F. NYENYEMBE** (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | **Imesainiwa** | **24.01.2022** |

Sisi tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa Taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathimini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa Taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | |
|---|---|---|
| **DR. EDMUND B. MNDOLWA** ***Mwenyekiti wa Bodi*** | **Imesainiwa** | **24.01.2022** |
| ***MS. ANNE C. MBUGHUNI*** **Mjumbe wa Bodi** | **Imesainiwa** | **24.01.2022** |

tcbbank

Head Office, Millenium Tower II, 10th Floor, Kijitonyama Opp. Makumbusho Village,
P.O. Box 9300, Dar Es Salaam | Telephone; +255 22 216 2940
E-mail: info@tcbbank.co.tz | www.tcbbank.co.tz | Customer Care: +255 787 669977 | +255 788 767 683 | +255 658 767 683

TANGAZO

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

# MINIMUM DISCLOSURE OF RATES AND CHARGES

| BANK CHARGES | | |
|---|---|---|
| ITEM | FEE DESCRIPTION | TZS |
| Minimum Opening Balance | Quick Account | 20,000 |
| | Salary Account | FREE |
| | Tabasamu Individual | 10,000 |
| | Tabasamu Group Account | 50,000 |
| | Platinum Account | 15,000 |
| | Minor Account | 20,000 |
| | Group Account | FREE |
| | Scout Minor Account | 10,000 |
| | Scout Account | 30,000 |
| | Yanga VIP Account | 1,200,000 |
| | Yanga Members Account | 25,000 |
| | Wavuvi Account | 10,000 |
| | Current / Call Account | 100,000 |
| | Fixed Deposit Account | 100,000 |
| | WADU Account | 20,000 |

| PRODUCT NAME | MINIMUM OPENING BALANCE | MINIMUM BALANCE | MONTHLY MAINTANCE FEES |
|---|---|---|---|
| Business current account TZS | 100,000/= | 100,000/= | 20,000/= |
| Business current account USD | 100 USD | 100 USD | 20 USD |
| Personal current account TZS | 100,000/= | 50,000/= | 7,000/= |
| Personal current account USD | 100 USD | 100 USD | 5 USD |

| MAINTENANCE FEE | FEE DESCRIPTION | TZS |
|---|---|---|
| Personal Call Account | Per Month | 6,500 |
| Corporate Call Account | Per Month | 10,000 |
| **Savings Accounts** | | |
| Quick Account | Per Month | 1,560 |
| Salary Account | Per Month | 1,560 |
| Tabasamu Individual / Group Account | Per Month | FREE |
| Platinum Account | Per Month | 1,560 |
| WADU Account | Per Month | FREE |
| Minor Account | Per Month | FREE |
| Group Account | Per Month | FREE |
| Scout Junior Account | Per Month | FREE |
| Scout Senior Account | Per Month | FREE |
| Yanga VIP/ Members Account | | 1,560 |
| Yanga Members Account | | 1,560 |
| Wavuvi Account | | 1,560 |
| **Cash Deposit** | | |
| Over the Counter | Per Transaction | FREE |
| Popote Agents | Per Transaction | FREE |
| **Bank Statement** | Per Page | 2,000 |

| Balance Enquiry | | |
|---|---|---|
| Over the Counter | Per Enquiry | 300 |
| At the ATMs | Per Enquiry | 300 |
| At POS Branches | Per Enquiry | 150 |
| At Popote Agents | Per Enquiry | 100 |
| At TCB Popote Mobile Banking | Per Enquiry | 300 |
| Internet Banking | Per Enquiry | FREE |

| TRANSACTION | DESCRIPTION | TZS |
|---|---|---|
| Dormant Accounts | | |
| Activations | Per Activation | FREE |
| Dormant Account Fees | 1 year to 5 years | 1,300 |
| | 6 year to 10 years | 5,000 |
| | 11 year to 15 years | 10,000 |
| Closing of Account | | |
| All Accounts | Per Account | 13,000 or Equiv. in Foreign Currency |

| ATM CASH WITHDRAW | | |
|---|---|---|
| ITEM | DESCRIPTION | TZS |
| TCB ATMs | Per Transaction | 1,300 |
| Other Banks Umoja Switch ATMs | Per Transaction | 1,300 |

| OTHER ATM & NORMAL CARDS FEE | |
|---|---|
| TRANSACTION / ITEM | TZS |
| PIN Re - Issue | FREE |
| Collection of ATM Card at Non Domicile Branch | 6,500 |
| Uncollected and destroyed ATM Card | 6,500 |
| First ID Card ( Local and Foreign Currency ) | 4,000 |
| Replacement of ID Card | 2,600 |

| LENDING INTEREST RATES AND OTHER CHARGES | | |
|---|---|---|
| LOANS | CATEGORY | INTEREST RATE |
| Consumer Loans | Consumer Loan Administration Fee | 1.5% of the Approved loan. Minimum TZS. 10,000/= |
| Wastaafu Loans | Loan Application fee | TZS 10,000/= |
| | Loan Administration fee | 1.5% Minimum TZS. 10,000/= Maximum TZS. 100,000/= |
| Other Charges On Individual Micro Credit | MIC Loan Application fee | TZS 25,000/= |
| | MIC Loan Processing/ Administration fee | 1.5% Minimum TZS. 50,000/= |
| Interest Rates And Charges On Business Loan | Loan Application fee for Business and Personal loans | TZS. 50,000/= |
| | Loan Administration fee - Business and Personal loans | 1.5% of the Approved Amount. |

| TRANSACTION / ITEM | TZS |
|---|---|
| Goverment Securities Transaction Handling fees | 50,000/= |

| TRANSACTION | DESCRIPTION | TZS |
|---|---|---|
| Internet Banking Registration | Per Registration | FREE |
| TCB Popote Mobile Banking Registration | Per Transaction | FREE |

| FEES | | |
|---|---|---|
| TRANSACTION | DESCRIPTION | TZS |
| Transfers | TISS - Outward | 10,000 TZS |
| | EFT - Outward | 2,000 TZS |
| | EFT - In House | 1,500 TZS |
| Standing Order | Within the Bank | FREE |
| | To other Banks | 13,000 TZS |
| Other Transfers | Internal Transfer | FREE |
| Others | Salary Handling - Cheque list | 1,000 TZS |
| | Introduction letter to Embassy, etc | FREE |

| USD TRANSACTION FEES | | |
|---|---|---|
| TYPE OF CHARGE | TRANSACTION / ITEM | CHARGES IN USD |
| **Maintenance Fee** | Savings Account | 1 |
| | Call Account | 5 |
| **Deposit Fee** | Non Account Holder | FREE |
| **Opening Balance** | | 50 |
| **Bank Statement** | | FREE |
| **Bank Statement** | Balance Enquiry - Banking Hall | FREE |
| | Confirmation letter | FREE |
| **Withdraw fees** | Below 50 | 1 |
| | 51 - 1,000 | 2.5 |
| | 1,000 - 2,250 | 5 |
| | 2,251 - 5,000 | 15 |
| | Above 5,000 | 0.25 Percent |
| **Dormant** | Dormant Account Fee | 5 |
| | Re - Activation | FREE |
| **TISS** | | 10 |

| CASH WITHDRAWAL OVER THE COUNTER | | |
|---|---|---|
| ITEM | DESCRIPTION | TZS |
| **All Accounts** | Teller Withdraw up to 10,000,000 | 2,600 |
| | Teller Withdraw form 10,000,000 - 50,000,000 | 5,000 |
| | Teller Withdraw form 50,000,001 - 100,000,000 | 15,000 |
| | TellerWithdraw above 100,000,001 | 30,000 |




**Head Office:** 10th Floor - PSSSF Millenium Towers II, Bagamoyo Road, Kijitonyama, P.O Box 9300, Dar es Salaam, Tanzania.
**Telephone:** +255 22 2162940, **Email:** info@tcbbank.co.tz | **Website:** www.tcbbank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wiki ya Sheria ichochee mabadiliko kwenye jamii

**MAADHIMISHO** ya Wiki ya Sheria ambayo hufanyika kila mwaka yalizinduliwa Jumapili jijini Dodoma na Rais wa Zanzibar, Hussein Ali Mwinyi, huku viongozi wa mahakama ngazi zote nchini wakitoa ushauri kwa jamii.

Ushauri ambao mahakimu na majaji wameusisitiza ni kuwataka wananchi kuhudhuria katika maonyesho hayo ili wazijue sheria na taratibu za kufuata katika kutafuta haki zao.

Wiki ya Sheria ina umuhimu mkubwa kwa jamii, kwa sababu ni sehemu sahihi ya wananchi kwenda kupata elimu inayotolewa kwa ajili ya kuwapa elimu kuhusu wapi pa kwenda kutafuta haki pamoja na hatua muhimu zinazotakiwa kufuatwa.

Kuna migogoro mingi sugu katika jamii yetu ikiwamo ya ardhi, ndoa, mirathi na mingine ambayo inashindikana kupelekwa kwenye vyombo vya sheria hususan kwenye mahakama kutokana na watu kukosa uelewa. Kutokana na hali hiyo, na sisi tunawahimiza wananchi kwenda kupata elimu katika maeneo yaliyo karibu nao kabla ya maadhimisho hayo kumalizika ambapo yanafanyika maonyesho yakiambatana na elimu na ufafanuzi unaotolewa na wataalamu mbalimbali wa sheria wa serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayojihusisha na sheria pamoja na haki za binadamu.

Tunahimiza hilo kutokana na wananchi wengi kutokuwa na uelewa kuhusu wapi pa kwenda kupata haki na taratibu za kufuata, hivyo mwishowe kupoteza haki zao za msingi.

Ukosefu wa elimu hiyo pia umekuwa kichocheo kikuu kwa watu kuamua kujichukulia sheria mkononi, ikiwamo kufanya mauaji ya wengine na wakati mwingine kuamua kujiua.

Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu Tanzania, Musphafa Siyani, akizindua Mahakama ya Wilaya ya Chemba mkoani Dodoma juzi, alisema ni aibu wananchi kujichukulia sheria mkononi kwa kufanya mauaji ya kikatili, badala ya kutumia mahakama ili kupata haki zao na kuepusha migogoro inayosababisha vifo.

Mbali na kuwahimiza wananchi kwenda kujifunza pamoja na kuzitumia mahakama katika kudai haki, tunaona kwamba maadhimisho ya Wiki ya Sheria ni jukwaa muhimu la jamii kuzijadili sheria zetu, ili zile zisizoendana na wakati zifutwe hususan ambazo zinakwaza maendeleo na ustawi wa jamii.

Sheria za aina hii nyingi ni za zamani ambazo taifa lilizirithi kutoka kwa wakoloni na nyingine walizitunga wakati wa ukoloni kwa maslahi yao binafsi ili kuwasaidia kufanikisha utawala wao.

Hata Tume ya Jaji Francis Nyalali iliziainisha sheria 40 ilizoziita kandamizi na kupendekeza zifutwe ilipokuwa ikitafuta maoni ya wananchi kuamua kama Tanzania iendelee na mfumo wa chama kimoja cha siasa ama wa vyama vingi urejeshwe.

Sheria hizo nyingi bado zipo na zinaendelea kulalamikiwa na jamii, hivyo tunaona kwamba maadhimisho ya Wiki ya Sheria yawe jukwaa la kuzipigia kelele sheria hizo zifutwe, tukiunga mkono kauli ya Rais Mwinyi kuwa sheria nzuri ni kichocheo cha maendeleo ya uchumi wa nchi.

Kadhalika, tunakubaliana na wito wa kiongozi huyo kwa wanasheria Tanzania Bara na Zanzibar kuzipitia sheria zilizoko na kushauri zilizo kinzani kuboreshwa.

Bila shaka wanasheria watakuwa wameipokea changamoto hiyo na kuwa tayari kuifanyia kazi. Kwa upande mwingine, Tume ya Kurekebisha Sheria nayo tunaamini kwamba itatimiza wajibu wake wa kushauri sheria ambazo ni kinzani na zimepitwa na wakati kwa maendeleo ya nchi yetu.

Tunawashauri mahakimu na majaji kuendeleza kasi ya kushughulikia mashauri yaliyoko mahakamani ili wananchi wapate haki zao kwa wakati, ili wauone mhimili huo kuwa ni mahali sahihi pa kukimbilia kutafuta haki.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Shule zimefunguliwa, walimu mjihadhari na UVIKO-19

**TAYARI** shule za msingi na sekondari zimeshafunguliwa. Wanafunzi wote wawe wanaoenda na kurudi nyumbani au wa bwenini, kwa sasa wamerejea masomoni baada ya mwezi mmoja na siku kadhaa za mapumziko majumbani mwao.

Hivi karibuni nchi yetu ikiwa ni safu ya dunia, ilikumbwa na upepo mbaya, baadhi ya watu waliumwa homa kali, mafua na kukohoa, wakiwamo hata wachezaji soka kiasi cha mechi zao kuahirishwa. Wengine walicheza huku wakiwa wagonjwa. Hakuna anayejiamini kwa usalama sana.

Upepo huo mbaya unatetema tukiwa si kisiwa, nchi yetu imo katika orodha ya wanaokabiliwa na ugonjwa wa UVIKO-19. Viongozi wetu wa ngazi za juu wameonyesha dhamira ya kutaka kuupunguza, kama si kutokomeza kabisa nchini.

Wakati viongozi wakuu wakionyesha dhamira hiyo, huku chini watu wa kada mbalimbali wanatakiwa kuwaunga mkono. Ni juzi tu akizungumza na wawakilishi wa Machinga jijini Dar es Salaam, Rais Samia Suluhu Hassan, alikumbusha tusijisahau kihivyo.

Viwandani, maofisini, hata shuleni ni wajibu wa kila mmoja kutekeleza kanuni za kupiga vita ugonjwa huo ambao Watanzania tusithubutu kujidanganya kwamba umekwisha kabisa.

Ni kweli kwa sasa kuna nafuu kutokana na dhamira ya dhati ya viongozi wetu kufanya kila njia liwezekanalo, tukianza na kuukubali kwamba upo, halafu ndio tunaingia vitani kuikubali kwa njia mbalimbali.

Leo nipo upande wa walimu wote nchini, ambao ni wiki moja na nusu sasa wamewapokea mamilioni ya watoto toka pande zote za nchi. Ni lazima waweke tahadhari ya kutoambukizana, wasiambukize au kuambukizwa.

Kwa walimu na wanafunzi wanaohudhuria kutwa, yaani kwenda na kurudi, walimu wao wanatakiwa wawakumbushe kunawa mikono kabla na baada ya kula chochote, pia waweke ndoo za maji tiririka na sabuni, ili wanawe wanapoingia na kutoka madarasani.

Pia mgeni yoyote anayeingia katika himaya ya shule kiofisi, au kwa darasa lolote, ni lazima apitie mlolongo huo huo wa kinga ya Uviko.

Wale wa mabwenini, kunapaswa wawekewe utaratibu wa kuwapima wanafunzi wote ambao wamerejea, kwa vipima joto ili kuhakikisha hawana joto la lililozidi kawaida. Hapo ndipo wajumuike na wenzao.

Hiyo ni kwa sababu wanakaa pamoja, hawana kazi kubwa sana kama wale wa kila siku wanaoenda majumbani na kurejea kesho yake.

La hatari zaidi lipo kwa walimu wenyewe wanaotakiwa kuwa makini maradufu, kwa sababu wana nafasi kubwa zaidi ya kuwaambukiza wanafunzi kwa sababu wote wanarejea majumbani.

Wanafunzi wao inategemea kati ya mmoja na mwingine, kulingana na kama yuko bwenini au la, pia kama wa bweni anapopata ruhusa kutoka shuleni.

Kingine ni kwamba, ifikie wakati walimu shuleni waanze angalau kidogo kutoa somo kwa wanafunzi juu ya kujikinga na UVIKO-19, jambo linaloweza kuwafanya wanafunzi kuwa na uelewa mkubwa zaidi wa ugonjwa huo, jinsi ya kujikinga kuliko hali iliyoko hivi sasa.

Mara zote, kumfundisha mwanafunzi ni sawa na kuifundisha jamii, kwa sababu huwa wanarudi majumbani na kuwaelimisha wazazi, familia, ndugu na jamaa wa karibu.

Wanafunzi wanatoka kwenye familia mbalimbali, za wazazi walioelimika na ambao hawajapata bahati hiyo. Hivyo, wazazi huwasikiliza na kuwaamini zaidi watoto wanaosoma kila wanachokileta nyumbani hasa kikiwa chanya, wanakipokea kwa mikono miwili.

Kilichobaki kwa walimu ni sasa wachukue tahadhari zote za UVIkO-19 wanapokuwa na wanafunzi, pia ni wakati wa kuanza kutoa elimu darasani juu ya ugonjwa huo, jinsi ya kujikinga ikilengwa si kwa manufaa yao tu, bali dira ya kuifikia jamii nzima.

Tujitahidi walimu, mara zote mwanzo huanza na moja walimu!

# Luteni Urio adai kortini kukubali kumtafutia Mbowe makomandoo

**Na Kulwa Mzee**

SHAHIDI wa 12 katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, na wenzake watatu, Luteni Dennis Urio, amedai kwamba alikubali kumtafutia kiongozi huyo Mbowe makomandoo watakaomsaidia kuchukua dola.

Urio alidai hayo jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joachim Tiganga, wakati akitoa ushahidi kwa kuongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Abdallah Chavula.

Alidai kuwa alimfahamu Mbowe mwaka 2008, alipokutana naye mara ya kwanza na kwamba mwaka 2012 hakumbuki tarehe lakini alimwambia kuna kitu anataka waongee akataka waonane Hotel ya CASA iliyoko Mikocheni, Dar es Salaam.

Alidai kuwa alimwambia Mbowe kuwa hapajui Mikocheni, hivyo akamwambia akodi teksi impeleke na alifanya hivyo. Alidai kuwa alipofikishwa, Mbowe alilipa Sh. 20,000.

"Mbowe aliniambia anataka kujua msimamo wangu kuhusu vyama vya upinzani. Nilimjibu kwa nafasi yangu sitakiwi kufungamana na chama chochote ila kwa kiongozi aliyekuwapo madarakani.

Alidai waliachana jioni kati ya saa tisa mpaka 11:00 na walikutana tena Julai 2020 alimpigia simu akimwambia ana mambo muhimu anataka waonane na alifanikiwa kuonana naye.

"Nilimkuta peke yake kwenye mgahawa, aliniambia komredi mwaka huu wa 2020 (wakati huo) kuna uchaguzi mkuu na kwamba chama chake kimepanga kuchukua dola kwa gharama yoyote.

"Aliniambia unaona wanyonge wa hali ya chini wanaishi maisha ya shida, wakichukua dola sitakosa cheo cha juu. Aliniambia jeshini kuna wanajeshi waliostaafu au kufukuzwa, aliomba nimtafutie makomandoo wenye mafunzo hayo ambao ataambatana nao kuchukua dola.

Shahidi huyo pia alidai kuwa walikuwa wanataka kukata miti katika mikoa ya Mbeya, Kilimanjaro hasa Moshi, Arusha, Morogoro na Mwanza.

"Nilitafakari nikamkubalia. Mbowe ni ndugu yangu, tayari alishakuja na nia, nikatafakari huenda mimi plan B au C. nilimwambia anipe muda nimtafutie vijana, hakukuwa na idadi ni wale watakaopatikana. Nilipofika Mgulani nilimpigia DCI Kamishna (Robert) Boaz kumweleza niliyoambiwa na Mbowe. Nilishindwa kumeza,"alidai.

Awali, shahidi alidai anamfahamu mshtakiwa Halfani Bwire, alifanya kazi naye Kikosi cha 92 KJ Ngerengere na walikuwa na uhusiano tangu mwaka 2006 mpaka 2019 Bwire alipofukuzwa jeshi kwa utovu wa nidhamu.

Pia alidai anamfahamu mshtakiwa Adam Kasekwa, maarufu Adamoo kwamba, anafahamiana naye tangu mwaka 2012 alipofika 92KJ na kufanya kazi hadi 2018 alipoachishwa kwa utovu wa nidhamu.

Shahidi alikiri kumfahamu Mohammed Ling'wenya alifanya naye kazi 92 KJ tangu mwaka 2010 mpaka mwaka 2017 alipofukuzwa kazi kwa utovu wa nidhamu pia.

Alidai Bwire, Kasekwa na Ling'wenya wakati wa utumishi wao wa Jeshi 92 KJ makazi yao yalikuwa Chalinze Ngerengere.

Shahidi alidai mwaka 2008 alifahamiana na Mbowe, lakini hakumbuki tarehe alimpigia simu kwenye namba 0754612518 huku yeye alimpigia kwa kutumia mtandao wa Airtel ila namba yake hakumbuki.

Anadai alipiga akauliza yeye ni Denis Urio, akamwambia ndiyo yeye alimfahamu kwa kuwa alikuwa anaonekana kwenye vyombo vya habari.

Washtakiwa katika kesi hiyo wanatuhumiwa kula njama kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei Mosi hadi Agosti 5, 2020.



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF KIBAHA

*(AT KIBAHA)*

CRIMINAL CASE NO. 92 OF 2021.

THE REPUBLIC

VERSUS

HJ FIBRE INVESTMENT (TANZANIA) CO. LTD.........................................ACCUSED PERSON

To:

Managing Director
HJ Fibre Investment (Tanzania) Co. Limited
Pingo Area, Chalinze District
**Pwani Region**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 3rd day of February 2022 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 18th day of JANUARY **2022**

**RESIDENT MAGISTRATE**

RESIDENT MAGISTRATE
KIBAHA COAST

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me/us:**
Name..........................................
Signature......................................
Qualification/Relationship
Date...........................................



## PM ataka Watanzania kuipa hadhi Tanzanite

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka Watanzania kushirikiana na kushikamana ili kuyapa thamani madini ya Tanzanite na kuifanya dunia itambue kuwa madini hayo yanapatikana Tanzania pekee na tayari imeweka mazingira ya kuyaongezea thamani.

Majaliwa aliyasema hayo jana alipozungumza na wananchi katika eneo la EPZA unapojengwa Mji wa Tanzanie katika Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro.

Alisema serikali itahakikisha rasilimali zote zilizoko nchini yakiwamo madini ya Tanzanite zinawanufaisha wananchi wote hususani wanaoishi katika maeneo zinapopatikana.

"Watanzania lazima tushirikiane na tushikamane kuyapa thamani madini hayo," alisema.

Alisema serikali itaendelea kukutana na wafanyabiashara wa sekta madini kwa lengo la kuhakikisha kwa pamoja wanaweka mikakati ya kusaidia kuikuza sekta hiyo ili iendelee kuleta tija kwa Watanzania na taifa kwa ujumla.

Majaliwa aliwasisitiza wananchi waendelee kufanya biashara hiyo ambayo ina manufaa makubwa kwao na taifa kwa ujumla na serikali ipo tayari kuwahudumia wakati wote. "Tumejipanga kuwahudumia iwe wakati wa jua au wakati wa mvua."

Naibu Waziri Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, amemwahidi Waziri Mkuu kuwa watahakikisha wanasimamia ujenzi wa eneo hilo ili liweze kukamilika kwa wakati na kuanza kutoa huduma iliyokusudiwa kwa Watanzania wenye nia ya kuwekeza.

# TAKUKURU yazuia ujenzi madarasa chini ya kiwango

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), mkoani Shinyanga imezuia ujenzi wa vyumba vya madarasa kujengwa chini ya kiwango.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani humo, Hussein Mussa, alibainisha hayo jana wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, kwa kipindi cha robo ya pili ya mwaka wa fedha (2021-2022) kuanzia Oktoba hadi Desemba 2021.

Alisema walifanya ufuatiliaji wa ujenzi wa vyumba vya madarasa 60 yaliyojengwa kwa fedha za mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano ya UVIKO-19, yenye thamani ya Sh. bilioni 4.085, awali madarasa hayo ilikuwa yajengwe chini ya kiwango, lakini wakadhibiti.

"TAKUKURU Shinyanga tulifanya ufuatiliaji wa ujenzi wa vyumba vya madarasa za fedha za UVIKO-19, katika madarasa 60 ili kuhakikisha fedha zilizotolewa kwa ajili ya miradi hiyo zinatumika ipasavyo, ili kuendana na thamani halisi ikilinganishwa na fedha iliyotolewa," alisema Mussa.

"Mapungufu tuliobaini awali katika ujenzi huu wa vyumba vya madarasa, ikiwamo utumiaji wa matofali ambayo yapo chini ya kiwango, tuliyadhibiti na kutoa maelekezo yaliyofanyiwa kazi, na sasa madarasa yamekamilika na yanatumika, lakini bado tunaendelea na uchunguzi wa madarasa mengine," aliongeza.

Aidha, alisema walifanya pia uchunguzi kwenye miradi mingine miwili ya rasilimali kilimo yenye thamani ya Sh. milioni 41.4 inayotekelezwa katika Kata ya Mwamalili Manispaa ya Shinyanga na Pandagichiza wilayani Shinyanga.

Katika hatua nyingine alisema walipokea taarifa za rushwa 42, na kubainisha idara zilizolalamikiwa ni serikali za mitaa taarifa 16, ardhi (9), biashara (6), elimu (2), maji (2), Uhamiaji (2), polisi (2), madini (1), vyama vya ushirika moja na sekta binafsi.

Alisema kati ya taarifa hizo, tisa uchunguzi wake unaendelea, 11 zimefungwa kwa kukosa ushahidi, mbili zilihamishiwa idara nyingine, huku taarifa 22 hazikuhusiana na masuala ya rushwa na kubainisha kesi 23 zinaendelea mahakamani..

# Wazazi waamua kuwalinda watoto

**Na Shaban Njia, SHINYANGA**

WAZAZI na walezi wa vijiji vitatu vya Kata ya Puni, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, wamekubaliana kuwasindikiza watoto wao wa kike katika maeneo ya minada na magulio ili kuwalinda dhidi ya wanaume wanaowafanyia vitendo vya kikatili ikiwamo kuwabaka na kuwalawiti.

Lengo la kuweka makubaliano hayo ni kuhakikisha mtoto wa kike anasoma na kuhitimu masomo yake katika hali ya usalama baada ya kubaini siku za magulio na minada kunafanyika vitendo viovu dhidi ya watoto wao na kusababisha kukatisha masomo yao. Kadhalika wamepitisha sheria ndogo za vijiji ambayo kuanzia sasa hakuna ndoa yoyote itakayofungwa katika vijiji vyao bila uongozi wa serikali za vijiji na kata kufahamu ili kujiridhisha kama mtu anayefunga ndoa ana umri unaotakiwa kisheria.

Wazazi hao walitoa kauli hiyo jana walipozungumza na gazeti hili katika vijiji hivyo wilayani Shinyanga.

Lengo la ziara hiyo ni kutaka kujua mila na desturi zinavyochangia ukatili wa kijinsia chini ya mradi wa nafasi ya vyombo vya habari katika kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, unatokelezwa na SPC kwa ufadhili wa Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT).




# Madiwani wakerwa kuitwa 'mizigo'

**Na Neema Sawaka, KAHAMA**

BARAZA la Madiwani katika Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga limekerwa na kauli walizodai kuwa ni kejeli zinazotolewa na wananchi kwa kuwaita madiwani 'mizigo' katika mitandao ya kijamii.

Madiwani hao wamejitetea wao sio mizigo kama wananchi wanavyowaita kwa kuwa wamefanya mambo mengi yanayohusiana na maendeleo.

Hayo yalisemwa juzi na diwani wa kata ya Majengo, Bernard Mahongo, katika kikao cha Baraza la Madiwani kilichokaa kwa lengo la kupitisha mapendekezo ya bajeti kwa kipindi cha mwaka 2022/2023.

Mahongo alisema kuwa wanakaa na makabrasha zaidi ya wiki wakiyapitia na kurekebisha panapohitaji marekebisho na kuongeza kuwa maendeleo ya Kahama hayafanywi na mtu mmoja ambaye ni Mkurugenzi wa manispaa husika pekee.

Aidha, alisema madiwani wamechoka kuitwa 'mizigo' na kutukanwa katika mitandao ya kijamii ambayo inajiita Kahama Political kwa kuwa katika wilaya hiyo wamefanya mambo mengi ya maendeleo ambayo yameleta manufaa kwa wananchi.

Mahongo aliomba wananchi kuwaheshimu na Mkurugenzi anapokuwa akisifiwa kwa kufanya maendeleo aseme kuwa hayupo peke yake bali nyuma yake kuna madiwani ambao ndiyo wamefanya kazi kubwa.

Kwa upande wake, Diwani wa Kata ya Kahama mjini, Hamidu Kapama, alisema katika mapendekezo ya bajeti ya mwaka huu, nguvu kubwa ielekezwe katika upatikanaji wa dawa Hospitali ya Manispaa ya Kahama kwa kuwa tatizo hilo ni kubwa kwa sasa.

Alisema kuwa katika bajeti hiyo wajikite kuhakikisha kuwa dawa zinapatikana katika hospitali ya manispaa kutokana na suala hilo kuwa tatizo kwa wananchi.

Kwa upande mwingine, diwani huyo alilalamikia kitengo kinachohusika na mikopo katika manispaa hiyo kwa kuchelewesha kuitoa kwa makundi yanayohitaji.

Alisema kuwa watu wanaomba mikopo na kukaa zaidi ya miezi sita hadi mwaka bila majibu ya moja kwa moja yanayotolewa na Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa wananchi ili kufahamu kinachoendelea kimaendeleo.

Katika kikao hicho, Manispaa ya Kahama imepitisha Sh. bilioni 47.5 kwa kipindi hicho katika kuendesha shughuli mbalimbali za maendeleo.

Akiwakilisha mapendekezo hayo mbele ya Baraza la madiwani wa Manispaa ya Kahama, Ofisa Mipango wa Manispaa hiyo, Flora Sangiwa alisema, Sh. bilioni 9.03 ni mapato ya ndani, Sh. bilioni 26.6 itatumika kama mishahara ya watumishi, Sh. bilioni 1.3 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 10.5 kwa ajili ya miradi ya maendeleo..

## Wizara yaipa NCT bil. 1.2/- mafunzo utalii

**Na Christina Mwakangale**

WIZARA ya Maliasili na Utalii imetoa shilingi bilioni 1.2 kwa Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT), kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa watoa huduma katika sekta ya utalii na ukarimu.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NCT, Dk. Shogo Mlozi, aliyasema hayo kwenye mahafali ya 19 ya chuo hicho kwa wahitimu 541 wa fani mbalimbali, ngazi ya astashahada na stashahada.

Alisema, mafunzo hayo yatatolewa kwenye mikoa minane ya Mbeya, Mtwara, Njombe, Mara, Lindi, Ruvuma, Iringa na Mwanza, yatakayoanza Februari, mwaka huu.

"Mafunzo haya yatatolewa kupitia Mpango wa Maendeleo na Ustawi wa Taifa wa Mapambano dhidi ya ugonjwa wa UVIKO - 19.

"Lengo la mafunzo haya ni kuongeza uwezo wa kutoa huduma bora kwa watalii wanaokuja kutembelea Tanzania kuona vivutio vyetu vya utalii na kupambana na corona," alisema.

Alisema chuo hicho kitahakikisha wafanyakazi wake wanazingatia weledi katika kutoa mafunzo ili kusaidia watoa huduma katika sekta ya utalii na ukarimu kufikia kiwango cha juu cha weledi katika kutoa huduma zilizo bora.

"Chuo cha Taifa cha Utalii ni chuo pekee cha umma kilichopo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii chenye dhamana ya kutoa mafunzo ya ukarimu na utalii.

"Pia kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu na kufanya tafiti mbalimbali katika fani ya ukarimu na utalii," alisema Dk. Mlozi.

Alisema kwamba, hadi sasa chuo kina kampasi nne katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha na kati ya hizo, kampasi mbili zinatoa mafunzo ya ukarimu na mbili, Temeke na Mwanza, zinatoa mafunzo ya utalii katika ngazi ya Stashahada na Astashahada.

# Jamhuri yataka kesi kupinga Job Ndugai kujiuzulu itupwe

**NA KULWA MZEE**

WAKILI Mkuu wa Serikali, Gabriel Malata, ameiomba Mahakama Kuu kutupilia mbali kwa gharama shauri la kikatiba lililofunguliwa na Mwenyekiti wa NCCR-Mageuza, James Mbatia, dhidi ya aliyekuwa Spika wa Bunge, Job Ndugai na wenzake, kwa madai halina mashiko na halikupaswa kufunguliwa Kikatiba.

Hayo yalidaiwa jana mbele ya jopo la majaji watatu, Jaji John Mugeta, Benhaji Masoud na Sedekia Kisanya wakati upande wa Jamhuri ukiwasilisha hoja mbili za kupinga shauri hilo kusikilizwa.

Akiwasilisha hoja za pingamizi, Wakili Malata alidai Januari 20, mwaka huu mleta maombi Mbatia alifungua shauri la kikatiba, wajibu maombi namba 2, Katibu wa Bunge na mjibu maombi namba tatu Mwanasheria Mkuu wa Serikali waliwasilisha majibu ya madai na majibu ya hati ya kiapo kinzani kama mahakama ilivyoelekeza.

Alidai katika maombi hayo kumeibuka hoja mbili za kisheria za kupinga maombi hayo ambapo hoja ya kwanza mleta maombi alikuwa na njia nyingine ya kufungua shauri hilo na si kufungua shauri la kikatiba na hoja nyingine maombi yana upungufu wa kisheria.

"Madai ya msingi kwenye shauri hili inadaiwa Ibara ya 149(1c) imekiukwa mdaiwa wa kwanza Job Ndugai alipeleka barua ya kujiuzulu CCM wakati alitakiwa kutoa taarifa hiyo Bungeni, na kwa kufanya hivyo alikiuka Ibara ya 149

"Wanaomba amri ya kutengua kujiuzulu kwa spika na itoe amri kwamba Ndugai bado ni spika wa Bunge," alidai Malata.

"Kufungua shauri la kikatiba lazima hilo suala liwe linaleta mgogoro wa kikatiba na ili mleta maombi afanikiwe kufungua shauri la kikatiba na kusikilizwa anatakiwa aonyeshe na kuthibitisha hakuna njia nyingine ya kushughulikia shauri hilo.

"Mleta maombi alishindwa kuonyesha hakuna njia nyingine, mahakama haiwezi kusimama kusikiliza shauri hilo, tunaomba shauri hili litupwe kwa sababu masharti hayakuzingatiwa.

"Maombi hayana msingi mleta maombi alipaswa kuthibitisha hilo shauri kama ni la kikatiba na hakuna namna nyingine ya kulishughukia, tunaomba litupwe kwa gharama,"alidai Malata.

Mleta maombi, Daimu Halfani akijibu alidai upande wa Serikali wanaona shauri hilo linaweza kusikilizwa kwa njia nyingine ya kufanyiwa marejeo lakini mleta maombi analalamikia kukiukwa kwa Ibara ya 149(1c) ya Katiba .

Anadai masuala yoyote ya ukiukwaji wa Katiba hayawezi kufanyiwa marejeo badala yake yanashughulikiwa kwa kufungua shauri la kikatiba.

,"Katiba haijaruhusu ukiukwaji wa Katiba ushughulikiwe kwa njia nyingine nje ya kufungua shauri la kikatiba mahakamani," alidai Halfani.

Wakili Halfani aliomba hoja za kupinga maombi zisizingatiwe kwa sababu hazina mashiko hivyo aliiomba mahakama iendelee kusikiliza shauri la kikatiba.

Awali Wakili Halfani aliifahamisha mahakama kwamba mjibu maombi namba moja, Ndugai hawakufanikiwa kumpa hati ya wito, muhudumu waliyemtuma apeleke nyumbani kwake hakufanikiwa kumpata.

Anadai walifika Bungeni kwa Katibu wake wa zamani ambaye aliwapa namba ya simu, walimpigia hakupokea na walimtumia hati hiyo kwa njia ya email.



Mwenyekiti wa Chama cha NCCR-Mageuzi, James Mbatia (wapili kulia), akizungumza na mawakili wake katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam jana, wakati alipokwenda kusikiliza kesi aliyoifungua ya kupinga mchakato wa kujiuzulu kwa aliyekuwa Spika wa Bunge, Job Ndugai. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Makamba awa mbogo kukatika kwa umeme

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imeonyesha kutoridhishwa na tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara na kulitaka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kutojificha nyuma ya mgongo wa waziri huku ikidai kuwa imeanza kuchukua hatua za haraka kuhakikisha changamoto hiyo inatatuliwa.

Akizungumza jana mkoani Arusha, Waziri wa Nishati, January Makamba, wakati alipotembelea kituo cha kupoza umeme kilichoko Njiro mkoani hapo, aliagiza hatua za haraka zichukuliwe kwa watendaji ambao ni wazembe ndani ya shirika hilo ikiwa ni pamoja na kuwawajibisha.

Alisema kumekuwa na changamoto kwa TANESCO katika kuwasiliana na wateja wake umeme unapokatika ghafla na kwamba hali hiyo imekuwa ikisababisha malalamiko mengi na lawama kwa serikali.

"Sisi kama serikali hatufurahishwi na malalamiko ya wananchi kuhusu kukatika kwa umeme pamoja na upungufu wa taarifa zitolewazo kwa wateja, hii ni changamoto umeme unapokatika, hivyo ni lazima TANESCO iwasiliane na wateja wao kwa wakati," alisema Makamba.

"Kazi hii ya umeme serikali tumelikabidhi shirika hili na ndilo lina wajibu kwa sababu tumelisaidia, tumeliwezesha linawajibu wa kuifanya hii kazi kwa ufanisi na kwa namna ambayo wateja wataridhishwa," alisema Makamba.

Aliongeza kuwa wanafahamu kwamba kuna changamoto za muda mrefu za uchakavu wa miundombinu ya usambazaji wa umeme, kituo hicho kimejengwa tangu mwaka 1983 na kuna baadhi ya vifaa viliwekwa kipindi hicho ambavyo vinatumika hadi sasa.

"Nyakati nyingine kutokana na uchakavu wa miundombinu hata inaponyesha mvua kidogo tu wananchi wanasema TANESCO itakata umeme kumbe shida ni miundombinu, kwa hiyo sasa tunajizatiti kuhakikisha matengenezo makubwa na ya haraka yanafanyika kurekebisha mfumo mzima wa usambazaji umeme nchini," alisema Makamba.

Aidha, alibainisha kwamba serikali inakusudia kubadilisha mfumo wa teknolojia ya LUKU ndani ya miezi 18 kuanzia sasa ambao utawawezesha wateja kununua umeme kwa njia ya simu ya mkononi na kuingia moja kwa moja bila kuweka tokeni.

Alisema ifikapo mwezi Juni mwaka huu zaidi ya wateja 80,000 wataunganishiwa umeme, huku akibainisha kuwa serikali inatarajia kubadilisha mfumo wa maombi ya umeme ambao utakuwa ukifanyika kwa njia ya mtandao.

Pia alisema serikali inakusudia kubadilisha mfumo wa usambazaji wa umeme kote nchini ili uendane na kasi ya ongezeko la wateja, kuwa uliopo kwa sasa ni wakizamani.

HABARI KITAIFA

# Mgodi wapunguza kiwango cha tope sumu

**Na Mwandishi Wetu,** MUSOMA

MGODI wa dhahabu wa North Mara umefanikiwa kupunguza majitaka kutoka mita za ujazo 7,000,000 hadi 800,000 kiwango ambacho ndicho kinakubalika.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, apotembelea mgodi huo kuangalia hali ya utunzaji wa mazingira.

Alisema hiyo ni hatua kubwa kimazingira na NEMC inafurahishwa na namna mgodi wa North Mara ulivyotunza na kuhifadhi mazingira eneo la mgodi tangu uanze kumilikiwa na kampuni ya Barrick.Mgodi huo unamilikiwa na Kampuni ya Twiga ambayo ni mbia baina ya Barrick na serikali ya Tanzania.

Dk. Gwamaka alisema mgodi huo umefanikiwa kwa kiwango kikubwa kudhibiti hali ya uchafuzi wa mazingira ambao umekuwa tatizo kubwa kwa miaka mingi kabla haujachukuliwa na mwekezaji mpya.

Alisema awali kulikuwa na maeneo hatarishi ambapo baadhi ya mimea ilianza kukauka kutokana na uchafuzi wa mazingira, lakini sasa mimea hiyo imeanza kuchipua kama kawaida.

"Linalotia faraja zaidi ni kwamba Barrick imewekeza kwenye mtambo mkubwa wa kutibu maji machafu. Kuna kiasi cha mita za ujazo 40,000 zinatibiwa eneo la mgodi hii ni habari njema sana," alisema.

Pia alisema kuna maji mita za ujazo 12,000 za chumvichumvi ambayo yamechujwa kwenye maji ambayo yanaweza kwenda kutumika kwa matumizi mengine ya jamii.

Alisema kulikuwa na bwawa lenye tope sumu lenye mita za ujazo 7,000,000 ambalo lilikuwa tishio kwa mazingira na viumbe hai, lakini mita za ujazo zimepungua hadi 800,000 na kwamba wameahidi kuendelea kupunguza hadi kufikia mita za ujazo 50,000.

"Tunaamini kabisa kwa hizi juhudi kama wataendelea kufanya hizi kwa kasi hii uchafuzi wa mazingira kwenye maeneo haya utakuwa ni historia," alisema Dk. Gwamaka.

Naye Redempta Samuel, Mkurugenzi wa Utekelezaji wa Sheria NEMC, alisema ziara hiyo ilikuwa `maalum kwa ajili ya kuangalia utekelezaji wa maagizo waliyoyatoa kwa mgodi.

"Kwanza niwapongeza maana mgodi huu tangu uchukuliwe na Barrick umetunza mazingira kwa kiwango kikubwa sana na wamejenga mtambo wa kusafisha majitaka yote yanayozalishwa na mgodi sisi tunaona hii ni hatua kubwa," alisema.




Ofisa Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Biashara ya DCB, Adelah Kaihula (kulia), akikabidhi zawadi ya pesa kwa mmoja wa washindi wa kampeni ya Sinia la DCB, Winston Jacob, jijini Dar es Salaam jana. Kampeni hiyo ya miezi mitatu, ina lengo la kudumisha utamaduni kwa wateja kujiwekea akiba na pia kuwa sehemu ya shukurani za benki hiyo kwa wateja wao, zawadi zikiwa pesa na simu za mkononi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mchezaji mahakamani Kwa tuhuma za kumbaka mtoto

**Na Mwandishi Wetu**

MCHEZAJI wa zamani wa Klabu ya Simba, Uhuru Seleman Mwambungu (30), amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Temeke akikabiliwa na kesi ya kubaka mtoto.

Mchezaji huyo alisomewa shtaka lake juzi alasiri katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Aziza Mbadjo.

Wakili wa Serikali, Sabina Ndunguru alidai kuwa Aprili 13, 2021 Chang'ombe kota za Jeshi la Polisi, alimbaka mtoto wa kike.

Mshtakiwa alikana shtaka hilo.

Hakimu alisema mshtakiwa atakuwa nje kwa dhamana kwa kuwa na wadhamini wawili watakaotia saini hati ya dhamana ya shilingi milioni tatu.

Mshtakiwa alidhaminiwa na mama yake mzazi na kaka yake.

Ndunguru alidai upelelezi wa kesi hiyo umekamilika aliomba mahakama kupanga tarehe ya kusikiliza maelekezo ya awali.

Hakimu Mbadjo alisema mshtakiwa atakuwa nje kwa dhamana, kesi hiyo itasikilizwa maelezo ya awali Februari 10, mwaka huu.

Wakati huohuo, Abdallah Makuka (25), amefikishwa mahakamani hapo akikabiliwa na shtaka la unyang'anyi wa kutumia silaha.

Ilidaiwa kuwa Januari 6, 2022 eneo la Mbande aliiba pikipiki yenye namba za usajili MC 233 CXX aina ya Boxer mali ya Latifa Kumboka.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa alimtishia Sudi Ally kwa panga na kisu na kufanikisha wizi huo.

Mshtakiwa alikana shtaka hilo amerudishwa mahabusu mpaka Februari 9, 2022 kesi hiyo itakaposikilizwa maelezo ya awali.

# Sheria ya ndoa yatajwa kikwazo dhidi ya ukatili

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SHERIA ya Ndoa ya mwaka 1971, imeelezwa kuendelea kuwa kikwazo kwa wanafunzi wa kike mkoani Shinyanga katika kutimiza ndoto zao kutokana na kuozeshwa na wazazi wao katika umri mdogo.

Sheria hiyo inaruhusu mwanafunzi chini ya umri wa miaka 14 kuolewa kwa ridhaa ya wazazi wake na miaka 15 chini ya mahakama, hatua ambayo imetajwa kusababisha baadhi ya wanafunzi ambao wanaingia kidato cha kwanza mwaka huu wilayani Shinyanga, kuzuiwa na wazazi kwenda shule kwa lengo la kuozeshwa ili wapate mifugo.

Mratibu wa Dawati la Jinsia kutoka Jeshi la Polisi wilayani Shinyanga, Brighton Rutajama, alibainisha hayo juzi kwenye kikao cha Shirika la Women Elderly Advocacy and Development Organization (WEADO) la mkoani Shinyanga, ambalo linatetea haki za wanawake na watoto, wakati wakitambulisha mradi wa kutokomeza matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika Kata ya Masengwa.

Alisema sheria hiyo inapaswa ifanyiwe marekebisho haraka ili kumaliza kabisa tatizo la wanafunzi wa kike kukatishwa ndoto zao na wazazi wao kwa kuozeshwa ndoa za utotoni kwa tamaa ya kupata mali na mifugo.

"Hivi karibu katika Kata ya Pandagichiza wilayani Shinyanga, mwanafunzi ambaye amefaulu kujiunga na kidato cha kwanza, baba yake alimzuia kwenda shuleni akitaka kumwozesha ili apate mifugo. Lakini bahati nzuri mwanafunzi huyo alikimbilia kwa mtendaji kutoa taarifa ndipo ikawa pona yake na sasa anaendelea na masomo," alisema Rujama.

"Baada ya sisi polisi kupewa taarifa na kufika kijijini hapo, mzazi alikimbilia kusikojulikana na tumemfungulia kesi ya kutishia kuuwa sababu alimwambia mtoto huyo kuwa kwa vile amegoma kuolewa basi atamuua. Kuna visa vingi tu vya namna hiyo vya wanafunzi kuzuiwa kwenda shuleni lakini hatujaletewa taarifa kwa sababu sisi tunafanyia kazi taarifa," aliongeza.

Naye Mtendaji wa Kata ya Masengwa, Hussein Majaliwa, alisema tatizo la wazazi kuozesha wanafunzi ndoa za utotoni hasa wale waliofaulu kuendelea na masomo ya sekondari limekuwa sugu. Kwenye kata hiyo kuna wanafunzi wawili nao walizuiwa na wazazi wao kwenda shuleni ili waolewe.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wilayani Shinyanga, Joram Magana, alisema ukinzani wa sheria kuhusu ulinzi wa mtoto, umeendelea kuwa mwiba kuchochea matukio ya ukatili wa kijinsia na kusababisha watoto wa kike kuendelea kuozeshwa ndoa za utotoni na kuzima ndoto zao.

Ofisa Miradi wa WEADO, Salome Shangali, alisema mradi ambao wanautekeleza kwenye kata hiyo kwa ufadhili wa Mfuko wa Ruzuku wa Wanawake Tanzania (WFT) wenye thamani ya Sh. bilioni 12.4 na watakuwa wakitoa elimu kwa jamii kuachana na vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto.

ALHAMISI JANUARI 27, 2022
AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 14

JIJI TANGA BINGWA USAFI KITAIFA...

**Meya: Ni mwanzo, tumepaniakushika rekodi kwa miaka 10**



Ukurasa 12

Maji ya bahari kuvamia ufukweni kunavyoua mashamba mboga Z'bar



Ukurasa 13

Asasi ya kijamii yajitosa kampeni ya chanjo Uviko 'nyumba hadi nyumba'

## KITENDAWILI USALAMA:

# Mtihani mauaji jamii yanavyorindima kifamilia, mikasa mipya kwa watoto

**Na Zawadi Ramadhan,** SJMC

KADRI siku zinavyosonga, katika jamii kumekuwapo changamoto za jinai hata kufikia mikasa ya vifo katika jamii na familia, baadhi yake ni misugano kati ya wazazi kuhusu maudhui ya kifamilia.

Hivi karibuni kumesikika wazazi wakichukua uamuzi wa kutoa uhai wa mtoto au watoto kutokana na ugomvi au kutoelewana na mzazi mwenziwe.

Huyo mdhurika, ambaye kwa tafsiri ya Sheria ya Watoto ya Mwaka 2009 ni yeyote mwenye umri chini ya miaka 18, anabaki kuonewa pasipo kujua chochote kutoka kwa wazazi au walezi, anakatiliwa hata kufikia ama kudhurika au kupoteza maisha.

Ukatili huo, kimsingi unaangukia tafsiri ya jinai, ambayo mwanasheria na wakili wa kujitegemea, Manace Ndoroma, analifafanua kwamba: "Ni tendo lolote ambalo limekatazwa kwa sheria, ambalo mtu yeyote akilitenda anakuwa ameikosea Jamhuri ya Muungano wa Tanzania."

Wakili huyo ana ainisha "kosa lolote la jinai linakamilishwa na vitu viwili; tendo lenyewe lililokatazwa na nia ovu ya kutekeleza tendo hilo."

Ikirejewa maana ya 'familia' ambako mtoto anayefanyiwa ukatili, kamusi inaitafsiri kuwa :"Ni mtu au kikundi cha watu wanaokaa pamoja kama baba, mama na watoto" na kwa ujumla katika jamii za Kiafrika, inagusa mustakabali mpana; babu, bibi na wengineo.



Watoto wakiwa sehemu muhimu ya jamii inayopaswa kulindwa na umma, wakiwa katika moja ya tukio la Siku ya Mtoto wa Afrika. **PICHA: MTANDAO**

### MALEZI YAKOJE?

Sheria ya mtoto nchini inawapa wanafamilia jukumu la kwanza la ulinzi, matunzo, uzazi na malezi ya mtoto, huku ikitoa tafsiri pana ya jukumu ya kuwaweka watoto mbali na unayanyasaji inayopata tafsiri kutoka Sura ya Tatu ya Sheria ya Mtoto, 2009:

"Unyanyasaji mtoto maana yake ni ukiukwaji wa haki ya mtoto ambao unasababisha madhara ya kimwili, kimaadili, au kifikra ikijumuisha kupigwa, kutukanwa, kubaguliwa, kutelekezwa, kunyanyaswa kijinsia..."

Sheria hiyo inamtetea mtoto dhidi ya madhara kimwili, kimaadili, au kifikra na kuipatia ufafanuzi kwamba ni katika malezi na ulinzi wa mtoto dhidi ya mazingira yanayomhatarisha kimaadili na kimwili.

Tafsiri ya kisheria inamtaja 'mzazi' kuwa: "Baba au mama mzazi, aliyeasili na mtu mwingine yeyote mwenye jukumu la kumlea mtoto."

Pia, 'mlezi' anatajwa kuwa yeyote mwenye mamlaka au uwezo kwa mtoto au aliyeteuliwa kwa kiapo, wosia au amri ya mahakama. Wakati mtoto huyo anapatiwa ulinzi na malezi, sheria tajwa inatamka wasimamizi hao watawajibika kuwakinga na kuwahudumia watoto kiafya, kuwapa haki ya kuishi, pia usalama wao kimwili na kiakili.

"Mtu hatomsababishia mtoto mateso au aina nyingine ya ukatili, kumpa adhabu zisizo za kibinadamu au kumdhalilisha mtoto, ikijumuisha mila na desturi zozote zenye madhara kwake," inafafanua sheria hiyo.

### UHALISIA ULIVYO

NI aina ya matukio yanayoendelea kushika kasi kwa miaka kadhaa, tafakari ikienea katika maeneo kadhaa ikiwamo mitazamo ya kishirikina; kudhulumiana pesa na mali, wivu wa mapenzi, mila, desturi na utamaduni.

Wiki moja iliyopita kumesikika mtikisiko wa jinai, moja mkoani Rukwa mama na watoto wake waliuawa na wasiojulikana, huku kukiwapo kisa kinachofanana nacho wilayani Bahi, mkoani Dodoma, vyote hadi sasa vikiwa ndani ya uchunguzi wa polisi.

Mtazamo wa wanafalsafa na saikolojia, wengi wanaosimama wana mtazamo kuwa, mbali na hatua za kiserikali, pia kunahitajika hatua za kiimani kuchukuliwa kupunguza misuguano hiyo.

'Muhimu ni kubeba jukumu la kuongea na waumini kuwaasa njia sahihi ya kufanya, wanapohisi kutofautiana na wenzao ndani na nje ya familia.

Mkasa mojawapo wa kurejewa ni mfululizo wa mauaji ya watoto 10 yaliyotokea wilaya na mkoa wa Njombe, kuanzia mwishoni mwa mwaka 2018 hadi mwanzoni mwa 2019.

Ni taarifa zilizoripotiwa zikidaiwa watoto walitekwa, kuuawa

INAENDELEA UK.14

MAZINGIRA

# Maji ya bahari kuvamia ufukweni kunavyoua mashamba mboga Z'bar

**Na Jenifer Gilla**

Ni ngumu kusimulia, lakini ndivyo yalivyo madhila yaliyomkuta mwaka jana. Hidaya Kombo mkazi wa Kiungwe Kidogo iliyoko Bumbwini Unguja, akilalama maji ya bahari yalivamia shamba lake na kuharibu matango yake na kumsababishia hasara .

"Msimu wa kwanza wa kilimo mwaka jana wakati matango yana mwezi na nusu, bahari ikafurika chumvi ikafika mpaka kwenye mazao yangu, nikapata hasara ya shilingi milioni moja. Sitosahau, maana lilikuwa ni pigo kubwa kwangu,"anasimulia Hidaya, alivyofikia hatua kukata tamaa kulima mwaka mzima, kabla hajathubutu tena.

"Nimeamua kujaribu tena maana fedha za kilimo zinanisaidia kulisha familia, kwenye ekari moja ya matango sikosi shilingi milioni moja hadi shilingi milioni moja na nusu, ambayo inanisaidia kulisha familia yangu," anasema.

Kwa miaka takribani 15 sasa kilimo cha mboga katika bonde la Kilimani kimezorota kutokana na kuvamiwa na maji ya bahari yenye chumvi, hata kuyafanya yanyauke na kufa.

Hidaya anasema asilimia 30 ya wanawake wanaendelea na kilimo katika Bonde la Kilimani linalolimwa mboga na mpunga, kukiwapo vijiji vinne; Donge, Mchangani, Kiungwe Kidogo, Bumbwini na Makoba, vyenye jumla ya wakulima 2000 .



Sehemu ya mashamba yaliyoko Unguja, yaliyoathirika na mabadikiko ya tabianchi. **PICHA: JERNIFER GILLA**

### WAKIMBIA SHAMBA

Sheha wa Kijiji cha Kiungwe Kidogo, Amir Mbarak Juma, anasema mpaka sasa wanawake wanaoendelea na kilimo katika bonde hilo ni takribani 300 kati ya 1000 walioandikishwa, wengi wakikatishwa tamaa na maji ya chumvi.

Kauli inayoungwa mkono na Dorka Heri mkazi wa kijiji hicho, anayesema amelazimika kuacha kulima baada ya kupata hasara katika nusu ekari ya shamba lake la mihogo, alikolima mwaka jana

Naye anasimulia:"Mwaka jana niliamua kukodi shamba na kulima mihogo baada ya shamba langu nililokuwa nalima mpunga kuingiwa na chumvi nyingi, kutokana na kuvamiwa na maji ya bahari."

"Kwenye mihogo napo nimepata mazao kidogo kutokana na tatizo hilo hilo, sasa nimeona bora nikae pembeni kwenye kilimo mpaka hapo hali itakapokuwa sawa," analalamika mama huyo mwenye watoto saba, sasa akiendesha maisha kupitia biashara ndogo ya kuuza 'mishelisheli'.

> **Kwenye mihogo napo nimepata mazao kidogo kutokana na tatizo hilo hilo, sasa nimeona bora nikae pembeni kwenye kilimo mpaka hapo hali itakapokuwa sawa.**

Baadhi ya wakulima wa bonde hilo wanalalamikia kukosa kabisa mashamba ya kulima, baada ya kufunikwa na maji ya bahari kama anavyosimulia mkulima, Khadija Amri: "Kina kikiongezeka tu shamba langu linakuwa la kwanza kuingia chumvi na sina uwezo wa kukodi shamba kama wenzangu. "

Anakumbuka awali kiilmo kilimpatia kipato cha wastani wa Sh milioni 1.50 kutoka kwenye ekari ya mpunga, alikosaidiana na mumewe, analalamika sasa jukumu hilo la matunzo limemuangukia mumewe pekee, maana shamba halipo.

Ripoti ya Athari za Mabadiliko ya Tabianchi iliyotolewa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - 2019, Zanzibar imeathirika kwa kiwango cha juu na mabadiliko hayo, kukitajwa mmomonyoko mkubwa unaoathiri vijiji vya pwani na kusababisha hasara za kiuchumi, ikiwamo kilimo, biashara na makazi.

Kutokana na uhaba wa maji ya umwagiliaji , wakulima hao wanalazimika kuchimba visima vidogo vya kuhifadhi maji ya mvua inaponyesha, teknolojia inayotajwa kuwa duni.

"Mvua zinaponyesha tunachimba visima vidogo kwa ajili ya kuhifadhi maji na hayo ndio tunatumia kwenye kumwagilia mashambani, hapo sasa inategemea na wingi wa maji, kama mashamba ni makubwa unaishia njiani, mazao mengine yananyauka, hasara kubwa,"anasema Lailatu Abdi (50).

Anasema ni hali iliyomsababishia hasara ya Sh. 400,000 ya kutelekeza nusu ekari yake ya matango, yakiwa na mwezi mmoja baada ya maji aliyovuna kuishia njiani.

"Hali hii ilinikuta mwaka juzi, mvua hazikunyesha za kutosha kwa hivyo kisima hiki hakikuingia maji ya kutosha, nililima heka moja, mazao yalipofika katikati nikaona kabisa maji hayatoweza kutosha ikanibidi nigawe nimwagilie nusu tu," anasimulia kwa uchungu.

### MIKAKATI ILIYOPO

Mkurugenzi wa Mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar, Farhat Mbarouk, anasema Zanzibar imepokea fedha kiasi cha Dola za Marekani milioni moja kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCC) kusaidia kuzuia majanga yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi (Adaptation Fund), uliozinduliwa tarehe 13 mwezi huu.

"Ni wa miaka mitatu na moja ya maeneo yatakayofikiwa na pesa hizo kwa ajili ya kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi ni Bimbwili na utekelezaji wa eneo hilo utafanywa na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji na Mifugo, Zanzibar," anasema.

Injinia wa Umwagiliaji kutoka Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji na Mifugo Zanzibar, Mohamed Mohammed anadai mradi huo ndio mkombozi wa kilimo katika maeneo yaliyoteuliwa Zanzibar, kwa kuwa fedha hizo zitasaidia kufanya maboresho katika eneo husika.

"Tutajenga tuta la mita 500 eneo la Kiongwe kidogo na Mafufuni tutajenga la mita 400, kuzuia maji ya chumvi yasiingie kwenye mashamba ambao utaghalimu dola 152,900 .

"Pia, kutajengwa mfumo wa umwagiliaji utakaogharimu Dola 46,000, pamoja na greenhouse Dola 29,000, Tangi la kuhifadhia maji la lita 1,800,000 kwa ajili ya umwagiliaji litagharimu Dola 75,000," anafafanua. Huku fedha Dola za Marekani 6200, zitatumika kutoa elimu na kuongeza ujuzi.

Ofisa Mazingira Mwandamizi wa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), ambaye ni Mratibu Kitaifa wa Mfuko wa Adaptation Fund, Fredrik Mulinda, anasema: " Kwa kuwa tumeshazindua mradi huo.

"Sasa utekelezaji unakwenda kuanza mara moja na sisi kazi yetu ni kufuatilia kwa karibu maendeleo ya utekelezaji huo, lengo ni kuona shughuli za kiuchumi zilizokwamishwa na mabadiliko ya tabianchi zinarudi katika mstari."

### CHANGAMOTO JE?

Kina mama wakulima wa Tovuni na Wingwi wanataja kutokuwa na elimu ya kilimo cha kisasa nayo ni kikwazo kwao, huku mkazi Haji Juma, analalamikia kukosekana miundombinu ya umwagiliaji inawarudisha nyuma katika kilimo hicho.

"Kilimo cha mboga kinahitaji maji ya kutosha, sasa hapa hatuna vifaa vya umwagiliaji vya kutosha, tunategemea vichache vya kukodi na kama mwenye mali naye amelima msimu huo inabidi umsubiri amalize kumwagilia ndio akukodishe, wakati huo shughuli zako nyingine zinasimama," analalamika

Ripoti ya Shirika la Chakula Duniani (FAO) inaonyesha wanawake wanajumuisha zaidi ya asilimia 40 ya nguvu kazi ya kilimo duniani na nusu ya nguvu kazi ya kilimo Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Huku shirika la Umoja wa Taifa linalotetea Haki za Wanawake linasema wasichana ni waathirika wakubwa wa mabadiliko ya hali ya hewa na mazingira.

AFYA

# Asasi ya kijamii yajitosa kampeni ya chanjo Uviko 'nyumba hadi nyumba'

• Wadau bodabodada wapewa jukumu, vijiwe navyo vimo

Na Sabato Kasika



Waendesha bodaboda wakiwa kijiweni. Kampeni mpya yatajwa inahamasisha chanjo maeneo ya kazi zao. **PICHA: MAKTABA**

KATIKA juhudi kuhakikisha Watanzania wanaepuka ugonjwa wa UVIKO-19, Shirika lisilo la kiserikali la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI) nalo limejitosa kwa kuanzisha kampeni za kuelimisha jamii umuhimu wa chanjo.

Shirika hilo lenye maskani yake Mwananyamala, Dar es Salaam, limeipatia alama kupitia tamko "Chanjo ya Corona ni Salama, Jikinge Wewe na Uwapendao"

Mkurugenzi wa shirika hilo, Janeth Mawinza, anabainisha kwamba WAJIKI imekuwa na kampeni ya 'Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana' katika wilaya tatu za Kinondoni, Ilala na Temeke kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania Trust (WFT) na kwamba, wameongeza kampeni ya chanjo inayofanyika katika wilaya hizo.

"Tunafanya kampeni hiyo kila baada ya miezi mitatu, katika mikutano ya serikali za mitaa, kata na kila tunapoendesha semina na mijadala kwenye jamii, pia matangazo mitaani ya mlango kwa mlango au nyumba kwa nyumba," anasema.

Anafafanua kwamba kuna waelimishaji rika wa shirika hilo ambao katika kampeni za kuhamasisha chanjo ya corona hutumia magari ya matangazo yanayozunguka mitaani na wakati mwingine wanaingia nyumba kwa nyumba.

### MDAU MHAMASISHAJI

Mkurugenzi huyo anasema, kila eneo lina kiongozi mdau. Charles Mbina, anayeratibu upande wa Kinondoni, anasema wanahamasisha jamii kwa kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa huo, pia anawataka watu wajitokeze kwa wingi kuchanja.

"Kwa mujibu wa maelekezo ya serikali, chanjo ni hiari, lakini vilevile kuna haja ya kila mtu kujiongeza kwa kuchukua hatua za kujikinga na ugonjwa huo ikiwamo kuchanjwa ili kuwa salama zaidi," anasema Mbina.

Anafafanua kuwa wanapoingia nyumba moja hadi nyingine, huwa wanazungumza na kujibu maswali ya watu mbalimbali wanaohoji kuhusu uwepo wa ugonjwa huo na undani wake, pia wanawaelekeza umuhimu wa chanjo.

"Kufanya matangazo tu hakutoshi, kwani watu huonyesha hamu ya kutaka kujua zaidi kuhusu corona, hivyo wanahitaji kujibiwa, ndiyo maana tunapoingia nyumba kwa nyumba huwa tunajibu maswali yao," anasema.

> **Wapo watu ambao huwa wanatushangaa, wengine wanadai tunapoteza muda, lakini ukweli ni kwamba, kuzingatia maelekezo yote ya kujikinga na corona ni muhimu, tutaendelea kutoa elimu.**

### KAMPENI VIJIWENI

Mmoja wa madereva wa bodaboda wa Mabibo, Jijini Dar es Salaam, Godvoice Kayombo, anasema pamoja na kuwapo kampeni za kupinga ukatili, huwa wanahamasisha chanjo ya Uviko -19 mara moja kwa wiki katika vijiwe vyao.

"Sisi ni mabalozi wa WAJIKI. Mbali na kampeni ya kupinga ukatili wa ngono, tumeelekezwa kuhamasisha chanjo ya corona, na tumejiwekea siku moja kwa wiki kuhamasisha chanjo katika vijiwe vyetu," anasema Kayombo.

Mwendesha pikipiki huyo anasema, hawawezi kujiweka pembeni na mapambano ya ugonjwa huo na kwamba, wamepokea maelekezo ya shirika hilo kama mabalozi wake na kuyafanyia kazi.

"Wapo watu ambao huwa wanatushangaa, wengine wanadai tunapoteza muda, lakini ukweli ni kwamba, kuzingatia maelekezo yote ya kujikinga na corona ni muhimu, tutaendelea kutoa elimu,"anasema Kayombo.

Pia, anaiambia Nipashe kwamba wataendelea kutoa elimu hiyo, kwa sababu baadhi ya madereva wa bodaboda na abiria wao hawachukui tahadhari ya kutosha, ikiwamo ya kuvaa barakoa na pia kutobeba abiria zaidi ya mmoja.

### SERIKALI INAVYOTAKA

Serikali kupitia wizara yenye dhamana ya afya za Watanzania, imeshatoa mwongozo unaoelekeza kutopuuza ugonjwa huo, ili kusaidia jamii kuwa salama dhidi ya ugonjwa huo, kwa kuchukua tahadhari zote zinazotakiwa.

Mwongozo huo unataka maeneo yenye mikusanyiko kama vile stendi ya mabasi ya abiria na sokoni, kuwe na maji tiririka na vitakasa mikono, kama njia mojawapo ya kukabiliana na kuenea kwa ugonjwa huo.



Janeth Mawinza, Mkurugenzi wa Asasi ya Wajiki, ambayo imejitosa kwenye kuhamasisha chanjo nyumba hadi nyumba, pia vijiwe vya bodaboda. **PICHA: SABATO KASIKA**

Pia, viongozi wa mtaa au maeneo husika wanaelekezwa kuhakikisha kuna vyombo vya kuhifadhi maji na sabuni za kutosha katika kila kituo, soko au stendi, huku uongozi wa maeneo husika ukitakiwa kusimamia uwapo wa vifaa hivyo na mahitaji yake yote muhimu ikiwemo vifaa vya kunawia kwa majitiririka na kuhakikisha abiria wote wananawa.

Katika vyombo vya usafiri, wakala wao wanatakiwa kuhakikisha wanatambua nafasi ya vitakasa mikono katika vyombo hivyo, ili kila msafiri anayeingia katika vyombo hivyo vya umma awe amepata huduma hiyo muhimu.

Maelekezo ni kwamba, abiria wote wanatakiwa kuendelea kuelimishwa kuhusu umuhimu wa kutosongamana ndani ya vituo vya mabasi kupitia walinzi getini, wahudumu wa mabasi na askari wa usalama barabarani.

Kwa upande wa madereva wa bodaboda, wanaelekezwa kubeba idadi sahihi ya abiria na siyo 'mshikaki' wavae barakoa, huku katika stendi zikitakiwa kuhakikisha zinatoa ujumbe wa kuelimisha jamii ya wasafiri mara kwa mara.

Ujumbe wa kuelimisha jamii kuhusu kuzingatia mwongozo, ni ule wa kupitia vipaza sauti, pia wawapo safarini, madereva na wahudumu wa vyombo hivyo wanatakiwa kuhakikisha elimu hiyo, inatolewa kila mara.

Mwongozo huo unavielekeza vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha magari ya usafiri wa umma yanabeba abiria kulingana na idadi ya viti, pasipo kuruhusu abiria kusimama, ili kuepusha msongomano ndani ya magari hayo.

Ni jana tu serikali ilipokea shehena nyingine ya chanjo 800,000 kutoka China huku ikitamka tangu chanjo ianze kitaifa jumla ya Watanzania milioni 1.9 wameshachanja sawa na asilimia 3.3 ya wananchi wote.

Pia, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema kuanzia sasa wanatakiwa kutoa taarifa za jumla ya watu waliougua na waliokwishakufa huku sehemu kubwa kitaifa ikiwa ni wasiochanja, akilalamika kwamba mwamko bado ni mdogo kwani lengo ni kuchanja asilimia 60 ya Watanzania wote.

AFYA

JIJI TANGA BINGWA USAFI KITAIFA...

# Meya: Ni mwanzo, tumepania kushika rekodi kwa miaka 10

**Na Boniface Gideon,** TANGA

MNAMO Desemba 17 ya mwaka jana ilikuwa ya kihistoria kwa wakazi wa jijini Tanga, pale ilipotangazwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (sasa Wizara ya Afya) kushika 'namba moja' kwa usafi na utunzaji mazingira kitaifa.

Ni orodha inayoangazia zaidi majiji sita nchini, ambayo ni Tanga yenyewe, Dodoma, Mwanza, Mbeya, Arusha na Dar es Salaam. Katika vinara watatu kileleni, wa pili ni Arusha, kisha Mwanza ni ya tatu.

Hiyo ni mara ya kwanza kwa jiji hilo lenye mpangilio mzuri wa ujenzi kuanzia barabara ya kwanza hadi 21 kutwaa tuzo hiyo, ikienda sambamba na zawadi ya motisha ya shilingi milioni 20 kutoka Wizara ya Afya.

Lengo ndani ya tuzo hiyo inatajwa ni kuendeleza mikakati zaidi ya kulifanya jiji la Tanga kubaki safi zaidi nchini na hata kuingia kwenye orodha za kimataifa. Kimsingi, kuna mengi yanayoendelea na mikakati inayowezesha kutwaa tuzo hiyo ya heshima kitaifa.

**MIKAKATI YA JIJI**

Meya wa Jiji la Tanga, Abdurhaman Shiloo, anamwagia sifa wakazi wa jiji hilo kujitolea kutunza mazingira mpaka kufikia viwango vya juu kabisa na kuwa jiji kinara wa usafi,

Meya Shiloo huku akijigamba kwa kauli 'usafi ndio asili yetu' anawataka wananchi kuendelea kudumisha utamaduni huo, akiwa na maelezo: "Niwaombe kila mmoja kwa nafasi yake atunze mazingira ili yamtunze.



Dampo la taka lililoko Majani Mapana, jijini Tanga, awali liliongoza kwa kuzidiwa na uchafu uliotapakaa hadi kwenye makazi ya watu. Kwa sasa lina hali nzuri zaidi. **PICHA BONIFACE GIDEON**

> **"Halmashauri ya Jiji la Tanga, imejitahidi kuboresha maeneo yake yote, ambayo yalikuwa katika hali sugu ikiwamo kujenga dampo la kisasa.**

Anataja baadhi ya mikakati ijayo ya jiji hilo, ni kuweka kundi la vijana 50 watakaofanya kazi ya ukachero kuwakamata wanaotupa taka ovyo na atakayekamatwa atalipa faini ya Sh.50,000 ambapo kuna asilimia itawaendea makachero hao walinda mazingira.

Pia, anataja mkakati mwingine ni kuendelea kuwahimiza wananchi kwa kila kaya kulipia fedha Sh.2000 kukabiliana na uchafu, pamoja na kufanya usafi kwenye maeneo yote muhimu.

Shiloo anataja kuwapo maeneo mengine kama bustani za mapumziko maarufu Forodhani, na kwamba wamefanikiwa kuwapata wafadhili wa kuboresha miundombinu yake.

"Pia maeneo mengine yote halmashauri imejipanga kuboresha miundombinu na bajeti ipo. Lengo ni tuzo hii kubakia Tanga Mjini kwa miaka hata kumi mbeleni" anajigamba.

**WAKAZI WAFUNGUKA**

Kwa wakazi wa jijini Tanga wamekuwa na maoni tofauti kuhusu mabadiliko makubwa katika mwonekano wake pamoja na kutwaa tuzo hiyo kubwa nchini.

Abdallah Said, mkazi wa Majani Mapana Tanga anakiri hakuwahi kuamini itakuwapo siku makazi yao yatakuwa na hadhi hiyo iliyoitwaa katika 'Tuzo ya Jiji Bora kwa Usafi Nchini.'

"Ila cha msingi hapa ni kuendelea kuweka mikakati zaidi ili jiji liwe safi zaidi muda wote na tuitetee nafasi yetu tuliyokuwa nayo hivi sasa. Pia, niupongeze uongozi wa halmashauri yetu kwa hatua kubwa kama hii," anasema Said.

Rhoda Joseph, anayeishi Chumbageni anasema Halmashauri ya Jiji la Tanga, imejitahidi kuboresha maeneo yake yote, ambayo yalikuwa katika hali sugu ikiwamo kujenga dampo la kisasa.

"Jiji letu sasa hivi linapendeza sana muda wote. Cha msingi hapa tujiwekee mikakati ni namna gani kila mwananchi atakuwa mlinzi kwa mwenzake, kama ilivyo kwa wenzetu wa Moshi Mjini (washindi wa tuzo mara nyingi). Naamini tutakuwa bora zaidi ya hapa " anafafanua Rhoda.

Zubeda Hassan, mkazi wa Mwang'ombe 'B' ana maoni:"Jiji letu ndani ya miaka mitatu limebadilika sana limekuwa safi na nadhifu muda wote."

"Halmashauri yetu imeleta magari ya kisasa ya kukusanyia taka yanapita mitaani, japo tunalipia huduma ya taka kwa gharama kubwa ya shilingi 2000 kwa mwezi, lakini mimi nadhani hii imetusaidia sana," anasisitiza.

Zubeda anaeleza kwamba elimu imewafikia wananchi wa jiji hilo na kwa sasa imefika hatua kuna mwamko wa wakazi, hata kati yao wanadhibitiana pale mmoja anapoonekana kuharibu mazingira.

"Kwa sasa ukionekana unatupa taka sehemu ambayo haistahili, utakuta mwananchi mwenzio anakufokea. Tumeona kwenye madampo kumewekwa makontena maalumu pamoja na vijana wanaosimamia muda wote ili kuhakikisha uchafu haujai hadi dampo lizidiwe uchafu.

"Pia, ujenzi wa dampo la kisasa umeleta mapinduzi makubwa, niwaombee viongozi wetu waendelee kusimamia hivi hivi," anafafanua Zubeda

## Mtihani mauaji jamii yanavyorindima kifamilia, mikasa mipya kwa watoto

**INATOKA UK.11**

na kisha wakanyofolewa baadhi ya viungo vya tumbo, macho, pua, vidole na sehemu za siri.

Wakati serikali iliyalaani, huku polisi nayo ikawasaka, kuwakamata na kuwafikisha katika mikono ya sheria watuhumiwa wake.

Tukio lingine linahusu tuhuma za mwanaume mkazi wa wilayani Mvomero, kuua wanawe watatu kwa sumu kutokana na ugomvi unaodaiwa wa kimapenzi, yeye pekee akipona.

Pia, lingine lililoripiriwa mkoani Manyara, mama kuua watoto wake watatu kwa matunda yaliyotiwa sumu ya panya, chanzo ni ugomvi wa wanandoa au wapenzi.

Inaelezwa kwa ujumla, Polisi imejitahidi kubaini wahusika wa jinai hizo na kutoa ulinzi kwa watoto hasa wanapokuwa nje ya nyumba, wakiamini mtoto anakuwa salama kwa mzazi wake.

Ni mustakabali unaotoa somo na mafundisho ya ndoa, kuwaandaa wahusika wa pande zote mbili, kujua kuwapo wakati wa raha na tabu, kutofautiana na kuelewana ndicho cha msingi kinachopaswa kifanyike ili amani iendelee kutamalaki ndani ya nyumba yao.

Kukaa kimya kwa jamii kunalezwa ndiko kunakochagiza visa vya namna hiyo kujitokeza kwenye jamii, ni wakati wa familia, ndugu, jamaa na jamii wakiwamo viongozi wa dini na serikali kuingilia kati madhila hayo mapya na ya zamani, wataalamu wa saikolojia na jamii wana mchango muhimu, kuungana na serikali.

**JICHO LA WADAU**

Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) kinasema, kadri siku zinavyoendelea mauaji ya wanawake na watoto yanayotokana na sababu mbalimbali yameripotiwa zaidi, hasa katika sehemu kama Njombe, Rombo, Mto wa Mbu na Simiyu, pia Arusha.

Mkurugenzi wa TAMWA, Rose Reuben anadadisi katika taarifa yake kwamba:"Tumeona na tunapongeza juhudi kubwa zilizofanywa na vyombo vya usalama nchini lakini pamoja na juhudi hizo cha kujiuliza ni kuwa kwanini bado matukio haya ya mauaji yameendelea kuripotiwa siku baada ya siku?"

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), nacho katika ripoti yake ya mwaka 2020, kinalalamikia haki ya kuishi inayoendelea kuathiriwa na matukio ya vifo, anaeleza.

Kimsingi hata Siku ya Mtoto wa Afrika, inatokana na kumbukumbu ya kuomboleza mauaji ya watoto jijini Soweto, Afrika Kusini, Juni 16 mwaka 1976, katika zama za utawala wa kibaguzi.

**Makala hii ni tathmini ya mwandishi kuhusu jinai inavyoshamiri katika umma.**

TANGAZO

# Letshego Bank LETSHEGO BANK (T) LIMITED

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka/ Mwaka wa sasa 31-Des-21 | Robo Mwaka iliyopita 30-Sep-21 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 845 | 837 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 1,146 | 1,316 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 4,806 | 1,131 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 3 | 2 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa Kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 20,791 | 23,541 |
| | (Baada ya tengo la mikopo) | - | - |
| 12 | Mali Nyingine | 2,007 | 1,494 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za Udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,369 | 1,526 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **30,968** | **29,845** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 2,437 | 2,125 |
| 18 | Amana za Wateja | 7,674 | 7,025 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa fedha Tslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limibikizo za Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 299 | 401 |
| 24 | Dhima la Tozo Kwaajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Meneja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | (87) | (87) |
| 28 | Madeni | 5,200 | 5,200 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **15,524** | **14,664** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 KUTOA 20)** | **15,444** | **15,182** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | - | - |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 47,831 | 45,877 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | - | - |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (28,202) | (28,202) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | (4,185) | (2,493) |
| 36 | Stahiki ya wenye Hisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **15,444** | **15,182** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 39 | Mikopo chechefu (Zaidi ya Siku 90) | - | - |
| 40 | Mikopo chechefu (Zaidi ya Siku 30) | 6,686 | 5,825 |
| 41 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 5,339 | 4,221 |
| 42 | Mali nyingine chechefu | - | - |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 0% | 0% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi (Zaidi ya Siku 90) | 50% | 51% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi (Zaidi ya Siku 30) | 25.6% | 20.7% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 258% | 247% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 86% | 86% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 81% | 81% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 11% | -18% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 4% | -8% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.12.2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka Sasa 31-Des-21 | Robo Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-21 | Limbikizo la Mwaka wa Sasa 31-Des-21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Des-20 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 1,092 | 1,335 | 5,175 | 6,576 |
| 2 | Gharama za Riba | (401) | (302) | (1,546) | (1,724) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **691** | **1,033** | **3,629** | **4,852** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 47 | (462) | (551) | (1,213) |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la Tengo katika Mikopo | (727) | (11) | (510) | 1,029 |
| **6** | **Mapato yasiyo na Riba** | **81** | **168** | **747** | **1,072** |
| | 6.1 Faida/(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | (3) | (2) | (7) | (11) |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 65 | 112 | 560 | 832 |
| | 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 19 | 57 | 194 | 252 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba** | **(1,785)** | **(1,762)** | **(7,465)** | **(7,985)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (968) | (968) | (4,029) | (4,548) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gawio | (817) | (794) | (3,436) | (3,437) |
| **8** | **Faida / (Hasara) ya Uendeshaji** | **(1,692)** | **(1,035)** | **(4,150)** | **(2,245)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 0 | (14) | (41) | (46) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Hasili Baada ya Kodi ya Mapato** | **(1,692)** | **(1,048)** | **(4,191)** | **(2,291)** |
| 11 | Idadi ya Waajiriwa | 83 | 83 | 83 | 135 |
| 12 | Mapato kwa Hisa | (0) | (0) | (0) | (0) |
| 13 | Mapato ya Hisa zilizochujwa | (0) | (0) | (0) | (0) |
| 14 | Idadi ya Matawi | 5 | 5 | 5 | 5 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -6% | -3% | -6% | 0% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa fedha za wanahisa | -11% | -6% | -11% | -1% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 152% | 117% | 152% | 126% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazo Zalisha | 2% | 3% | 2% | 2% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.12.2021
(Kiasi cha shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa Sasa** | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | **36,487** | **8,520** | **-** | **-** | **(28,202)** | **16,805** |
| 1 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 1,955 | - | - | - | - | 1,955 |
| 2 Mapato Mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | | - | - |
| 3 Miamala na wanahisa | - | - | - | | - | - |
| 4 Gawio lililolipwa | - | - | - | | - | - |
| 5 Ziada ya Kisheria | - | - | - | | - | - |
| 6 Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | | (4,185) | (4,185) |
| 7 Mengineyo | - | - | - | | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **38,442** | **8,520** | **-** | **-** | **(32,387)** | **14,575** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | **29,937** | **8,520** | **-** | **-** | **(25,579)** | **12,878** |
| 1 Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 6,550 | - | - | - | - | 6,550 |
| 2 Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - |
| 3 Miamala na Wanahisa | - | - | - | - | - | - |
| 4 Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - |
| 5 Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - |
| 6 Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | (2,623) | (2,623) |
| 7 Mengineyo | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **36,487** | **8,520** | **-** | **-** | **(28,202)** | **16,805** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31.12.2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya Sasa 31-Des-21 | Robo Mwaka Iliyopita 30-Sepr-21 | Limbikizo la Mwaka wa Sasa 31-Des-21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31-Des-20 |
|---|---|---|---|---|---|
| I. | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (1,692) | (1,035) | (4,191) | (2,247) |
| | **Marekebisho Kwa Ajili ya:** | - | - | - | - |
| | -Badiliko Halisi Katika Mikopo | 679 | 473 | 1,060 | 1,723 |
| | -Hasara Katika Mali za Kudumu | 112 | 189 | 312 | 444 |
| | -Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali za Kudumu | (7) | - | (7) | - |
| | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji kabla ya Mabadiliko ya Mtajikazi** | **(907)** | **(372)** | **(2,826)** | **(80)** |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mikopo | 2,070 | 2,497 | 6,570 | (4,412) |
| | -Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali nyingine | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana | 961 | (1,988) | (3,685) | 3,720 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana za muda mfupi | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana Inayohitajika Kisheria | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (200) | (560) | (1,702) | (727) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (513) | 21 | 134 | 271 |
| | -Kodi iliyolipwa | - | (14) | (41) | (31) |
| | -Mengineyo | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uendeshaji** | **1,412** | **(416)** | **(1,550)** | **(1,260)** |
| II. | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawiwo Lililopokelewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | 150 | 37 | (115) | (515) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **150** | **37** | **(115)** | **(515)** |
| III. | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | 2,606 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | (1,500) | (4,000) |
| | Madeni ya Muda Mrefu | 1,955 | 870 | 2,825 | 6,600 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawiwo Lililipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mengineyo | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **1,955** | **870** | **1,325** | **5,206** |
| IV. | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | | | | |
| | **Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **3,516** | **490** | **(340)** | **3,431** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo mwaka | 3,285 | 2,784 | 7,141 | 3,710 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka** | **6,801** | **3,285** | **6,801** | **7,141** |

### MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| SN | PRODUCT/SERVICE | | PRODUCT/SERVICE DESCRIPTION | (TZS | (USD) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | DEPOSIT PRODUCTS | | | | |
| 1.1 | CURRENT ACCOUNT (letsGo Account) | a | Opening amount (cash only) | | |
| | | | Companies, institutions, firms | 100,000 | 100.00 |
| | | | Solipropriator | 50,000 | 50.00 |
| | | | Group/Associations | 30,000 | 30.00 |
| | | | Individuals/personal | 20,000 | 20.00 |
| | | | Interest rate (VARIES) | Same interest rates | N/A |
| | | b | Maintance/ Monthly fee | | |
| | | | Companies, institutions, firms | 8,000 | 8.00 |
| | | | Solipropriator | 6,000 | 5.00 |
| | | | Groups/Associations | 6,000 | 2.00 |
| | | | Individuals/personal | 2,000 | 2.00 |
| | | c | Minimum operating balance | | |
| | | | Companies, institutions, firms | 100,000 | 100.00 |
| | | | Solipropriator | 50,000 | 50.00 |
| | | | Groups/Associations | 30,000 | 30.00 |
| | | | Individuals/personal | 10,000 | 10.00 |
| | | d | charges below minimum operating balance | | |
| | | | Companies, institutions, firms | N/A | N/A |
| | | | Solipropriator | N/A | N/A |
| | | | Groups/Association | N/A | N/A |
| | | | Individuals/personal | N/A | N/A |
| 1.2 | SAVING ACCOUNTS (LETSGO FLEX) | a | Opening amount (cash only) | | |
| | | | Companies, institutions, firms(call account) | 100,000 | 100.00 |
| | | | Solipropriator | 50,000 | 50.00 |
| | | | Groups | 30,000 | 30.00 |
| | | | Individuals/personal | 20,000 | 20.00 |
| | | | Kids | 10,000 | 10.00 |
| | | | Interest rate (VARIES) | Same interest rates | N/A |
| | | | minimum interest bearing balance | 50,000 | |
| | | b | Maintance/Monthly fee | | |
| | | | Companies, institutions, firms | 2,000 | free |
| | | | Groups/Associations | free | free |
| | | | Individuals/personal | 2,000 | free |
| | | | kids | free | free |
| | | c | Minimum interest bearing balance | | |
| | | | Companies, institutions, firms | 50,000 | 50.00 |
| | | | solipropriator | 50,000 | 50.00 |
| | | | Groups/Associations | 50,000 | 50.00 |
| | | | Individuals/personal | 50,000 | 50.00 |
| | | | kids | 50,000 | 50.00 |
| | | d | Charges below minimum operating balance | | |
| | | | Companies, institutions, firms | N/A | N/A |
| | | | Solipropriator/Groups/Association | N/A | N/A |
| | | | Individuals/personal | N/A | N/A |
| 2 | BANK STATEMENTS | | | | |
| | | | Monthly e-statements (Current month) | Free | Free |
| | | | one page | No charge | |
| | | | Additional pagies(Current Year Data) | one copy TZS.1000 ,max TZS.20,000 | equivalent to TZS |
| | | | Ad Hoc copies (Back Up Data)from 2018 back ward | one copy TZS.1000,max TZS.40,000 | equivalent to TZS |
| 3 | REPORTS(CERTICATES,CONFIRMATION,REPORTS&INTRODUCTION LETTER) | | | | |
| | | | Certificate of Balance | 20,000 | equivalent to TZS |
| | | | Confirmation to Auditors | 30,000 | equivalent to TZS |
| | | | status report/Introduction letter | | |
| | | | local Bank Request | 40,000 | equivalent to TZS |
| | | | international Bank Request | 60,000 | equivalent to TZS |
| | | | Search fees -Information of : | | |
| | | | Less than 1 yrs | 30,000 | |
| | | | Between 1-3 years | 70,000 | |
| | | | over 3 years | 100,000 | |
| | | | CCTV Photo searching charges | 40,000 | equivalent to TZS |

| SN | PRODUCT/SERVICE | | PRODUCT/SERVICE DESCRIPTION | (TZS | (USD) |
|---|---|---|---|---|---|
| 4 | CHEQUE TRANSACTIONS | | | | |
| | | | counter cheque leaf | | |
| | | | Cheque Deposit other banks | Free | |
| | | | Cheque paid to customers of other banks(inward cheque) | 1,000 | |
| | | | cheque withdraw over the counter | 5,000 | 5.00 |
| | | | Stop payment order/cheque | 30,000 | equivalent to TZS |
| | | | Dishonoured cheques for lack of funds | 1.45% min 50,000 max 100,000 | 0.02 |
| | | | Refer to Drawer of Effects not cleared | 1.45% min 50,000 max 100,000 | 10.00 |
| | | | Special clearance | 50,000 | 35.00 |
| | | | cheque book fee Per leaf | | |
| | | | Companies, institutions, firms | 400 | |
| | | | Solipropriator/Groups/Association | 400 | |
| 5 | DORMANT ACCOUNT & CLOSING ACCOUNT | | | | |
| | | | Dormant account on activation | free | |
| | | | Dormant charges(Monthly) | | |
| | | | Current Account | free | |
| | | | Saving Account | free | |
| | | | Closing account less than 1 year | | |
| | | | current | 10,000 | 5.00 |
| | | | savings | 5,000 | 2.50 |
| 6 | CASH WITHDRAW | | | | |
| | | a | Cash withdrawal over the counter | | 0.02 |
| | | | current account(LetsGo) | | |
| | | | companies | 0-500,000=TZS.3,000 | |
| | | | solipropriator | 500,001-1,000,000=TZS.5,000 | |
| | | | Groups/Associations | 1,000,001-5,000,000=TZS.10,000 | 0.02 |
| | | | individuals/Personal | 5000,0001-10,000,000=TZS.15,000 | |
| | | | | 10,000,001-30,000,001=TZS.20,000 | |
| | | | | 30,000,001 and above = 50,000/= | |
| | | | saving account(LetsGo Flexi) | 2,000 | |
| 7 | LOAN REGISTRATION FEES & EXPENSES | | | | |
| | LENDING FEES(old rates prevail with flexibility to negotiation) | | | | |
| | | | Comfort letters/Reference letters | 30,000.00 | |
| | LEGAL FEES | a | (in addition to registration fees and expenses) | | |
| | | | Debenture over company's assets for a limited liability company & partnerships | 250,000 | |
| | | | Debenture over assets of sole proprietor/individual | 250,000 | |
| 8 | GUARANTEES | | | | |
| | | a | Bid Bonds/Guarantees | 350,000 | |
| | | | unsecured maxmumum 500 Million | 350,000 | |
| | | | secured Above 500 Million | 350,000 | |
| | | b | Advance payment bonds | | |
| | | | Cash cover | 0.5% to 1% | |
| | | | legalmorgage | 1% to 2% | |
| | | c | Performance | | |
| | | | cash cover-Commission | 0.5_to 1% | |
| | | | legal mortgage-Commission | 1% to 2% | |
| 9 | Funds transfer charges - Local | | | | |
| | | a | Commission on outward TISS transfers | 12,800 | |
| | | c | All internal transfer same customer | free | |
| | | | All internal transfer different customer | 1,200 | |

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uendeshaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikuwa na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka sasa,

| Jina/ Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Omar S. Msangi **(Mkurugenzi Mtendaji)** | | 27/01/2022 |
| Lydia Machangu **Meneja wa Fedha na Utawala)** | | 27/01/2022 |
| **Rashid Sendoro (Mkaguzi wa ndani)** | | 27/01/2022 |

Sisi, tuliotajwa hapo juu chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benk na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006, nazinaonesha hali halisi.

| Jina/ Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Simon Jengo **(Mwenyekiti wa Bodi)** | | 27/01/2022 |
| Noel Sangiwa **(Mkurugenzi)** | | 27/01/2022 |




TANGAZO

NMB Karibu yako

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

## NMB BANK PLC

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DISEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Robo Mwaka ya sasa 31.12.2021 | Robo Mwaka iliyopita 30.09.2021 | Robo Mwaka ya sasa 31.12.2021 | Robo Mwaka iliyopita 30.09.2021 |
| **A.** | **MALI** | | | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 490,175 | 472,717 | 490,175 | 472,717 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 999,775 | 867,924 | 999,775 | 867,924 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 1,739,279 | 1,477,857 | 1,739,279 | 1,477,857 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 312,683 | 413,592 | 312,683 | 413,592 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 22,521 | 39,517 | 22,521 | 39,517 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 104 | 2,878 | 104 | 2,878 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 31,761 | 32,951 | 31,761 | 32,951 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 4,658,035 | 4,465,222 | 4,658,035 | 4,465,622 |
| 12 | Mali Nyingine | 242,398 | 216,396 | 313,275 | 291,601 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 2,920 | 2,920 | 2,920 | 2,920 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 192,888 | 193,610 | 161,036 | 160,934 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **8,692,539** | **8,185,584** | **8,731,564** | **8,228,513** |
| **B.** | **DHIMA** | | | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 46,836 | 43,138 | 46,836 | 43,138 |
| 18 | Amana za Wateja | 6,442,284 | 6,051,740 | 6,443,658 | 6,053,622 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 150,957 | 142,797 | 150,957 | 142,797 |
| 20 | Amana Maalumu | 6,900 | 37,157 | 6,900 | 37,157 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 2,178 | 2,180 | 2,178 | 2,180 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 83,226 | 75,521 | 82,064 | 75,168 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadaye | 42,642 | 40,571 | 42,642 | 40,571 |
| 27 | Dhima Nyingine | 80,115 | 69,215 | 123,302 | 114,787 |
| 28 | Madeni | 486,450 | 441,742 | 486,450 | 441,742 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **7,341,588** | **6,904,061** | **7,384,987** | **6,951,162** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **1,350,951** | **1,281,523** | **1,346,577** | **1,277,351** |

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Robo Mwaka ya sasa 31.12.2021 | Robo Mwaka iliyopita 30.09.2021 | Robo Mwaka ya sasa 31.12.2021 | Robo Mwaka iliyopita 30.09.2021 |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 1,037,941 | 1,037,941 | 1,040,642 | 1,040,642 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 288,632 | 210,965 | 285,469 | 208,004 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 466 | 8,705 | 466 | 8,705 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 3,912 | 3,912 | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **1,350,951** | **1,281,523** | **1,346,577** | **1,277,351** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 1,235,676 | 1,135,812 | 1,235,676 | 1,135,812 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 157,785 | 178,924 | 157,785 | 178,924 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 205,897 | 220,436 | 205,897 | 220,436 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 3,353 | 11,016 | 3,353 | 11,016 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 16% | 16% | 15% | 16% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 3.2% | 3.8% | 3.2% | 3.8% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 73% | 75% | 73% | 75% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 54% | 55% | 53% | 54% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 77% | 78% | 77% | 77% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 6% | 5% | 6% | 5% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 6% | 8% | 6% | 7% |

Trilioni **8.7** Jumla ya Mali +23% YoY

Trilioni **6.4** Amana za Wateja +25% YoY

Trilioni **4.7** Mikopo Halisi Iliyopo +13% YoY

**3.2%** Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DISEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | KUNDI | | BENKI | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Robo ya Mwaka sasa 31.12.21 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31.12.20 | Robo ya Mwaka sasa 31.12.21 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31.12.20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.12.21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31.12.20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.12.21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31.12.20 |
| 1 | Mapato ya Riba | 219,426 | 197,566 | 219,426 | 197,597 | 815,446 | 712,648 | 815,446 | 712,977 |
| 2 | Gharama za Riba | (35,169) | (36,743) | (35,169) | (42,582) | (133,331) | (141,483) | (133,331) | (147,322) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **184,257** | **160,823** | **184,257** | **155,015** | **682,115** | **571,165** | **682,115** | **565,655** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (26,022) | (38,313) | (26,022) | (38,313) | (109,095) | (119,312) | (109,095) | (119,312) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **83,814** | **81,301** | **83,844** | **81,301** | **306,460** | **271,279** | **306,490** | **271,279** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 11,058 | 11,848 | 11,088 | 11,848 | 33,553 | 30,484 | 33,583 | 30,484 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 65,082 | 64,009 | 65,082 | 64,009 | 250,005 | 226,400 | 250,005 | 226,400 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - | 63 | 17 | 63 | 17 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 7,674 | 5,444 | 7,674 | 5,444 | 22,839 | 14,378 | 22,839 | 14,378 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(124,043)** | **(113,946)** | **(125,011)** | **(110,169)** | **(459,612)** | **(421,852)** | **(463,541)** | **(421,879)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (65,646) | (41,547) | (65,646) | (41,547) | (243,680) | (195,515) | (243,680) | (195,515) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (718) | (3,591) | (718) | (3,591) | (11,516) | (10,603) | (11,516) | (10,603) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (57,679) | (68,807) | (58,647) | (65,031) | (204,416) | (215,734) | (208,345) | (215,761) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **118,006** | **74,241** | **117,068** | **74,241** | **419,868** | **301,280** | **415,969** | **295,743** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (35,690) | (28,084) | (35,393) | (27,045) | (131,236) | (90,980) | (130,500) | (89,941) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **82,316** | **46,157** | **81,675** | **47,196** | **288,632** | **210,300** | **285,469** | **205,802** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa Faida/(Hasara) uthamanishaji Dhamana za Kuuzwa | (8,239) | (124) | (8,239) | (124) | (326) | (257) | (326) | (257) |
| | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **74,077** | **46,033** | **73,436** | **47,072** | **288,306** | **210,043** | **285,143** | **205,545** |
| 12 | Idadi ya Waajiriwa | 3,482 | 3,474 | 3,482 | 3,474 | 3,482 | 3,474 | 3,482 | 3,474 |
| 13 | Mapato kwa Hisa | 165 | 124 | 163 | 122 | 577 | 420 | 571 | 412 |
| 14 | Idadi ya Matawi | 226 | 226 | 226 | 226 | 226 | 226 | 226 | 226 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Mali | 4% | 4% | 4% | 3% | 3% | 3% | 4% | 3% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 24% | 22% | 25% | 19% | 21% | 19% | 23% | 18% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 46% | 47% | 47% | 50% | 46% | 50% | 47% | 51% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 11% | 12% | 12% | 10% | 10% | 10% | 11% | 13% |

Bilioni **419.9** Faida kabla ya Kodi ya Mapato +41% YoY

Bilioni **288.6** Faida Baada ya Kodi ya Mapato +39% YoY

Uwiano wa Matumizi yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi **47%**

*YoY - Linganishi mwaka kwa mwaka





TANGAZO

NMB Karibu yako

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

## NMB BANK PLC

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA

### KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | KUNDI | | BENKI | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Robo Mwaka ya sasa 31.12.2021 | Robo Mwaka iliyopita 30.09.2021 | Robo Mwaka ya sasa 31.12.2021 | Robo Mwaka iliyopita 30.09.2021 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.12.2021 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.12.2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.12.2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31.12.2020 |
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 118,006 | 107,915 | 117,068 | 106,817 | 419,868 | 301,280 | 415,967 | 295,743 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | | | | | |
| | - Hasara Katika Mali | 5,615 | 13,610 | 5,158 | 13,118 | 39,132 | 68,308 | 37,198 | 68,550 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (191,623) | (221,225) | (191,223) | (221,225) | (581,007) | (518,783) | (580,536) | (513,572) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 372,145 | 281,500 | 371,637 | 281,238 | 1,190,303 | 506,677 | 1,191,672 | 500,955 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 20,674 | 19,923 | 17,480 | 19,449 | 9,269 | 42,333 | 10,328 | 49,370 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (3,035) | (33,502) | 1,293 | (31,176) | (44,686) | 20,168 | (42,119) | 17,886 |
| | - Kodi Iliyolipwa | (46,479) | (38,795) | (46,110) | (38,795) | (141,185) | (123,140) | (140,816) | (122,089) |
| | - Mengineyo (SMR) | 10,973 | (45,023) | 10,973 | (45,023) | (56,620) | 64,078 | (56,620) | 64,078 |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **286,276** | **84,403** | **286,276** | **84,403** | **835,074** | **360,921** | **835,074** | **360,921** |
| **II.** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (5,260) | (8,271) | (5,260) | (8,271) | (19,206) | (18,581) | (19,206) | (18,581) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Mengineyo (Uwekezaji katika Hisa na Amana) | (269,661) | (124,124) | (269,661) | (124,124) | (435,350) | (540,614) | (435,350) | (540,614) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(274,921)** | **(132,395)** | **(274,921)** | **(132,395)** | **(454,556)** | **(559,195)** | **(454,556)** | **(559,195)** |

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | KUNDI | | BENKI | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Robo Mwaka ya sasa 31.12.2021 | Robo Mwaka iliyopita 30.09.2021 | Robo Mwaka ya sasa 31.12.2021 | Robo Mwaka iliyopita 30.09.2021 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.12.2021 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.12.2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.12.2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31.12.2020 |
| **III:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - | (68,500) | (48,000) | (68,500) | (48,000) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 44,708 | 188,405 | 44,708 | 188,405 | 162,710 | (67,297) | 162,710 | (67,297) |
| | Mengineyo (Mabadiliko yatokanayo na bei za fedha za kigeni) | - | - | - | - | - | (11,944) | - | (11,944) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **44,708** | **188,405** | **44,708** | **188,405** | **94,210** | **(127,241)** | **94,210** | **(127,241)** |
| **IV:** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | | | | | |
| | Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 56,063 | 140,413 | 56,063 | 140,413 | 474,728 | (325,515) | 474,728 | (325,515) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 1,325,694 | 1,185,281 | 1,325,694 | 1,185,281 | 907,029 | 1,232,544 | 907,029 | 1,232,544 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **1,381,757** | **1,325,694** | **1,381,757** | **1,325,694** | **1,381,757** | **907,029** | **1,381,757** | **907,029** |

## TAARIFA YA KUNDI YA MABADILIKO YA MTAJI

### KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DISEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Uthamanishaji Amana za Kuuzwa) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2021** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | **-** | **1,106,441** | **-** | **-** | **4,704** | **1,131,145** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 288,632 | - | - | - | 288,632 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (326) | (326) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (68,500) | - | - | - | (68,500) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | **-** | **1,326,573** | **-** | **-** | **4,378** | **1,350,951** |
| **Mwaka Uliopita 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | **-** | **944,473** | **-** | **-** | **4,630** | **969,103** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 209,969 | - | - | 331 | 210,300 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (257) | (257) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (48,000) | - | - | - | (48,000) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | **-** | **1,106,442** | **-** | **-** | **4,704** | **1,131,146** |

## TAARIFA YA BENKI YA MABADILIKO YA MTAJI

### KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DISEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Uthamanishaji Amana za Kuuzwa) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2021** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | **-** | **1,109,142** | **-** | **-** | **792** | **1,129,934** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 285,469 | - | - | - | 285,469 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (326) | (326) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (68,500) | - | - | - | (68,500) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | **-** | **1,326,111** | **-** | **-** | **466** | **1,346,577** |
| **Mwaka Uliopita 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | **-** | **951,341** | **-** | **-** | **1,049** | **972,390** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 205,802 | - | - | - | 205,802 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (257) | (257) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (48,000) | - | - | - | (48,000) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | **-** | **1,109,143** | **-** | **-** | **792** | **1,129,935** |

## BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA DISEMBA 2021

**Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Ruth Zaipuna **Afisa Mtendaji Mkuu** | | Januari 25, 2022 |
| Juma Kimori **Afisa Mkuu wa Fedha** | | Januari 25, 2022 |
| Benedicto Baragomwa **Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | | Januari 25, 2022 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Dr. Edwin P. Mhede **Mwenyekiti wa Bodi** | | Januari 25, 2022 |
| Benson Mahenya **Mkurugenzi** | | Januari 25, 2022 |

BENKI BORA TANZANIA
TUZO 7 ZA KIMATAIFA
Asante kwa kuchagua Benki ya NMB!







# CRB yashukuru serikali kutoa kazi za ujenzi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BODI ya Usajili wa Makandarasi (CRB), imeishukuru serikali kwa kuanza kutoa kazi nyingi za ujenzi na kuwataka makandarasi wazalendo kuchangamkia fursa hiyo.

Hayo yalisemwa jana mkoani Dodoma na Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Injinia Consolata Ngimbwa, wakati akifungua mafunzo ya siku tatu kwa makandarasi wazalendo kuhusu wajibu wa makandarasi katika miradi ya ujenzi.

Alisema kuna kazi nyingi za ujenzi ambazo zimekuwa zikitangazwa kwa miradi hata ya ujenzi wa madarasa na barabara ambayo makandarasi wazalendo wanaweza kupata.

Alisema wanachotakiwa kufanya ni kujaza zabuni zao kwa umakini mkubwa na kuachana na kawaida ya kuwapa watu wengine wawajazie huku akiwataka kuitekeleza miradi hiyo kwa ufanisi.

"Kuna tabia ya kutumia watu wengine kuwajazia zabuni sasa unamwamini mtu anakujazia kumbe ndiye anayekuangusha, tumia muda mwingi kutulia ili ujaze kitu kinachoeleweka kwa sababu wakati mwingine unakosa kazi kwa uzembe wa uliyemwamini," alisisitiza.

Alisema makandarasi wazalendo wanapaswa kuanza kuungana kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi vinginevyo watabaki watazamaji.

Pia alisema kampuni kubwa za kigeni zinapata miradi mingi ya ujenzi kutokana na kuunganisha rasilimali walizonazo na ndizo zimekuwa zikifanikiwa kupata miradi mikubwa nya ujenzi inayogharimu fedha nyingi.

"Kufanya kazi kwa ubia sio utamaduni wa siku nyingi sana, lakini wenzetu wameanza zamani sana. Tuache ubinafsi tuingie ubia kwasababu hata ukipata changamoto ichukue kama changamoto tu ya kukufanya usonge mbele na kuwa muwazi kwa mtu unayetaka kuingia naye ubia," alisema.

Alisema baadhi ya makandarasi wazalendo wanakwama kuungana kutekeleza miradi mikubwa kutokana na ubinafsi wa baadhi yao ambao hawaweki uwazi na kusababisha migogoro baina yao wakati wa utekelezaji wa miradi.

Injinia Ngimbwa aliwataka pia wawe na chama kimoja chenye nguvu kubwa ambacho kitakuwa sauti yao wanapokuwa na changamoto mbalimbali badala ya kuwa na vyama vingi visivyo na tija.

Naye Naibu Msajili wa CRB, Injinia David Jere, alisema makandarasi wanapaswa kulipa ada ya mwaka kwa wakati kwasababu ni takwa la kisheria na kwamba wale ambao watakaidi watachukuliwa hatua kali.

Alisema CRB ilianzisha Mfuko wa Kusaidia Makandarasi (CAF) ambapo makandarasi wanaweza kukopa fedha kwa ajili ya kuanza kutekeleza miradi anayopata lakini wengi hawajajiunga ili kunufaika na fedha hizo.

Alisema makandarasi wanaopata mikopo hiyo wanapaswa kuirejesha kwa wakati ili kuwezesha wenzao kupata mikopo kama hiyo pindi wanapopata zabuni za ujenzi.

# Watoto 5,390 wanaofanya kazi mitaani watambuliwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kipindi cha mwaka 2020/2021, serikali na wadau wake imetekeleza mambo mbalimbali yanayohusu ustawi wa watoto ikiwamo kutambua watoto 5,390 wanaoishi na kufanya kazi mitaani.

Aidha, kati yao 135, waliunganishwa na familia zao, 821 walipatiwa vifaa vya shule na 75 familia zao ziliunganishwa na huduma za kuimarisha uchumi wa kaya.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alibainisha hayo jana jijini hapa katika ziara yake ya kutembelea na makao ya kulelea watoto na wazee ya Home of Love and Joy yaliyoko Kata ya Hombolo.

Alisema pia vituo vya kulelea watoto mchana na wachanga 303 vikiwa na idadi ya 6,772 vilisajiliwa na kufanya idadi ya vituo kufikia 2,068 vyenye jumla ya watoto 163,394 walioandikishwa nchi nzima.

"Nyumba salama sita zimesajiliwa za hifadhi ya muda kwa waathirika wa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

"Mafunzo kazini yametolewa kwa walezi 1,156 katika mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya na Pwani ili kuboresha utoaji wa huduma katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na watoto wachanga," alisema.

Vilevile, alisema huduma ya malezi ya kambo imetolewa kwa watoto 22 na huduma ya kuasiliwa kwa watoto 27 imetolewa. Kadhalika, alisema makao 24 ya kulelea watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi yenye watoto 707 yamesajiliwa na kufanya idadi ya 244 ya wote 24,254 nchini.

"Huduma kwa watoto 116 wanaokinzana na sheria imetolewa ambapo 58 wanahudumiwa katika mahabusu tano za watoto na 58 wanapatiwa huduma ya marekebisho ya tabia katika shule ya maadilisho Irambo-Mbeya," alisema.

Dk. Gwajima alisema jumla ya mashauri ya jinai 188 yamefanyiwa kazi yanayohusisha watoto 229 waliopatiwa msaada wa kisheria, marekebisho ya tabia, unasihi na msaada wa kisaikolojia na kijamii.

Alisema programu za kijamii za marekebisho ya tabia kwa watoto wanaokinzana na walio katika hatari ya kukinzana na sheria zimeanzishwa katika mikoa sita na halmashauri 10.

Alitaja mikoa hiyo na halmashauri kuwa ni Mbeya Jiji, Mji wa Kibondo na Njombe, halmashauri za Kasulu, Magu na Mbarali pamoja na Manispaa za Iringa, Temeke, na Kigamboni.

"Jumla ya watoto 78 wamechepushwa kutoka kwenye mfumo wa haki jinai kwenda kwenye mpango wa marekebisho ya tabia," alisema.

Aliongeza kuwa mpango wa wasaidizi wa watoto mahakamani (Guardian Ad Litem) umeanzishwa katika halmashauri tatu za Mbeya Jiji, Manispaa ya Temeke na wilaya ya Kisarawe ambapo wasaidizi 30 walisajiliwa na kujengewa uwezo wa kuwahudumia watoto wanaoshtakiwa kwa makosa mbalimbali.

"Tukumbuke kuwa watoto wanapokuwa wanaishi kwenye mazingira hatarishi pamoja na changamoto nyingi pia wanakutana na ukatili mkubwa.

"Aidha, ukatili wa majumbani ni sababu mojawapo inayowafanya watoto wakimbilie mitaani na matokeo yake wanakutana na aina zingine za ukatili na mazingira hatari zaidi," alisema.

Alibainisha kuwa takwimu zinaonyesha waathirika wakubwa wa vitendo vya ukatili kwa upande wa watoto asilimia 70 ni wa kike.

Hata hivyo, alisema serikali inaangalia suala la maendeleo ya watoto na imezindua programu mpya kubwa tatu kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa watoto.




Jaji Mkuu Tanzania, Prof. Ibrahim Juma (kulia), akiwa na Waziri wa Katiba na Sheria, George Simbachawene, wakifungua jiwe la msingi ujenzi wa makao makuu ya Mahakama ya Tanzania, jijini Dodoma jana. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# TRA yaomba viongozi wa dini kuhamasisha kudai risiti

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imetoa wito kwa viongozi wa dini nchini kutumia majukwaa ya ibada kuhamasisha wananchi kulipa kodi kwa hiari na kudai risiti wanaponunua bidhaa yoyote.

Wito huo ulitolewa jijini hapa na Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi TRA, Richard Kayombo, wakati akizungumza kwenye mkutano wa amani wa Jumuiya ya Maridhiano Tanzania uliokuwa na lengo la kuipongeza serikali ya awamu ya sita kwa kuongeza kasi ukusanyaji mapato.

Kayombo alisema serikali imeleta jambo zuri la wananchi kudai risiti kila wanapofanya ununuzi lakini kuna tatizo la wengi kutodai.

"Niwaombe viongozi wa dini kwa sauti zenu za upole, zinazoheshimika tutumie sauti hizo kuhamasisha Watanzania watekeleze wajibu wao wa kulipa kodi wakati wa mahubiri kwenye nyumba za ibada (misikiti, makanisa).

Asiyetoa risiti ana nia ya kijidhulumu yeye na serikali yake na wananchi wenzake na atatuchelewesha kwenye masuala ya upatikanaji wa dawa, barabara za lami, maji, umeme," alisema Kayombo.

Alieleza kuwa nchini kuna ukanda mrefu wa bahari, maziwa na kumepakana na nchi nane na kuna vichochoro vingi vya magendo ambavyo vinanufaisha baadhi ya watu na kusababisha ukusanyaji mapato kutoongezeka wakati lengo la kufikia zaidi ya Sh. trilioni tatu lipo.

Kayombo alifafanua kuwa suala hilo likiendelea kuna athari zinazoweza kujitokeza ikiwamo bidhaa zinazoingia kupita sehemu isiyo sahihi kwa kutofanyiwa ukaguzi na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), zinazoweza kuathiri afya za Watanzania.

"Kuna hatari nyingi kama silaha haramu, dawa za kulevya ndiyo maana sisi kama TRA kazi yetu si kukusanya tu bali kudhibiti bidhaa haramu zinazoweza kuingia nchini na kuvuruga amani," alisema.

Alisema wapo wafanyabiashara wanaojishughulisha na shughuli mbalimbali wasiosajiliwa licha ya kuwekwa utaratibu rahisi wa kujisajili kwa njia ya mtandao na kuwataka kufanya hivyo ili nchi izidi kupata maendeleo.



## Wataalamu afya watakiwa kutoa huduma vijijini

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WIZARA ya Afya imewataka wataalamu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya, kutoa huduma kwa njia ya mkoba (outreach) ili kuwajengea uwezo watoa huduma walioko hospitali ngazi ya mkoa na wilaya kuboresha huduma na kupunguza rufani.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Seif Shekilaghe, alisema hayo juzi alipotembelea hospitali hiyo kukagua maendeleo ya ujenzi wa jengo la wazazi katika Hospitali ya Rufani ya Meta.

Shekilaghe alisema ili kurahisisha shughuli za utoaji huduma za afya nchini wataalam wote katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya wanapaswa kujifunza namna ya kutoa huduma kwa njia ya mkoba ili kupungua mzigo wa rufani kwa wagonjwa.

Alisema njia hiyo pia itasaidia kupunguza mrundikano wa wagonjwa katika hospitali na kwamba zitasaidia pia kuondoa foleni pindi wanapopata huduma za matibabu.

Katika hatua nyingine, Dk. Shekilaghe alipongeza maendeleo ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto linalojengwa katika hospitali hiyo huku akimhimiza mkandarasi kumaliza ujenzi huo kabla ya Aprili 30, mwaka huu.

Alisema hadi sasa jengo hilo limekamilika kwa asilimia 92 na kwamba kukamilika kwake kutasaidia kuhudumia wajawazito wengi na kinamama wanaosumbuliwa na masuala ya uzazi kutoka maeneo mbalimbali ya Nyanda za Juu Kusini ikiwamo Katavi, Rukwa, Mbeya, Iringa, Ruvuma, Njombe na Songwe.

Serikali kupitia Wizara ya Afya itaendelea kushirikiana na vituo vya kutolea huduma za afya nchini ili kutatua vikwazo mbalimbali vilivyopo lengo ni kuboresha hali ya utoaji huduma za matibabu kwa wananchi na kuwasihi watumishi wa afya kudumisha ushirikiano, nidhamu na maadili ya taaluma zao kazini.

# Wajifungia kutafuta mwarobaini vikwazo vya kibiashara mipakani

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKUU wa mikoa minane na wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama, wamejifungia jijini Mbeya kujadili namna ya kuondoa vikwazo vya kibiashara baina ya Tanzania na mataifa jirani pamoja na ulinzi wa mipaka ya nchi.

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema hayo jana alipofungua kikao cha kujadili hali ya ulinzi na usalama pamoja na fursa za kibiashara katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema kikao hicho kitakuja na mwarobaini wa namna ya kuviondoa vikwazo vya kibiashara ili kusaidia wafanyabiashara kufanya shughuli zao kwa uhuru.

Kigahe alisema ushirikiano wa kibiashara katika mataifa mbalimbali si mzuri na kwamba kikao hicho ni muhimu kujadili mambo ya kufanya ili kufanya shughuli zao bila tatizo lolote kulinganisha na ilivyo sasa.

"Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizotia saini makubaliano ya kufanya biashara bila mipaka barani Afrika. Tangu kutiwa saini kwa mkataba huo, Watanzania wanaruhusiwa kufanya biashara zao ndani na nje ya mipaka ya nchi lakini bado kuna vikwazo mbalimbali katika kujitafutia riziki. Ni muhimu kujadili ili kuviondoa," alisema.

Kigahe aliwashauri viongozi hao kutengeneza mazingira mazuri ya uwekezaji kupitia fursa mbalimbali zilizoko katika mikoa hiyo kama vile bandari za Itungi, Kiwira, Kasanga na Kalema ambazo zinatumiwa na wafanyabiashara wa ndani na nje kusafirisha bidhaa zao.

Mwenyekiti wa Wakuu wa Mikoa Nyanda za Juu ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema kikao hicho kina tija katika kuleta maendeleo kwa wananchi.

Alisema kupitia fursa mbalimbali za kibiashara, kilimo na miundombinu mingine kutawezesha kuwakwamua wananchi na wimbi la umaskini na kunufaika na uwekezaji kupitia mipaka mbalimbali ya nchi.

Mikoa iliyoshiriki kikao hicho ni Mbeya ambao ndio mwenyeji, Songwe, Rukwa, Njombe, Iringa, Ruvuma, Katavi na Tabora ambao ni mgeni mwalikwa.



Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Exaud Kigahe (katikati), akizungumza na wakuu wa mikoa nane ya Nyanda za Juu Kusini na Tabora pamoja wa wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama kutoka mikoa hiyo, wakijadili mikakati ya kukuza biashara na kuimarisha mipaka jijini Mbeya jana. Kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera na Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joseph Mkirikiti. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Serikali yaombwa kuimarisha barabara hifadhini

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Hifadhi ya Taifa Kitulo iliyoko katika mikoa ya Mbeya na Njombe, Theodora Batiho, ameiomba serikali kuboresha miundombinu ya barabara ndani ya hifadhi hiyo.

Amesema hatua hiyo inawezesha hifadhi kuendelea kupokea watalii katika kipindi chote cha mwaka kuliko ilivyo sasa. Wakati wa mvua za masika, watalii hushindwa kutembelea hifadhi hiyo kutokana na uharibifu wa miundombinu.

Batiho alitoa ombi hilo jana alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu mikakati ya hifadhi hiyo katika kutangaza vivutio vya utalii. Alisema wamejitahidi kutangaza vivutio lakini kikwazo kikubwa ni ubovu wa miundombinu ya barabara kuingia na kuzunguka hifadhi hiyo.

"Tunashukuru Watanzania na wageni wanaoendelea kuvutiwa na uzuri wa hifadhi yetu kutokana na mandhari iliyopo yakiwamo maua ya kupendeza, wanyama, uoto wa asili, miinuko na maporomoko ya maji ambayo yanamvutia mtalii pamoja na mwekezaji," alisema Batiho.

Licha ya serikali kuweka mazingira mazuri ya kutangaza vivutio vya utalii ikiwamo kuwahamasisha wananchi kutembelea vivutio hivyo, alisema bado kuna tatizo katika miundombinu ya barabara ambayo ndiyo muhimu kutangaza hifadhi hiyo.

Pia alisema katika kutangaza vivutio vya utalii, Hifadhi ya Kitulo imeandaa program maalumu ambayo itawahusisha wanafunzi wa vyuo vikuu katika mkoa wa Mbeya na maeneo mengine kufanya tafrija ambayo itabeba ujumbe wa kutangaza uzuri wa hifadhi hiyo.

Alisema program hiyo itatoa fursa kwa hifadhi ya Kitulo kutangaza vivutio vya utalii kwa kutumia wanavyuo hao ambao kwa pamoja watakula na kunywa.

"Licha ya uhitaji wa barabara katika hifadhi yetu ya Kitulo, kipekee tunamshukuru Rais wetu Samia Suluhu Hassan kwa kuwa mstari wa mbele kutangaza vivutio mbalimbali vya utalii nchini. Uamuzi huo umeleta manufaa kwani umechochea kuongeza idadi ya watalii kutembelea hifadhi na kwamba wanaendelea na moyo huo," alisema Batiho.

Baadhi ya wananchi mkoani Mbeya, wamesema uwapo wa hifadhi ya Kitulo umefungua fursa kwa vijana kupata ajira ikiwamo kuwaongoza watalii.

Mmoja wa wananchi hao, Lameck Paschal, alisema hifadhi hiyo kila mara inazidi kupokea idadi kubwa ya watalii kutoka ndani na nje ya nchi lakini kikwazo kilichopo ni mwitiko mdogo wa wananchi kufanya uwekezaji ndani ya hifadhi hiyo.



## Mbunge amwaga misaada miaka 45 ya kuzaliwa CCM

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA kuadhimisha miaka 45 ya Chama cha Mapinduzi (CM), Mbunge wa viti maalumu Mkoa wa Kaskazini Unguja, Saada Mansour, amekabidhi vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni tisa kwa umoja wa wanawake wa CCM (UWT) ili kusaidia katika jamii.

Miongoni mwa vifaa hivyo alivyokabidhi ni vitanda, magodoro kwa ajili ya hospitali kwa wodi ya wanawake, taulo za kike,cherehani, mabati kwa ajili ya kiwanda cha nafaka, simu kwa ajili ya Tehama na gari kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalumu.

Akizungumza jana baada ya makabidhiano hayo, katika ofisi za CCM Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mbunge huyo alisema utoaji wa vifaa hivyo ni utekelezaji wa ilani ya chama hicho.

Alisema kuwa hospitali na vituo vya afya katika Mkoa huo zinakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo uhaba wa vitanda hasa katika wodi za wanawake, hivyo vitendea kazi alivyovitoa vitasaidia kupunguza changamoto hizo.

Alisema taulo za kike zitasadia kuwasitiri wanawake wanapoingia katika siku zao za hedhi ambao wapo katika ofisi za chama.

Alieleza kuwa atahakikisha anasaidia jamii katika kupata huduma mbalimbali muhimu kama ilani cha CCM inayoelekeza.

Naye Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mariam Muharam Shomari, alisema kuwa vifaa hivyo vitatumiwa kwa malengo yaliyokusudiwa ikiwemo vitanda kwa ajili ya kusaidia wodi za kinamama.

Alimpongeza mbunge huyo kwa juhudi zake katika kuwasaidia wanawake wa Mkoa huo kwa kutatua changamooto mbalimbali za wanawake bila ya kujali itikadi za vyama.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kaskazini Unguja, Iddi Ali Ame, alimpongeza Mbunge huyo wa viti maalumu kwa kutekeleza ahadi alizoziahidi wakati akiomba kura ya kuchaguliwa nafasi hiyo na kuwataka wana CCM kushiriki kikamilifu katika sherehe za miaka 45 ya kuzaliwa kwa CCM.

# Makandarasi wapewa wiki 2 kuanza miradi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amewaagiza makandarasi wanaosimamia miradi ya maendeleo amabao hawajaanza kazi kuhakikisha wanaanza ndani ya wiki mbili.

Hemed alieleza hayo katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo katika mikoa ya Kaskazini na Kusini Unguja.

Katika ziara hiyo Hemed alieleza kufurahishwa kuona makandarasi wameanza kazi katika maeneo yao, ambapo amezitaka wizara na taasisi husika kuhakikisha wanasimamia vyema ili kuleta tija.

Hemed alisema hakuridhishwa na mradi wa tangi la maji Bumbwini, ambapo alimwagiza waziri wa maji, nishati na madini kuhakikisha makandarasi wanapatikana na kuanza kazi mara moja ili kuondoa kero ya maji kwa wananchi wa eneo hilo na maeneo jirani.

Hemed alisema serikali imeshatenga fedha kwa ajili ya miradi hiyo ambapo kila mkandarasi atakabidhiwa fedha kwa mujibu wa taratibu na makubaliano ya mikataba waliofunga na wizara husika.

Kuhusu miradi ya hospitali za wilaya na majengo ya shule, Makamu wa Pili alieleza kufurahishwa na kazi inayofanywa na makandarasi waliokabidhiwa kazi hizo, na kuwataka kuendelea na miradi hiyo, kwa ushirikiano na ofisi za wakuu wa wilaya na wakuu wa mikoa ambapo miradi hiyo inatekelezwa kwa wakati na viwango kwa mujibu wa makubaliano.

Katika hatua nyingine, Hemed alielekeza Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) kuhakikisha wanasimamia majengo hayo kuwa ya viwango bora na yenye kudumu kwa muda mrefu, ili kunakisi fedha iliyotolewa na serikali kwa ajili ya kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

Kuhusu shule zinazofanyiwa matengenezo, alisema serikali imeamua kuzifanyia matengenezo ili wanafunzi wasome katika mazingira mazuri na kuutaka uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha ukarabati huo unasimamiwa ipasavyo.

Kuhusu umeme katika ujenzi wa Hospitali ya Kusini na Wilaya ya Kati, Hemed aliagiza uongozi wa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto kukaa pamoja na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kuhakikisha umeme unafika katika maeneo hayo ili kurahisisha ujenzi wa miradi hiyo.

Wakuu wa Mikoa ya Kaskazini Unguja na Kusini Unguja walimhakikishia Makamu wa Pili wa Rais kuwa watatoa ushirikiano kwa makandarasi hao na kuhakikisha wanatatua changamoto zote zitakazowakabili ili kufanikisha ujenzi wa miradi hiyo kama ilivyokusudiwa.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Khamis Juma, alimhakikishia kuwa fedha zimeshaingizwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa madarasa ya shule, na kwamba utaanza haraka iwezekanavyo.



Mbunge wa Viti Maalum, Saada Mansour (kushoto), akikabidhi kiti mwendo kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa CCM, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mariam Shomari, kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum ikiwa ni sehemu ya vifaa mbalimbali vyenye thamani ya shilingi milioni tisa ikiwa ni utekelezaji wa ilani ya CCM, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kampuni tatu kuingiza vileo Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Vileo Zanzibar (ZLB) imesema imepitisha kampuni tatu kati ya tisa zilizoomba zabuni ya uingizaji wa vileo kwa mujibu wa Sheria Namba 9 ya Mwaka 2020 katika Mwaka wa Fedha 2022.

Akizungumza na waandishi wa habari Mjini Zanzibar, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Khamis Haji, alisema kampuni hizo zimechaguliwa baada ya kufikia sifa za vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa kifungu 33(1) cha Sheria ya Vileo Namba 9 ya Mwaka 2020 kuhusu uingizaji wa vileo Zanzibar.

"Kwa mujibu wa sheria kifungu cha 33(1) kibali cha uingizaji kitatolewa kwa waingizaji wasiozidi watu awe na sifa za mlipakodi, awe na ghala la kuhifadhia, awe Mzanzibari na awe na gari ya kusambazia vinywaji.

Haji alisema kwa mujibu wa kifungu cha 33(2), mtu yeyote ambaye atabainika kuingiza vileo bila ya kuwa na kibali atakuwa ametenda kosa la jinai na adhabu yake ni kifungo cha miaka miwili au kulipa faini ya kiwango cha milioni tatu na vileo vilivyokamatwa kutaifishwa. Kampuni zilizopewa vibali ni ZMMI (Zanzibar Maritime and Mercanle International CLD), Scoch Store Limited na One Stop Campany baada ya kukidhi sifa na masharti ikiwamo kulipia kibali Sh. milioni 30 na gharama za ukaguzi Sh. milioni tano.

Alieleza kwamba vibali hivyo vimetolewa baada ya kufanyika ukaguzi kwa kampuni zote zilizojitokeza katika zabuni kasoro kampuni moja ambayo ukaguzi haukufanyika kutokana na mmiliki wake kuwa nje ya nchi.

Alisema kwa mujibu wa sheria, kampuni ambazo hazijapata vibali zitaendelea kutoa huduma kwa kununua vileo kutoka kwa kampuni ambazo zimetuliwa kuingiza vileo Zanzibar mwaka huu.

"Kuweka kampuni tatu kuingiza vileo Zanzibar kutasaidia kudhibiti mapato ya serikali na kulinda mila na utamaduni wa Zanzibar baada ya kuwapo uingizaji holela wa vileo na kusababisha serikali kupoteza mapato.

Alivitaka vyombo vya ulinzi na usalama kusimamia sheria hasa katika maeneo ya bandari, viwanja vya ndege ili kudhibiti uingizaji wa vileo kinyume cha sheria ili malengo ya kutungwa sheria mpya ya vileo kufikiwa.

"Kampuni zote zilizojitokeza waliofanikiwa kupata na waliokosa wote tumeshawataarifu kwa kuwaandikia barua tangu Januari 19, mwaka huu, baada ya bodi ya vileo kukamilisha zoezi la kuchagua kampuni za uingizaji wa vileo kwa mujibu wa sheria," alisema.

# TANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA: KWA AJILI YA UPATIKANAJI WA VIFAA VYA KITAALAM VYA UTAMBUZI WA VITU SUMAKU CHINI YA ARDHI KATIKA MRADI WA BOMBA LA MAFULA LA AFRIKA MASHARIKI
## KUMBUKUMBU NA. 0010007415

Kampuni ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V. ya nchini Tanzania, inakaribisha mashirika yenye uzoefu na yenye sifa kuonesha nia yao ya utoaji wa huduma ya upatikanaji wa vifaa vya kitaalam vya utambuzi wa vitu sumaku chini ya ardhi katika Mradi wa Bomba la Mafuta la la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

- Usambazaji wa chapa ya Schonstedt, modeli ya GA-72Cd, vitambuzi vya sumaku chini ya ardhi nchini Tanzania.
- Usambazaji wa chapa ya EBINGER, modeli ya UPEX® 740 M, kitambua sumaku kikubwa cha kitanzi cha chuma.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni/Mashirika yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na kuambatanisha nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa Usajili pamoja na Leseni ya Biashara.
- Uthibitisho wa uwakala /muuzaji aliyeidhinishwa na upatikanaji wa huduma za ukarabati zilizoidhinishwa nchini.
- Rejea za usambazaji wa vifaa vinavyofanana na hivi.
- Uthibitisho wa uwezo wa kampuni kimtaji.
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na Cheti cha Kulipa kodi ya mapato kwa (TRA) cha mwaka wa hivi karibuni.
- Wakati wa kuwasilisha majibu kuonesha nia inasisitizwa sana kuambatisha maombi ya kujisajili kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma wa Ndani.
- Kukidhi vigezo na Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya Ndani.

Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Maombi yote ya kuonesha nia ni lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza

**Muhimu:** Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali zakutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia yao kwa kutuma pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya tarehe **9 Februari 2022** saa **09 :00** za Afrika Mashariki (EAT), Baruapepe inapaswa kuwa **0010007415.**

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA: KWA AJILI YA UTOAJI WA HUDUMA ZA KISHERIA KWA WAGUSWA WA UTWAAJI WA ARDHI YA MKUZA WA BOMBA LA MAFUTA KATIKA MRADI WA EACOP.
## KUMBUKUMBU NA.0010007423

Kampuni ya Mafuta na Gesi ya Total Energies East Africa Midstream B.V. ya nchini Tanzania, inakaribisha watoa huduma wenye uzoefu na sifa kuonesha nia yao kwa ajili ya utoaji wa huduma za kisheria kwa waguswa wa utwaaji wa Ardhi ya Mkuza wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

Mradi wa EACOP unatafuta kampuni ya uwakili iliyo na uwezo wa kutoa ushauri na usaidizi kwa Watu Walioguswa na Mradi (PAPs) wakati wa mchakato wa utwaaji wa ardhi kwa ajili ya Mkuza wa Bomba la mafuta. Ushauri na usaidizi unaohitajika utalenga taarifa za stahiki, mchakato wa mkataba wa fidia (EBCA) kwa muda wa miezi 3 baada ya malipo ya fidia kufanyika. MZABUNI ataanzisha madawati ya muda ya msaada katika vijiji vilivyoguswa na utwaaji wa ardhi kwa ajili ya mkuza wa bomba la mafuta na kuwapatia washauri wenye sifa na waliosajiliwa. Washauri hawa watakuwa na ufahamu katika sheria ya Tanzania ya utwaaji ardhi na taratibu zinazohusiana. Huduma hizo za ushauri zitatolewa bure kwa PAPs.

**VIGEZO MUHIMU:**

Kampuni za uwakili zinazoonyesha nia zinaalikwa kutuma maombi yao huku zikiambatanisha:

- Uthibitisho wa usajili ikiwa ni pamoja na leseni ya sasa ya biashara.
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na Cheti cha mlipa kodi ya mapato (TRA) cha mwaka wa hivi karibuni.
- Wakati wa kuwasilisha majibu kuonesha nia unasisitizwa sana kuambatisha maombi ya kujisajili kwenye kazi data ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma wa Ndani.
- Kukidhi vigezo na Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa Vyeti vya kutoa huduma na shughuli za kisheria vya sasa.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia yao kwa kutuma pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya tarehe **9 Februari 2022** saa **11 jioni** saa za Afrika Mashariki (EAT), Barua pepe inapaswa kuwa **0010007423.**

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Maombi yote ya kuoesha nia ni lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza.

EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

**MAOMBI YA KUONESHA NIA: KWA AJILI YA USAMBAZAJI WA VIFAA VYA KAMBI YA MUDA KATIKA MRADI WA EACOP KUMBUKUMBU NA. 0010007422**

Kampuni ya Mafuta na Gesi ya Total Energies East Africa Midstream B.V. ya nchini Tanzania, inakaribisha mashirika yenye uzoefu na yenye sifa kuonesha nia yao kuwezesha uanzishwaji na usimamizi wa vifaa vya kambi ya muda katika mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpakaChongoleani, MkoawaTanga nchini Tanzania. Urefuwa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
Mradi wa EACOP unamtafuta Mzabuni mwenye uzoefu wakutosha ili kuanzisha na kusimamia kambi za muda kandokando mwa Ukanda wa Mkuza wa Bomba la mafuta ili kusaidia mchakato wa utwaaji wa ardhi. Uanzishaji na usimamizi wa Kambi za muda zinazohamishika utajumuisha kwa kiwango cha kawaida:

- Upatikanaji wa maeneo yanayofaa na yanayofikika ili kuanzisha kambi za muda.
- Utoaji wa mahema kwa ajili ya mahali pa kuishi kwa watu katiya 30 hadi 50.
- Utoaji wa huduma za usafi wa mazingira (kama vile kusafisha, ufuaji, maji taka, kuoga, vyoo n.k) kwa watu kati ya 30 hadi 50, na kuhakikisha kuna mgawanyo mzuri wa vifaa vya wanaume/wanawake.
- Utoaji wa huduma ya chakula angalau milo mitatu kwa siku, huku milo ya mchana ikitolewa kwa ajili ya kula palepale au kuondoka na chakula. Maandalizi yote ya chakula yatafuata viwango vya juu na kuzingatia mahitaji ya kitamaduni.
- Utoaji wa huduma za afya, usalama na ulinzi ikijumuisha ulinzi wa vitu, kinga na udhibiti na usimamizi wa moto, na vifaa vya matibabu/uimarishaji katika maeneo ya Mradi.
- Mfumo wa usimamizi ili kuruhusu utunzaji/uhifadhi wa malazi katika kambi za muda kwa ajili ya timu za EACOP.
- Usimamizi wa aina zote za taka zinazozalishwa kupitia shughuli za kambi za muda.

**VIGEZO MUHIMU:**
Makampuni yanayoonyesha nia yanakaribishwa kuandika maombi yao kwa kuambatanisha:
- Uthibitisho wa Usajili pamoja na Leseni ya Biashara ya sasa.
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na Cheti cha mlipa kodi ya mapato (TRA) cha mwaka
  wa hivi karibuni.
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Mamlaka ya Usalama na Afya Kazini – OSHA
- Wakati wa kuwasilisha majibu kuonesha nia inasisitizwa sana kuambatisha maombi ya kujisajili kwenye kazidata ya EWURA (LSSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani.
- Kukidhi vigezo na Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa uzoefu katika uanzishaji na usimamizi wa kambi za muda kwa ajili ya shughuli za viwanda nchini Tanzania.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonesha nia yao kwa kutuma pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya tarehe **09 Februari 2022** saa **11 jioni** saa za Afrika Mashariki (EAT), Baruapepe inapaswa kuwa **0010007422.**

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Maombi yote ya kuoesha nia ni lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza.

166680

# Nyanda za Juu wauza korosho tani 26.2

**Na Stevie Chindiye, TUNDURU**

TANI 26,267,488 za korosho zilizozalishwa na wakulima wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini katika mikoa ya Mbeya, Njombe na Ruvuma, zimeuzwa katika kipindi cha msimu wa mwaka 2021/2022.

Ofisa Ushirika wa Wilaya ya Tunduru, mkoani Ruvuma, George Bisani, alisema hayo wakati akiongea na wakulima wa Kijiji cha Kitanda, katika mnada wa 13 na wa mwisho katika msimu huo.

Alisema kutokana na mauzo hayo, Sh. 41,152,007,000 ziliingizwa kwenye mzunguko wa pato la fedha katika maeneo hayo ambayo kinara ni wakulima wa Wilaya ya Tunduru.

Meneja wa Bodi ya Korosho Tanzania, tawi la Tunduru, Shauri Mokiwa, pamoja na mambo mengine aliwapongeza wakulima wa maeneo hayo kwa kujitahidi kusimamia ubora na kuifanya wilaya hiyo na viunga vyake kuuza korosho zote kwa ubora wa daraja la kwanza.

Wakiongea kwa nyakati tofauti, baadhi ya wakulima walidai kutoridhishwa na bei zilizotolewa na wanunuzi katika msimu huo walizodai kuwa sio za kuridhisha hali iliyosababisha wakulima wengi kupata hasara.

Akizungumzia utekelezaji wa mauzo ya zao hilo, Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Wilaya ya Tunduru (TAMCU), Mussa Manjaule, alisema miongoni mwa vikwazo vilivyojitokeza ni pamoja na mzabuni wa kusambaza magunia kuwakimbia kabla ya kusambaza mzigo huo.

Alisema kutokana na hali hiyo, uuzaji wa korosho ulidhorota kwa kupungua kasi ya wakulima kupeleka korosho zao magulioni hali iliyosababisha malalamiko ya kucheleshewa malipo kwa baadhi ya wakulima ambao walipeleka mapema.

Manjaule alifafanua kuwa taarifa hiyo tayari TAMCU imekwishafanya marekebisho ya vikwazo na kwamba watahakikisha katika msimu ujao hayajitokezi.

# TIC, washirika kutembelea miradi iliyosajiliwa

**Na Mwandishi Wetu**

Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na taasisi 12 zinazoshirikiana na kituo hicho jana zimeazimia kutembelea miradi ambayo imepitishwa na TIC ili kujiridhisha juu ya namna miradi hiyo inavyoibua ajira na kuchangia katika ukuaji wa pato la taifa.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumaliza kikao cha TIC na taasisi hizo 12 katika Ofisi ya Waziri Mkuu , Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Dk. Maduhu Kazi, amesema kikao hicho ni sehemu ya mwendelezo wa vikao vyenye lengo la kujadili changamoto na kuibua mapendekezo yatakayosaidia kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini.

"Tumeazimia kuanza kutembelea miradi mbalimbali ambayo imepitishwa na TIC ambayo sote tulishirikiana kuipitisha kwa kutumia chemba yetu ya huduma ya mahala pamoja (one stop facilitation centre) ili kujionea maendeleo ya miradi hiyo na namna inavyochangia katika kuzalisha ajira na kukuza pato la taifa," alisema Dk. Kazi.

**"Tumeazimia kuanza kutembelea miradi mbalimbali ambayo imepitishwa na TIC ambayo sote tulishirikiana kuipitisha kwa kutumia chemba yetu ya huduma ya mahala pamoja (one stop facilitation centre) ili kujionea maendeleo ya miradi hiyo na namna inavyochangia katika kuzalisha ajira na kukuza pato la taifa," alisema Dk. Kazi.**

Alisema moja ya miradi itakayotembelewa ni kiwanda cha kutengeneza mbolea ya asili (organic fertiliser) cha Intracom Limited ambacho pia kilitembelewa jana.

"Kiwanda hicho kinajengwa Nala jijini hapa na ambacho kimepewa cheti cha uwekezaji namba 20214355 kupitia chemba ya huduma mahala pamoja." alisema

"Wakuu wa taasisi watakitembelea kiwanda hiki na kujionea maendeleo ya mradi huo ambao unatarajiwa kutekelezwa kwa muda wa miaka mitatu hadi 2024 ambapo kwa sasa mradi huu umefikia asilimia 52 ya utekelezaji wake," alisema.

Alisema kwa kampuni hiyo imewekeza zaidi ya dola za Marekani milioni 180 na kwamba inatarajiwa zaidi ya ajira za moja kwa moja 3000 zitaibuliwa na zisizokuwa za moja kwa moja ni 1500. Zaidi ya tani laki 600,000 zitazalishwa kila mwaka.

"Mradi huu utalifanya eneo la viwanda la Nala kuchangamka kimaendeleo na kupelekea kuzalishwa kwa fursa mbalimbali za ujasiriamali jambo litakalopelekea wananchi wengi kujiajiri na wengine kuajiriwa," alifafanua Dk.Kazi.

Ameeleza kuwa kukamilika kwa kiwanda hicho kutatoa fursa kwa Watanzania kuuza malighafi mbalimbali katika kiwanda hicho ili kuzalisha mbolea ambayo inahitajika kuendeleza kilimo nchini.

Naye mjumbe wa kamati hiyo ambaye pia ni Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), Dk. Godwill Wanga, alisema jambo muhimu ni kuhakikisha mfumo wa pamoja wa kuwahudumia wawekezaji unajengwa ili kutoa fursa kwa wawekezaji kupata huduma kwa haraka, wawekeze na kuiletea nchi faida.

"Tunapokuwa kwenye mfumo mmoja kama taasisi za kuhudumia wawekezaji na wafanyabiashara ufanisi katika usajili miradi utaongezeka pamoja na kuwafanya wawekezaji zaidi kuja kuwekeza hapa nchini," alisema Dk.Wanga

HABARI KITAIFA

## Mkurugenzi awafunda wanufaika wa TASAF

**Na Elizabeth Zaya, HANDENI**

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Mji wa Handeni, Maryam Ukwaju, amewataka wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini (PSSN II), unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), kutumia vizuri pesa wanayopewa na mfuko huo na siyo kuimalizia kwenye starehe ikiwamo shughuli za kijadi maarufu kama vigodoro.

Alitoa kauli hiyo alipotembelewa na maofisa wa TASAF kutoka makao makuu.

Alisema TASAF imekuwa mkombozi katika halmashauri hiyo kwa kusaidia kuhuishwa na kuboresha maisha ya wananchi wa hali duni ikiwamo kuchagiza watoto wa familia hizo kuwainua kielimu, kiafya na malazi hivyo ni vema kuhakikisha wanaendelea kuitumia vizuri na kufikia malengo yaliyokusudiwa ili wanufaike zaidi na mpango huo.

"Katika eneo letu hili ni ukweli usiofichika, TASAF imesaidia kwa kiwango kikubwa kukomboa maisha ya wananchi wetu waliokuwa wakiishi katika hali duni, kaya nyingi kwa sasa ambazo zilikuwa na hali duni zina uhakika wa kupata milo mitatu kwa siku, watoto wana uhakika wa kupata sare za shule na kuhudhuria masomo kama wenzao, wanahudumiwa kiafya," alisema Ukwaju.

"Na ndio maana tunawaambia kwamba hizi fedha wanazopatiwa wasizitumie vibaya wakazipeleka kwenye shughuli za vigodoro badala ya kutumia kwenye malengo yaliyokusudiwa."

Kwa upande wake Mratibu wa TASAF Handeni Mji, Frank Anania, alisema mpango huo wa kunusuru kaya maskini awamu ya kwanza ulinufaisha walengwa hao kutoka katika mitaa 40, lakini kwa awamu ya pili umenufaisha walengwa kutoka mitaa 60.

Alisema katika awamu hiyo ya pili ya mpango, imechukua walengwa wote tofauti na awamu ya kwanza ambayo ilichukua asilimia 70 ya walengwa.

Pia Anania alisema awamu hiyo imesaidia kuondoa malalamiko yaliyokuwa awali wakati wa kuchukua idadi ndogo ya walengwa.

"Wakati mpango unachukua walengwa kwa asilimia 70, kulikuwa na malalamiko kidogo, wananchi wenye hali duni walikuwa wanalalamika kwamba wanaachwa, si hao tu hata viongozi kutoka kwenye mitaa na kata mbalimbali nao walikuwa wanalalamika kwa nini baadhi ya wananchi wao wanaachwa wakati wana hali ngumu, lakini kwa sasa yote hayo yamekwisha," alisema Anania.

# Mil. 100/- zaanza kuwapanga machinga masoko Jiji la Ilala

**Na Salome Mwasamale**

HALMASHAURI ya Jiji la Ilala imetenga shilingi milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa shedi katika soko la Zingiziwa ili kuondoa baadhi ya changamoto zinazosababisha wafanyabiashara washindwe kufanya biashara.

Akizungumza na Nipashe, mkuu wa masoko wa Jiji la Ilala, Victor Rugemalira, alisema ujenzi huo utaanza mapema mwezi ujao baada ya mchumi wa halmashauri kuingiza fedha hizo kwenye akaunti ya kata zilizokusudiwa.

Alisema ziko tayari kinachosubiriwa ni mchakato wa matumizi ya fedha hizo kwenda kwenye kata ili viongozi wazielekeze kwenye masoko husika.

Aidha, alisema soko la Zingiziwa linauhitaji wa shedi nne, lakini kwa kuanza wataanza na moja kulingana na upatikanaji wa fedha na katika bajeti ya fedha ijayo wataidhinisha fedha nyingine mpaka pale litakapokamilika.

Aliongoza kuwa mkakati wa halmashauri ni kuboresha masoko yote yaliyoko Ilala ili kuhakikisha wafanyabiashara wanakosa visingizio vya kukaa barabarani.

"Kisingizio kikubwa cha wafanyabiashara kukimbia kwenye masoko ni miundombinu mibovu na kweli inaweza kuwa sababu ambayo tumeamua kukabiliana nayo ili kuondoka kero ya wafanyabiashara barabarani," alisema.

Aliongoza kuwa ujenzi wa shedi hizo utasaidia kuondoka changamoto nyingi zinazosababisha zoezi la kuondoka wafanyabiashara barabarani ikiwamo ile ya msuguano wa watendaji wa serikali na wa kisiasa.

Masoko yaliyoingia katika awamu hiyo ya kwanza ya mradi wa ujenzi wa shedi ni Zingiziwa Kigogo Freshi, Pugu Kajiungeni na Tabata Muslim.

Shedi moja yenye thamani ya shilingi milioni mia moja ina uwezo wa kubeba wafanyabiashara 200 hadi 250.

Hassan Namkwacha, makamu mwenyekiti soko la Zingiziwa alipongeza serikali kwa maamuzi yake mazuri ya uboreshaji wa masoko na kuanza na shedi.

Namkwacha alisema shedi inatoa mpangilio mzuri wa vizimba na kuwafanya wafanyabiashara wafanye biashara zao bila kero kwa kuwa hawabughudhiwi na mvua wala jua.

Alisema soko lake linauhitaji wa shedi nne na waliahidiwa kupewa shedi tatu, lakini wanashukuru hata kwa hiyo moja.



Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa Kampuni ya ALAF, Hawa Bayumi (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu hafla ya kuwatangaza washindi wa Tuzo ya Kiswahili ya Mabati-Cornell ya Fasihi, itakayofanyika kesho katika Ukumbi wa Mlimani City jijini humo. Kushoto ni Ofisa Masoko wa kampuni hiyo, Theresia Mmasy. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mabalozi wa kodi watoa somo kwa wananchi biashara magendo

**Na Mwandishi Wetu, TANGA**

MABALOZI wa kodi wamewataka wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla kuacha biashara za magendo kwa kuwa vitendo hivyo vinaikosesha serikali mapato yake stahiki kutokana na wahusika kukwepa kulipa kodi.

Wito huo ulitolewa jana na mabalozi wa kodi ambao ni: Zulfa Omar, Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Kusini Pemba, Subira Mgalu, Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Pwani na Edo Kumwembe ambaye ni mwandishi wa habari wakati wa ziara yao ya kikazi katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga iliyolenga kuhamasisha wafanyabiashara kulipa kodi kwa hiari.

"Katika ziara yetu tumepita katika mipaka mingi na kila mipaka tuliyopita tumekuta kuna changamoto ya magendo, wananchi wanapitisha bidhaa kwenye njia zisizo rasmi na ukiwahoji, baadhi yao wanakwambia wao wamezaliwa, wanasoma na wanakula kwa kufanya biashara hiyo.

"Niwaombe sana wananchi, tusiishi kwa mazoea, tuache kabisa biashara hii kwa sababu sote tunafahamu kwamba kulipa kodi ndio njia inayotuwezesha kujenga Tanzania yetu na mimi kama balozi nitaendelea kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi kuacha biashara hii ya magendo," alisema Balozi Zulfa.

Balozi Kumwembe alisema sababu kuu ya kuwahamasisha wananchi kuacha biashara za magendo ni kukosekana kwa uhakika wa ubora wa bidhaa zinazopitishwa katika njia zisizo rasmi na hivyo zinaweza kuhatarisha afya za wananchi.

"Dhumuni la kuzuia biashara za magendo kwanza ni kutukosesha mapato lakini vilevile hatuna uhakika na ubora wa bidhaa zenyewe kiasi kwamba zinaweza kuleta athari kwenye afya za walaji," alisema Balozi Kumwembe.

Balozi Subira aliwaomba wafanyabiashara kulipa kodi kwa hiari na kuacha kupitisha bidhaa kwenye njia za panya ambapo wakikamatwa bidhaa zao zote na vyombo vya usafiri vilivyotumika kusafirishia bidhaa hizo hutaifishwa ikiwa ni pamoja na kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kufungwa jela.

Ziara ya mabalozi hao katika mikoa ya Kasikazini ilimalizika jana ambapo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kupitia Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi, Richard Kayombo, ilibainisha kuwa itaendelea kutoa ushirikiano kwa mabalozi hao ili kuhakikisha wanafanya kazi yao ya kuelimisha na kuhamasisha wananchi kulipa kodi kwa hiari na wakati.

Mabalozi hao wa kodi waliotеuliwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, wakati akihitimisha mjadala wa Bunge la Bajeti mwezi Juni 2021, wamepata fursa ya kutembelea mipaka ya Namanga, Holili na Tarakea iliyoko katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro.

# THRDC yamwangukia Samia mgogoro wa ardhi Ngorongoro

**Na Enock Charles**

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC) umetaka kuwapo kwa usuluhishi wa kudumu katika mgogoro wa ardhi kati ya wakazi wa Wilaya ya Ngorongoro na Mamlaka ya Uhifadhi wilayani humo uliodumu kwa muda mrefu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mratibu wa Mtandao huo kitaifa, Onesmo Ole Ngurumwa, amemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuingilia kati kutatua mgogoro huo unaodaiwa kudumu tangu mwaka 1992 ili kuleta amani na utulivu wilayani humo.

"Taharuki imekuwa ikiibuka mara kwa mara katika kipindi cha miaka kadhaa toka mwaka 1992, mtu pekee tunayeona atafaa kutatua mgogoro ule asiyekuwa na maslahi ya upande mmoja ni mheshimiwa Rais," alisema Ngurumwa na kuongeza:

"Mheshimiwa Rais wale ni wananchi wake na Mamlaka ya Uhifadhi ipo chini yake kwa hiyo itakuwa vyema akileta suluhu ama ateuliwe mtu asiyekuwa na masilahi ya upande mmoja."

Mtandao huo umesema mpango wa serikali uliowekwa wazi na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, wa kutaka kuchukua kilometa za mraba 1,500 kutoka ardhi za vijiji vya Loliondo kwa ajili ya matumizi ya pekee ya uhifadhi na uwekezaji kwa kile kilichoelezwa kuwa ni masilahi ya taifa umeleta taharuki kwa wananchi hao wakihofia kuchukuliwa maeneo yao.

"Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ilitoa maelekezo ya kuwaondoa baadhi ya wananchi katika eneo la hifadhi kwa madai kuwa ni wahamiaji haramu na wengine kwa mamia kutakiwa kubomoa majengo yakiwamo shule na vituo vya afya," alisema Ngurumwa.

"Baada ya malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi zoezi hilo lilisitishwa hadi mwaka huu tena, ambapo mikakati mingi isiyo shirikishi imekuwa ikionekana kuelekeza baadhi ya watu kujiandaa kuondoka eneo la Tarafa ya Ngorongoro," alisema.

Mtandao huo ulizipongeza taasisi mbalimbali zilizojitahidi kutafuta suluhu ya mgogoro wa tatizo hilo kikiwamo Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani humo ambacho kwa mujibu wa mratibu huyo, kimekuwa kiunganishi kati ya wananchi na serikali.



Rais na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Barrick, Mark Bristow (kushoto), akitoa maelezo kwa Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko, Waziri wa TAMISEMI, Innocent Bashungwa na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema (katikati), jinsi mtambo wa kielekitroniki wa uchimbaji madini chini ya ardhi unavyofanya kazi wakati walipotembelea mgodi wa Bulyanhulu, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PM: Tutamsaidia Rais kwa uaminifu na weledi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema wasaidizi wote wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan wamejipanga kuhakikisha kwamba wanamsaidia kwa weledi wote, uaminifu ili malengo na matamanio yake ya kuwaletea Watanzania maendeleo yaweze kufanikiwa.

Hivyo, Majaliwa amewataka Watanzania waendelee kufanya kazi kwa bidii pamoja na kuwa na imani ya serikali, kwa sababu imedhamiria kuwatumikia kwa lengo la kuboresha na kuimarisha maendeleo ya mwananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Waziri Mkuu aliyasema hayo juzi alipozungumza na wananchi baada ya kukagua mradi wa ujenzi wa vyumba sita vya madarasa katika Shule ya Msingi Shikizi Kazaroho iliyoko wilayani Babati akiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo mkoani Manyara.

Alisema serikali imeendelea kuweka mipango ya kuboresha sekta ya elimu nchini ili kila mtoto apate elimu bora, hivyo alisisitiza kila kulipokuwa na shule ya msingi lazima kuwe na madarasa ya awali.

Nao wanafunzi wa shule hiyo wakizungumza mbele ya Waziri Mkuu walimshukuru Rais Samia kwa uamuzi wake wa ujenzi wa madarasa hayo yaliyojengwa kupitia fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19.

"Tunamshukuru Rais Samia kwani madarasa haya yaliyojengwa karibu na makazi yetu yametusaidia kutuondolea changamoto ya kutembea umbali mrefu kufuata elimu. Tunaomba na walimu wetu wajengewe nyumba kwani wanaishi mbali na hapa shuleni."

Kwa upande wake, Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Mwalimu Domonick Magula, alisema Shule ya Msingi Shikizi Kazaroho ilianzishwa mwaka 2018 ikiwa na wanafunzi 58 wa darasa la awali, ambapo kwa sasa ina jumla ya wanafunzi 332 kuanzia darasa la awali hadi darasa la tano. Madarasa hayo sita yamegharimu Sh. milioni 120.

Awali, Majaliwa alikagua maendeleo ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Babati, ambapo alisema kuwa ujenzi wa hospitali hiyo una lengo la kusogeza huduma za afya karibu na wananchi, hivyo utawapunguzia safari ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma hizo.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Dk. Festo Dugange, alisema serikali imetoa shilingi 300 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kisasa la kutolea huduma ya dharura katika Hospitali ya Wilaya ya Babati na Sh. milioni 90 za ujenzi wa nyumba tatu za watumishi.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Babati, Dk. Hoseah Madama, aliishukuru serikali kwa kutoa shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa hospitali ya wilaya hiyo.

Alisema mradi huo unajengwa kwa awamu mbili ambapo ya kwanza inajumuisha ujenzi wa majengo mawili ambayo ni jengo la wagonjwa wa nje na maabara na awamu ya pili inahusisha ujenzi wa majengo matano nayo ni utawala, mama na mtoto, kufulia, mionzi na stoo ya dawa.

# Watanzania waondolewa hofu ya ajira za Barrick

**Na Faustine Feliciane,** KAHAMA

SERIKALI imesema licha ya kampuni ya Barrick kuanza kuchimba madini kwa kutumia mfumo wa kompyuta ambapo mashine za uchimbaji zinaenda chini ya ardhi kwa zaidi ya kilometa 1.5 bila kuwa na mtu, hakuna Mtanzania atakayepoteza ajira yake kutokana na ujio wa teknolojia hiyo.

Mgodi wa Barrick wa Bulyanhulu ulioko Kahama umeanza kuchimba madini kwa kutumia teknolojia ya kisasa, kwamba mtambo ulioko chini ya ardhi unaendeshwa kwa kompyuta na mtaalamu ambaye anakuwa nje kwenye chumba maalum. Akizungumza juzi mgodini hapa, Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alisema hakuna mfanyakazi ambaye ataondolewa kazini kutokana na utaalamu huo na badala yake ameitaka Barrick kuwatafutia ajira mbadala wale wote ambao walikuwa wakichimba madini kwa kuendesha mitambo.

"Serikali tunaridhishwa na tunapongeza kwa juhudi zinazofanywa na mgodi huu kwa kuongeza teknolojia, lakini niseme hapa wale wafanyakazi wote ambao teknolojia hii mpya imechukua nafasi za kazi zao niombe mgodi uwatafutie ajira mbadala waendelee na kazi zao humu," alisema Biteko.

Alisema kuwa Rais Samia Suluhu Hassan anataka kuona kila uwekezaji unaofanywa hapa nchini unaleta manufaa kwa Watanzania.

Waziri Biteko alisema katika mgodi huo asilimia 96 ya wafanyakazi wake ni Watanzania na asilimia 41 kati yao wametoka kwenye maeneo yanayozunguka mgodi huo.

"Tutakuwa tunaendelea kufanya tathmini kila baada ya muda kwa pamoja Serikali na Barrick kuona tunavyoenda, lengo ni kuhakikisha kila upande unaendelea kunufaika," alisema Biteko.

Awali akizungumza mgodini hapo, Rais na Mtendaji Mkuu wa Barrick Gold Corporation, Mark Bristow alisema migodi ya Bulyanhulu na North Mara katika kipindi cha miaka miwili tangu ilipoichukuwa imeweza kufikisha uzalishaji wa zaidi ya wakia 500,000 za dhahabu zenye thamani ya zaidi ya Dola za kimarekani milioni 875 mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka jana.

"Mafanikio haya yamefikiwa wakati migodi yote miwili ikiendelea kuwa na hadhi ya ubora wa kimataifa ISO 45001 katika uzingatiaji usalama na ISO 14001 katika utunzaji wa mazingira ni jambo la kujivunia sana," alisema Bristow.

Alisema Barrick inaendelea kujiimarisha katika maeneo ya Bulyanhulu kutokana na kupata leseni sita za kutafiti madini katika maeneo yanayopakana na mgodi huo.

Aidha, alisema timu ya wataalamu wa jiolojia na utafiti wa kampuni hiyo wanaendelea kutafuta fursa katika maeneo mengine hapa nchini.

# MATUKIO KATIKA PICHA



1) Meneja wa Kiwanda cha Uchapishaji cha Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), Balasubramaniyan Venkadachalam, akitoa maelezo kuhusu uzalishaji wa magazeti kwa wanafunzi wa Shule ya Genesis, walipofanya ziara ya mafunzo katika ofisi za TGL, Mikocheni, Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



2) Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akionyeshwa na Mkurugenzi wa Kampuni ya Tanzanite Forever Lapidary, Faisal Juma Shabhai, madini ya Tanzanite ambayo yamechongwa na kampuni hiyo iliyoko kwenye jengo la soko la madini, Mererani wilayani Simanjiro, akiwa katika ziara ya kikazi ya mkoani Manyara jana. **PICHA: OWM**



3) Naibu Msajili wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Mhandisi David Jere (kulia), akizungumza katika ufunguzi wa mkutano wa makandarasi wazalendo, jijini Dodoma jana. Katikati ni Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Consolatha Ngimbwa na Makamu Mwenyekiti wa Bodi, Joseph Tango. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**



4) Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) Mkoa wa Ilala, Pilly Mwakasege, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu ufuatiliaji wa fedha za mpango wa maendeleo Sh. bilioni 5 kwa ustawi wa jamii wa taifa wilayani humo. **PICHA: JUMANNE JUMA**



5) Kamishna wa Kodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Herbert Kabyemela, akizungumza wakati akifungua kikao na wakaguzi wa hesabu, wahasibu na washauri wa masuala ya kodi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



6) Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde (wapili kushoto), akipata maelezo kutoka kwa mmiliki wa kitalu cha miche ya parachichi, Khadija Mchapakazi (kushoto), alipotembelea shamba hilo, wilayani Iringa juzi. Wengine ni Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo (watatu kushoto) na Mbunge wa Iringa Mjini, Jesca Msambatavangu. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

HABARI KITAIFA



Msafara wa magari ya viongozi wa Msumbiji, akiwamo Gavana wa Mkoa wa Tete na Meya wa Mji wa Tete uliosombwa na maji kwenye Mto Rovubwe jana, ingawa waliokolewa pamoja na abiria wengine. **PICHA: BBC**

# Jeshi Burkina Faso lakemewa pamoja na uungwaji mkono

**Ouagadougou, BURINA FASO**

UTAWALA mpya wa kijeshi Burkina Faso unakabiliwa na ukosoaji kutoka jamii ya kimataifa, pia unapata uungwaji mkono kutoka ndani ya nchi.

Rais Roch Marc Christian Kabore bado anashikiliwa mahali na eneo lisilojulikana.

Wafuasi wa utawala mpya wa kijeshi, Burkina Faso waliandamana jana katika mitaa ya mji mkuu Ouagadougou wakati Umoja wa Mataifa (UN), Ufaransa na nchi jirani za ukanda wa Sahel zikilaani mapinduzi hayo ya karibuni ya kijeshi.

Maofisa wa jeshi walimkamata Rais Roch Marc Christian Kabore, Jumatatu wakati kukiwa na hasira kuhusu anavyoushughulikia uasi wa itikadi kali.

Koloni hilo la zamani la Ufaransa, sasa liko mikononi mwa chama cha Patriotic Movement for Preservation and Restoration - MPSR, jina la utawala wa kijeshi ukiongozwa na Luteni Kanali Paul-Henri Sandaogo Damiba.

Mamia kadhaa ya watu walikusanyika katikati mwa mji mkuu Ouagadogou, wakisherehekea na kupeperusha bendera kuonyesha uungaji mkono kwa wanajeshi wa mapinduzi.

Jeshi lilitangaza jana, kurejea kwa safari za angani wakati likifungua mipaka ya ardhini kwa magari yanayosafirisha bidhaa za kiutu, kijeshi na bidhaa muhimu.

Afrika Magharibi, imekumbwa na matukio matatu ya mapinduzi katika muda wa chini ya miezi 18, kuanzia Mali Agosti mwaka 2020, kisha Guinea Septemba mwaka jana.

Katibu mkuu wa UN, Antonio Guterres alikashifu mapinduzi hayo ya mara kwa mara akisema hayakubaliki, akiongeza kuwa jamii za kidemokrasia ni thamani ambayo lazima ihifadhiwe.

"Nina wasiwasi mkubwa kuhusu mapinduzi ya karibuni Burkina Faso.

Jukumu la jeshi ni kulinda nchi zao na watu wao na sio kuzishambulia serikali na kupigania madaraka.

Jumuiya ya Kiuchumi ya Mataifa ya Afrika Magharibi (ECOWAS), ambayo inajumuisha Burkina Faso, iliandaa mkutano maalumu wa kilele na kutoa taarifa iliyolaani vikali mapinduzi hayo.

Uingereza na Afrika Kusini, pia ilijiunga na sauti za ukosoaji.

Muungano wa kijeshi wa nchi za Sahel unaopigana dhidi ya uasi wa itikadi kali - G5 Sahel ambao unajumuisha Chad, Mali, Mauritania na Niger, ulikemea kile ulichokiita jaribio la kuvuruga utaratibu wa kisheria nchini Burkina Faso ambayo ni mwanachama wake watano.

*DW*

# Mafuriko yaua watu tisa Uganda

**Kampala, UGANDA**

WATU tisa, akiwamo mtoto mmoja, wamefariki kufuatia mafuriko na maporomoko ya udongo katika Wilaya ya Kisoro, Kusini-Magharibi mwa Uganda.

Miili minane kati ya miili hiyo, ilikuwa imefukuliwa kufikia Jumanne asubuhi, limesema Shirika la Msalaba Mwekundu, Uganda.

"Watu tisa na mtoto ambaye aliangukiwa na udongo wakati alipokuwa akikimbia. Kwa hiyo hakuna anayejua ni wapi hasa pa kuchimba ,"lilisema.

Mvua kubwa imeharibu nyumba, barabara, na miundo mbinu.

Jumatano, shirika hilo lilisema kuwa, linatoa msaada wa dharura kwa ajili ya familia 300 zilizoathiriwa na mkasa huo.

Awali shirika hilo lilituma picha kwenye Twitter, zilizoonyesha baadhi ya uharibifu.

*BBC*

# Waliberia waghadhabika kifo cha mtoto baada ya kubakwa

**Monrovia, LIBERIA**

KIFO cha msichana wa umri wa miaka 13, kilichotokea baada ya kudaiwa kubakwa na mwanamume mwenye umri wa miaka 47 katika mji mkuu, Monrovia kimezua hisia.

Kisa hicho cha unyanyasaji wa kingono unaohusisha mtoto ni cha tatu katika kipindi cha mwezi mmoja na kusababisha maandamano.

Blessing Molton, alikufa siku ya Jumatatu, wiki moja baada ya kushambuliwa na siku moja kabla ya kufanyiwa upasuaji, kulingana na gazeti la Frontpage la Liberia.

Waandamanaji walikusanyika nje ya bunge siku ya juzi kutaka juhudi zaidi kufanywa kukomesha unyanyasaji wa kingono.

Waandamanaji walishikilia mabango ya kutaka kukomesha ubakaji na haki kwa Blessing Molton.

**BBC**

# Msafara wa watu mashuhuri wasombwa na maji mto Msumbiji

**Maputo, MSUMBIJI**

MSAFARA wa watu mashuhuri umesombwa na maji kwenye mto Magharibi mwa Msumbiji baada ya kimbunga Ana, kukumba nchi hiyo.

Gavana wa Mkoa wa Tete na Meya wa Mji wa Tete, walikuwa wakirejea kutoka kwa shughuli ya kutathmini uharibifu uliosababishwa na kimbuka hicho, wakati msafara wao uliposombwa na maji ya Mto Rovubwe.

Inasemekana viongozi hao waliokolewa pamoja na abiria wengine.

Hata hivyo, watu watatu akiwamo mwandishi wa habari bado hawajulikani waliko.

Mkoa huo, umeathiriwa vibaya na kimbunga hicho.

Watu sita miongoni mwao watoto wamefariki, wengi wao baada ya kuangukiwa na kuta.

Mji wa Tete umetenganishwa na Wilaya ya Moatise, baada ya daraja la Mto Rovubwe, unaotokana na Mto Zambezi, kuanguka.

Kimbunga Ana kiligonga Kaskazini mwa nchi siku ya Jumatatu na kusababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu ikiwemo nyumba, hospitali, shule, nguzo za umeme na madaraja.

Ijapokuwa kimbunga hicho kimetulia, watabiri wa hali ya hewa wanasema, mvua kubwa ikiandamana na upepo mkali na ngurumo za radi, itaendelea kushuhudiwa katika maeneo ya kati na kaskazini.

**BBC**

# Yanga SC yatoa neno mkataba wa Mukoko

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema imemuuza kiungo Mukoko Tonombe kwenda TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemkorasi ya Congo bila kuweka vipengele vyovyote vile vinavyoweza kumzuia kucheza timu yoyote hapa nchini, hivyo hata kama akishindwa mazingira anaweza kujiunga na timu nyingine.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, amesema Yanga haina dhiki ya kuweka vipengele vya ajabu kwenye mikataba ya wachezaji wake inayowauza, hivyo Mukoko ana uhuru wake, kama akishindwa kupata namba au kuendana na mazingira yoyote, hakuna chakumzuia kujiunga na klabu yoyote nchini Tanzania.

**"Yanga haina dhiki ya ku weka vifungu vya ajabu ajabu kuwa anakwenda kule akishindwa mazingira basi ni lazima arudi kwetu, sasa kama akivunjika mguu atarudi kufanya nini? Kuna klabu ambazo zina tabia hiyo, sisi hatumkomoi mtu, kama atapata timu ny ingine inayomhitaji Tan zania sawa hatuna haja naye, lakini kama tuna haja naye tutafanya ma zungumzo upya na klabu yake na tutamsajili upya. Hatuna ulazima wa kuweka vitu kwenye mikataba ya wachezaji wetu sijui asi chezee timu gani, hapana yeye ni mcheza mpira na n i mfanyakazi," alisema.**

Hapana shaka kijembe hicho kilikuwa kikirushwa kwa watani wao wa jadi, Simba ambao hivi karibuni walimrudisha kiungo wao Clatous Chama kutoka RS Berkane ya Morocco.

Inadaiwa klabu ya Simba iliweka baadhi ya vipengele ambavyo vilirahisisha mchezaji huyo kurejea, huku kukiwa na kipengele cha kutomruhusu kusajiliwa na timu yoyote ya hapa nchini.

Yanga imemuuza Mukoko kwenye klabu ya TP Mazembe baada ya kuhudumu kwenye klabu hiyo kwa msimu mmoja na nusu, ilipomsajili kutoka AS Vita Club kutoka huko huko nchini DR Congo.

# KOCHA SIMBA QUEENS AANZA TAMBO LIGI KUU WANAWAKE

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Simba Queens, Sebastian Nkoma, amesema kila timu ishinde mechi zake na kwamba hesabu zake kubwa kwa sasa ni kuhakikisha anapata pointi 12 katika michezo minne ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Kauli hiyo aliitoa juzi baada ya timu yake hiyo kuibuka na ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya The Tigers Queens uliochezwa katika Uwanja wa Simba Mo Arena, Bunju E nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

Katika mchezo huo, shukrani hazina budi kuwaendea straika hatari wa Simba Queens, Opah Clement, mshambuliaji mwingine Mmalawi Sabinah Thom, Mnigeria Olaiya Barakat dakika ya 30, Amina Ramadhani akiifunga timu ambayo alichezea msimu uliopita na kiungo Mrundi Joelle Bukuru aliyehitimisha ushindi huo dakika ya 90.

Ushindi huo pia unakuwa wa saba mfululizo kwa mabingwa hao watetezi, wakiwa na ushindi wa asilimia mia moja, wakifikisha pointi 21, mabao 42 ya kufunga, ikiwa imeruhusu mawili wakati huu ikizidi kujichimbia kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo yenye timu 12.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Nkoma alisema ligi imekuwa na ushindani mkubwa lakini hana presha kabisa na wapinzani wake zaidi ya kupambana na kikosi chake kutafuta pointi tatu katika kila mechi.

Alisema mikakati yao ni kuhakikisha wanashinda michezo hiyo mitano na kupata pointi 13 ili kuendelea kujiimarisha kileleni na hatimaye kutetea ubingwa wao.

"Hakuna mechi rahisi, ukingalia leo mechi yetu dhidi ya The Tigers Queens, inakupa taswira ya ugumu wa mechi, licha ya kupata ushindi, unaona wapinzani wetu ni wazuri ila tumetumia makosa madogo kupata ushindi.

"Timu inahitaji kupata ushindi, kwanza tunahitaji kufikia malengo yetu ya kushinda mechi zetu nne za kwanza baada ya hizo tutaangalia mechi zijazo," alisema Nkoma.

Katika mechi nne ilizobakiza kabla ya kukamilika kwa mzunguko wa kwanza, Simba Queens itacheza tatu katika uwanja wake wa nyumbani wa Mo Arena dhidi ya Fountain Gate utakaopigwa Januari 25 na 28 watacheza dhidi ya Mlandizi Queens kabla ya Februari 4, mwaka huu kuikaribisha JKT Tanzania.

Baada ya hapo Februari 7, mwaka huu watatoka kwenda Dodoma kuvaana na Baobab Queens.

**DOGO UNATISHA...**



Winga wa Simba na timu ya Taifa ya Malawi, Peter Banda (kushoto), akiwa na kiungo wa timu ya Taifa ya Morocco, Achraf Hakimi, baada ya mechi ya hatua ya 16-bora ya michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon), kumalizika juzi usiku kwa Wamorocco hao kushinda mabao 2-1. Katika mechi hiyo Hakimi ndiye aliyefunga bao la ushindi dakika ya 70. **PICHA: MTANDAO**

# *Mbeya City kutumia FA kusoma mbinu Yanga*

**Na Saada Akida**

KLABU ya Mbeya City imesema itatumia wiki ya Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup, kujiimarisha kila idara hususan safu ya ulinzi kuelekea mechi yao ijayo ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Yanga.

Mbeya City iliyotolewa kwenye michuano hiyo ya FA katika raundi ya 32 na African Sports kwa mikwaju ya penalti ya 4-3, baada ya kukamilika kwa dakika 90 bila ya kufungana.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule, alisema hawako katika michuano ya Kombe la Shirikisho baada ya kuotolewa jambo ambalo sasa linampa nafasi ya kutumia muda huo kuwasoma zaidi Yanga.

Alisema msimu huu amedhamiria 'kuchafua' watu, na kwamba wakati akiwasoma Yanga katika michezo ya Kombe la Shirikisho, pia atatumia muda huo kufanyia kazi mapungufu ya kikosi chake kujiimarisha zaidi katika safu yake ya ulinzi na ushambuliaji.

"Hatukufanikiwa kusonga mbele katika michuano ya Kombe la Shirikisho, sasa tunatumia nafasi hiyo kujiimarisha kuelekea mechi yetu dhidi ya Yanga ili kuhakikisha nao tunawachafua kama kilichowakuta Simba," alisema Lule.

Alisema ana tumai utakuwa mchezo wa ushindani mkubwa na mgumu na kwamba msimu huu amedhamiria kuweka historia ya kuzifunga timu hizo na kumaliza ligi katika nafasi ya juu.

"Yanga watakuwa nyumbani, hilo halitatufanya kuhofia kwa sababu tumekuwa tukiwasoma ubora na madhaifu yao, ninaamini kipindi wao wanacheza FA, tutakitumia kujiimarisha zaidi," alisema kocha huyo.

Alisema wanatarajia kufunga safari mapema kwenda Dar es Salaam kwa ajili ya kuzoea hali ya hewa ya jiji hilo kabla ya siku ya mchezo huo.

Mbeya City wanatarajiwa kuingia jijini Dar es Salaam Februari Mosi, tayari kwa ajili ya mchezo dhidi ya Yanga utakaopigwa Februari 5, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamini Mkapa.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MANE: TAYARI NIMETOKA HOSPITALI, NIKO FITI KABISA

## Anatakiwa kufanya vipimo kadhaa, tumempigia simu, anasema yuko sawa, hakutaka kuondoka, lakini...

**YAOUNDE, CAMEROON**

SADIO Mane amesema "yote yako sawa" baada ya kupelekwa hospitalini kutokana na mgongano mbaya wa vichwa wakati Senegal ikishinda dhidi ya Cape Verde kwenye hatua ya 16-bora katika michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), juzi.

Bao zuri la Mane lilikiwezesha kikosi hicho cha kocha, Aliou Cisse kupata ushindi wa mabao 2-0 na kutinga robo fainali ya mashindano hayo.

Hata hivyo, mshambuliaji huyo wa Senegal, Mane alitolewa nje muda mfupi baadaye, akionekana bado anahisi madhara ya mgongano wa awali na Vozinha.

Alipokuwa akiufukuza mpira uliodunda kwenye eneo la hatari, Mane aligongana na kipa wa Cape Verde, ambaye alitolewa kwa kadi nyekundu baada ya mapitio ya VAR.

Picha iliyowekwa kwenye akaunti rasmi ya Twitter ya Kombe la Mataifa ya Afrika - ilifichua kwamba Vozinha alimtembelea mshambuliaji huyo wa Liverpool hospitalini baada ya mchezo huo.

Akishiriki picha hiyo kwenye Instagram, Mane aliwaambia wafuasi wake milioni 9.1: "Yote ni sawa. Asanteni nyote kwa ujumbe."

Sasa atakuwa na matumaini ya kuwa fiti kwa robo fainali, ambapo Senegal itacheza na Mali au Equatorial Guinea Jumapili.

Nahodha Kalidou Koulibaly alisema baada ya mchezo huo: "Sadio Mane anatakiwa kufanya vipimo kadhaa. Tumempigia simu, na anasema yuko sawa. Hakutaka kuondoka, lakini hakuna hatari. Ni mchezaji muhimu kwetu."

Ripoti baadaye Jumanne jioni zilisema Maneameruhusiwa kutoka hospitalini.

## ZISIKUPITE

### LENO KUONDOKA ARSENAL

GOLIKIPA wa Arsenal, Bernad Leno mwenye umri wa miaka 29, anashinikiza kuondoka Emirates, huku Newcastle wakiwa na nia ya kumsajili kipa huyo wa kimataifa wa Ujerumani kwa mkataba wa mkopo hadi mwisho wa msimu. ***(Football.london)***

### NEWCASTLE YAKATALIWA

OFA ya Tottenham ya takriban pauni milioni 38 kwa winga wa Porto kutoka Colombia, Luis Diaz, 25 imekataliwa. ***(Guardian)***

### BENTANCUR KUTUA VILLA

KLABU ya Aston Villa inakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili kiungo wa kati wa Juventus na Uruguay, Rodrigo Bentancur mwenye umri wa miaka 24. ***(Football Insider)***

### SEVILLA YAMZUIA CARLOS

KLABU ya Newcastle haitamsajili mlinzi wa Brazil, Diego Carlos kwani Sevilla wameamua kumbakisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Fabrizio Romano)***

### WIJNALDUM ANUKIA ARSENAL

KIUNGO wa kati wa Paris St-Germain na Uholanzi, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 31, yuko tayari kuhamia Arsenal. ***(Sky Sports - kupitia Daily Mail)***

### LIVER, CITY KWA TIELEMANS

LIVERPOOL na Manchester City ndizo klabu zinazovutiwa zaidi kumsajili kiungo wa kati wa Leicester na Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 24. ***(Fichajes - kupitia Leicester Mercury)***

### VLAHOVIC, JUVE WAKUBALIANA

KLABU ya Juventus imefikia makubaliano ya kumsajili mshambuliaji, Dusan Vlahovic kutoka Fiorentina, na hivyo kuzima matumaini yoyote ya Arsenal kumnasa mchezaji huyo wa kimataifa wa Serbia mwenye umri wa miaka 21, pale Emirates. ***(Goal)***

### NDOMBELE ATAKIWA EVERTON

EVERTON wamejitokeza kutafuta saini ya kiungo wa kati wa Tottenham na Ufaransa, Tanguy Ndombele mwenye umri wa miaka 25. ***(Sky Sports)***

### DELE AWINDWA KLABU EPL

KLABU ya Brighton wanamfuatilia kiungo wa Tottenham Hotspur, Dele Alli kwa nia ya kumnunua kwa mkopo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, lakini Burnley, Everton na Newcastle pia wanahusishwa na Mwingereza huyo. ***(Mail)***

### ORSIC ATAKIWA BURNLEY

KLABU ya Burnley inakaribia kumsajili kiungo wa Dinamo Zagreb na Croatia, Mislav Orsic mwenye umri wa miaka 29. ***(Sky Sports)***

### ARTETA ATAKA NYOTA

MSHAMBULIAJI wa Everton, Dominic Calvert-Lewin mwenye umri wa miaka 24, kiungo wa kati wa Wolves, Ruben Neves mwenye miaka 24 na Douglas Luiz wa Aston Villa mwenye miaka 23, wako kwenye orodha ya kocha wa Arsenal, Mikel Arteta.

### JOHNSON APANDIWA DAU

KLABU ya Brentford imeongeza ofa yao kwa kiungo wa Nottingham Forest, Brennan Johnson, ambaye pia anafuatiliwa na Newcastle. ***(Independent)***

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 878

MECHI KALI
SAUDI ARABIA
VERSUS
OMAN
1 | 1.37
X | 4.13
2 | 7.69

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# JUVENTUS MAMBO SAFI KWA VLAHOVIC

**TURIN, Italia**

KLABU ya Juventus wamekubaliana na Fiorentina kumsajili mshambulliaji Dusan Vlahovic kwa ada ya uhamisho kiasi cha pauni milioni 62.8 kwenye dirisha hili la Januari.

Juventus na Fiorentina wamekuwa wakifanya majadiliano kwa muda mrefu, kuhusu ada ya uhamisho wa mshambuliaji huyo wa kimataifa kutoka Serbia.

Fiorentina walikuwa na mpango wa kumuuza mchezaji huyo wa kimataifa mwenye umri wa miaka 21, katika dirisha hili ili kuongeza faida baada ya kubakisha miezi 18 kwenye mkataba wake, huku klabu za England ambazo ni Arsenal na Tottenham zikiwa pia zinawania saini yake.

Mkurugenzi wa Klabu ya Fiorentina, Daniele Prade aliambia SportItalia: "Ni thamani nzuri zaidi ya euro milioni 70 pasipo makubaliano ya ubadilishanaji wa mchezaji yeyote na hakuna malipo yoyote ambayo yatakuwa upande wetu.

"Milango yote iko wazi kwenye suala hili, kwa sababu tunahitaji kuelewa ni nini mchezaji na wakala wake wanataka kufanya, tuko tayari kwa mazungumzo na tumeshatoa ofa mbalimbali kwa ajili ya kumuongeza mkataba, na pia kuna ofa ya kumuuza ina ushawishi mkubwa.

"Nasema hivi kwa sababu klabu yetu inatengeneza faida ya euro milioni 75 kwa mwaka na hatuwezi kuipoteza rasilimali muhimu bure bure tu."

Vlahovic amekuwa na msimu mzuri tangu msimu ulioisha ambapo aliweza kufunga mabao 21 kwenye michezo 40 kwa klabu yake pia msimu huu ameendeleza makali yake baada ya kufunga mabao 20 kwenye mechi 24




# United kuamua kuhusu Lingard

**MANCHESTER, England**

KIMSINGI kwa hali ilivyo kwa sasa, klabu ya Manchester United ndio wataamua kama Jesse Lingard anaondoka sasa hivi au mwishoni mwa msimu.

Newcastle United wameweka mezani kila walichojipanga nacho ili kumsajili Lingard Januari hii.

Kwa upande wa Lingard mwenyewe, hana mpango wa kubaki United baada ya mkataba wake kumalizika msimu huu.

Hana tatizo na kwenda pale kwenye dimba la St. James' Park kwa nusu ya msimu huu uliosalia, lakini kikwazo ni Man United wenyewe.

Inaripotiwa kuwa, Man United haijatoa jibu lolote kwa Newcastle hadi sasa.

Ingawa uongozi wa Newcastle unaendelea kuweka jitihada kukamilisha hili ndani ya siku chache zilizobaki kwenye dirisha hili la usajili.

Wanachokifanya United pengine kinaweza kuwagharimu zaidi mbeleni. Lingard amebakiza miezi michache kumaliza mkataba wake na timu hiyo.

Endapo hatotolewa kwa mkopo au kuuzwa majira haya, United wajiandae kutoka patupu ifikapo Juni 30, mwaka huu.

Muda huo, Lingard atakua mchezaji huru na United haitohusika na hata thumni ya usajili wa mchezaji huyo.



## HABARI MICHEZO

# ,152,880






Mshindi wa Jackpot Bonasi ya SportPesa, Hamis Moshi Masanja kutoka Chuo Kikuu cha UDOM, jijini Dodoma akionyesha mfano wa hundi ya shilingi 8,189,223, baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 11 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. Jackpot inayoshindaniwa wiki hii imefika Sh. 878,152,880. **PICHA: SPORTPESA**

# Mwanafunzi UDOM afunguka ushindi mamilioni ya SportPesa

**Na Mwandishi Wetu**

MWANAFUNZI wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Hamisi Moshi Masanja, Jumatatu wiki hii ameamka mfuko umetuna baada ya kujaribu bahati yake kwa kubashiri Jackpot ya SportPesa na kuibuka mshindi wa Bonasi ya Jackpot ya Sh. milioni nane kutokana na kupatia mechi 11 kati ya 13.

Hamis (26), ambaye ni mwenyeji wa Kahama mkoani Shinyanga, lakini kwa sasa akiwa masomoni UDOM, akifanya shahada ya biashara akibobea kwenye masoko, amesema njia pekee ya kushinda ni kutokata tamaa ya kubashiri.

Akizungumza na mwandishi wetu katika Ofisi za Sportpesa, jijini Dar es Salaam baada ya utambulisho na makabidhiano ya mfano wa hundi, Hamis alisema juhudi yake ya kucheza na kutokata tamaa, ndizo zilizompatia ushindi.

"Unajua nimeanza kucheza na Sportpesa miaka mitatu iliyopita, na kwa muda wote huo, nimekuwa najaribu bahati yangu bila kuchoka. Mfano wiki ile ya nyuma, nilishinda mechi nne tu kati ya 13, lakini sikukata tamaa ya kuacha kucheza. Nilikuwa navutiwa sana, kwa namna nilivyokuwa naona vijana wenzangu, walivyokuwa wanashinda mara kwa mara," alisema.

Alifafanua kuwa mara kwa mara alikuwa na utamaduni wa kuperuzi kurasa za mitandao ya kijamii ya Sportpesa na kuona washindi kila mara. "Nilihamasika sana kwa jinsi nilivyoona wenzangu wakiwekwa kwenye kurasa za Instagram, Facebook na Twitter za Sportpesa, nilitamani na mimi siku moja nibahatike kutokea, na kweli leo na mimi ni mmoja wa washindi."

Akielezea namna alivyocheza Jackpot ya wikiendi iliyoisha ambayo ndio iliyompatia ushindi, Hamis anasema aliziona mechi za ushindi siku ya Jumatano iliyopita na kisha alijipa siku mbili za kufanya tathmini na uchambuzi wa kina.

"Unajua Jumatano nilifungua Sportpesa App na kukuta timu kumi na tatu zilizowekwa kwa ajili ya Jackpot. Niliangalia na kufuatilia mwenendo wa kila timu zilizowekwa na kujua namna ya kuzicheza.

"Ninawaomba vijana wenzangu na Watanzania kwa ujumla wacheze na Sportpesa kuanzia 'multibet', 'single bet' na hata hii Jackpot ambayo nimeshinda mimi timu 11."

Kwa upande wa Meneja Uhusiano wa Sportpesa, Sabrina Msuya, aliwaasa Watanzania kutokata tamaa na kujaribisha bahati yao kwa kucheza kila mara.

"Niwaombe sana kujaribu bahati zenu kwani Jackpot sasa imepanda wiki hii mpaka Sh. 878,152,880. Lakini hata kama hujabahatika kushinda Jackpot, basi Jackpot bonasi inakusubiri kwa watakaobashiri kwa usahihi mechi 10 hadi 12," alisema Sabrina.

d




## JACKPOT
## MECHI WIKI HII

**BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13**

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 29/01/22 | 18:00 | Amorebieta vs Girona | 2.80 | 3.09 | 2.50 |
| 02. 29/01/22 | 18:00 | Tranmere vs Forest Green | 2.64 | 3.18 | 2.59 |
| 03. 29/01/22 | 18:00 | Oldham vs Rochdale | 2.80 | 3.25 | 2.41 |
| 04. 29/01/22 | 18:15 | Nancy vs Amiens | 2.52 | 3.16 | 2.77 |
| 05. 29/01/22 | 23:00 | Real Oviedo vs Almeria | 2.75 | 3.09 | 2.55 |
| 06. 29/01/22 | 23:00 | SBV Excelsior vs Emmen | 2.56 | 3.49 | 2.46 |
| 07. 30/01/22 | 16:30 | Vicenza vs Alessandria | 2.66 | 3.05 | 2.66 |
| 08. 30/01/22 | 18:30 | FC Sion vs Grasshoppers | 2.56 | 3.40 | 2.56 |
| 09. 30/01/22 | 18:30 | FC Vizela vs Vitoria Guimaraes | 2.90 | 3.20 | 2.47 |
| 10. 30/01/22 | 19:00 | Cardiff vs Nottingham | 2.55 | 3.20 | 2.80 |
| 11. 30/01/22 | 20:30 | PAOK vs Olympiakos | 2.61 | 3.10 | 2.71 |
| 12. 30/01/22 | 23:00 | Lens vs Monaco | 2.77 | 3.26 | 2.46 |
| 13. 30/01/22 | 23:00 | Ponferradina vs Tenerife | 2.42 | 3.11 | 2.91 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## ALHAMISI - 27/01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3100 | Dynamo Kiev vs Bodo Glimt | 1.67 | 3.94 | 4.03 |
| 13:00 | 3641 | Japan vs China | 1.19 | 5.57 | 12.48 |
| 15:00 | 2970 | Lebanon vs South Korea | 6.15 | 3.70 | 1.50 |
| 16:00 | 1249 | Rutsiro FC vs Musanze | 2.25 | 2.93 | 3.17 |
| 16:00 | 1492 | Bugesera FC vs Gicumbi | 1.78 | 3.37 | 4.14 |
| 16:00 | 1690 | Espoir FC vs Gorilla FC | 1.70 | 3.56 | 4.33 |
| 16:00 | 2309 | Mukura vs Etincelles | 1.76 | 3.33 | 4.34 |
| 16:00 | 3222 | Nkana FC vs Kabwe Warriors | 1.91 | 2.94 | 4.24 |
| 16:00 | 5301 | Rayon Sports FC vs Gasogi United | 1.66 | 3.48 | 4.74 |
| 16:00 | 5546 | Etoile de Lest vs AS Kigali | 5.97 | 3.75 | 1.50 |
| 17:00 | 1014 | Australia W vs Thailand W | 1.01 | 18.25 | 28.82 |
| 17:00 | 3845 | Philippines W vs Indonesia W | 1.02 | 22.00 | 30.00 |
| 17:00 | 4739 | Delhi Dynamos FC vs Hyderabad FC | 3.52 | 3.52 | 1.88 |
| 17:30 | 4127 | Iran vs Iraq | 1.37 | 4.04 | 8.28 |
| 18:00 | 1525 | America Mexico U20 vs Atlas U20 | 1.75 | 3.75 | 3.80 |
| 18:00 | 4564 | United Arab Emirates vs Syrian Arab Republic | 2.00 | 3.08 | 3.61 |
| 18:00 | 5960 | Bahrain vs Uganda | 2.41 | 3.05 | 3.15 |
| 20:00 | 3280 | Sporting CP U23 vs FC Vizela U23 | 1.94 | 3.52 | 3.33 |
| 20:00 | 4806 | Maccabi Bnot Emek Hefer W vs MS Kiryat Gat W | 4.63 | 4.05 | 1.57 |
| 20:15 | 2274 | Saudi Arabia vs Oman | 1.37 | 4.13 | 7.69 |
| 20:30 | 2079 | Maccabi Kishronot Hadera W vs Hapoel Beer Sheva W | 1.56 | 4.25 | 4.44 |
| 20:30 | 3286 | Puskas Akademia vs Ferencvaros TC | 3.14 | 3.42 | 2.05 |
| 21:00 | 2116 | Uniclinic CE vs Pacajus | 3.67 | 3.33 | 1.89 |
| 21:00 | 2513 | UD Extremadura vs CF Talavera De La Reina | 16.42 | 6.18 | 1.14 |
| 21:00 | 4615 | Cruz Azul W vs FC Juarez W | 1.47 | 4.24 | 5.39 |
| 21:30 | 5555 | Madureira RJ vs Resende RJ | 2.05 | 3.14 | 3.42 |
| 21:30 | 5871 | Taguatinga EC DF vs Luziania DF | 1.48 | 3.86 | 5.98 |
| 21:30 | 5925 | Ferroviario CE vs Crato EC CE | 1.08 | 7.89 | 22.13 |
| 21:45 | 3563 | Hapoel Marmorek Rehovot W vs Hapoel Nir Ramat Hasharon W | 5.20 | 4.53 | 1.46 |
| 22:00 | 1675 | Caucaia vs Maracana CE | 2.15 | 2.99 | 3.33 |
| 22:00 | 4919 | Atletico Madrid B vs Villaverde Boetticher | 1.24 | 5.00 | 10.58 |
| 22:00 | 5090 | Icasa CE vs Iguatu CE | 4.80 | 3.65 | 1.73 |
| 22:30 | 2833 | Atletico Cliper Clube AM vs Penarol AM | 2.07 | 3.42 | 3.08 |
| 22:30 | 4022 | Nacional AM vs JC Futbol Clube AM | 1.43 | 4.33 | 5.97 |
| 22:30 | 4235 | Arsenal W vs Brighton and Hove Albion W | 1.06 | 8.85 | 24.04 |
| 22:45 | 1375 | Brugge vs Union Saint Gilloise | 2.03 | 3.54 | 3.34 |
| 23:00 | 3414 | UD Logrones vs CD Calahorra | 2.13 | 3.08 | 3.27 |
| 23:15 | 5243 | GD Estoril vs FC Arouca | 1.96 | 3.30 | 3.84 |

## IJUMAA - 28/01/2022

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 3933 | Ecuador vs Brazil | 3.25 | 3.15 | 2.30 |
| 02:00 | 2108 | Paraguay vs Uruguay | 3.09 | 2.99 | 2.48 |
| 02:30 | 3994 | Fluminense vs Bangu RJ | 1.15 | 6.15 | 14.40 |
| 03:00 | 4878 | USA vs EL Salvador | 1.17 | 5.78 | 14.45 |
| 03:00 | 5894 | Jamaica vs Mexico | 5.19 | 3.27 | 1.66 |
| 03:15 | 4466 | Chile vs Argentina | 2.60 | 3.09 | 2.84 |
| 03:30 | 2134 | SAO Jose RS vs Guarany de Bage FC | 1.68 | 3.50 | 5.60 |
| 03:30 | 5678 | Guarani SP vs Sao Paulo | 4.44 | 3.62 | 1.67 |
| 04:05 | 3340 | Honduras vs Canada | 3.70 | 3.12 | 1.96 |
| 04:10 | 1025 | Deportivo Pereira vs America De Cali | 2.65 | 3.03 | 2.55 |
| 05:05 | 5817 | Costa Rica vs Panama | 2.09 | 2.98 | 3.51 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Alhamisi Januari 27, 2022
Nipashe



Mane: Tayari nimetoka hospitali, niko fiti UKURASA 29

KAZI KAZI!...



Beki wa Simba, Henoc Inonga Baka (chini), akiwa amechezewa madhambi na mshambuliaji wa Kagera Sugar, Hassan Mwatelema, katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Kaitaba, Bukoba jana. Kagera Sugar ilishinda bao 1-0. **PICHA: SIMBA**

## Nabi amtaja Ushindi hesabu Kombe FA

**Na Saada Akida**

WAKATI akiendelea kukiandaa kikosi chake kuelekea mechi ya Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup dhidi ya Mbao FC Jumapili wiki hii, Kocha wa Yanga, Nasreddine Nabi, ametaja wachezaji atakaowapa nafasi huku akimchambua winga mpya, Chiko Ushindi.

Jumapili Yanga itakuwa mwenyeji wa mchezo huo utakaopigwa katika Uwanja wa CCM Kirumba baada ya kuhamishiwa huko kutokana na ule wa Benjamin Mkapa uliopangwa awali, kuwa na matumizi mengine.

Akizungumza na Nipashe kuelekea mchezo huo, Nabi alisema anaamini hakuna mechi ambayo itakuwa rahisi kwao kwa sababu timu yoyote inapokuwa katika mashindano hujiandaa vizuri, hivyo hata Mbao FC itawapa ushindani mkubwa hasa ukizingatia ni michuano ya mtoano.

"Hii ni mechi gumu na ushindani ukiangalia anayepoteza hapa anatolewa na akishinda anasonga mbele, tunahitaji kwenda kutafuta matokeo mazuri tunalazimika kujiandaa vizuri kuelekea mchezo wetu huo," alisema kocha huyo.

Nabi alisema anatarajia kuwapa nafasi wachezaji wengi ambao hawachezi mara kwa mara na kwamba tayari Ushindi ambaye amesajiliwa katika dirisha dogo, yupo katika programu maalum ya kumjenga kimwili na kumrejesha katika ubora wake.

"Ushindi ni mchezaji mzuri, amesajiliwa kwenye kikosi cha Yanga kutokana na uwezo wa kutumia miguu yote miwili jambo ambalo ni nadra kwa wachezaji wengi wanaocheza nafasi ya winga," alisema Nabi.

# SIMBA YAPAKATWA TENA

## ●●● Wachezaji wajilaumu wenyewe kukosa mabao, sasa yawaachia Yanga kutamba kileleni kwa pointi 10 zaidi huku...

**Na Adam Fungamwango**

BAO lililofungwa na straika wa zamani wa timu hiyo, Hamisi Kiiza, limewafanya Mabingwa Watetezi, Simba kupoteza mechi ya pili msimu huu kwenye Ligi Kuu Tanzania, Bara kwa kufungwa 1-0 na Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera jana.

Dakika ya 70 ilikuwa chungu kwa wanachama na mashabiki wa timu hiyo wakati Kiiza, aliyeichezea Simba msimu wa 2015/16, akiingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Ally Ramadhani, na kuunasa mpira mrefu uliopigwa na Ally Nassor 'Ufundu', kipa Aishi Manula akiwa anatoka golini kumfuata ili kuuwahi lakini akaudokoa na kufunga kirahisi.

Ni mechi ya tatu mfululizo kwa Simba kushindwa kuondoka na alama tatu, baada ya kukubali kipigo kama hicho dhidi ya Mbeya City kisha kulazimishwa suluhu na Mtibwa Sugar, michezo yote ikicheza ugenini.

Mara ya mwisho timu hiyo kufunga bao na kupata ushindi kwenye Ligi Kuu ni Januari Mosi, mwaka huu ilipoifunga Azam FC mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mchezo wa jana ulikuwa rahisi kwa Simba kushinda kuliko kupoteza kutokana na kukosa mabao mengi ya wazi.

Mfululizo wa kukosa mabao kwa Simba ulianza dakika ya tisa, wakati Pape Sakho alipopiga krosi iliyoleta kizaazaa langoni mwa Kagera Sugar, lakini wakati wakitaka kuuweka mpira wavuni, Bernard Morrison aliunawa na kuwa faulo.

Saido Kanoute alifanya makosa dakika tatu baadaye alipopokonywa mpira karibu na eneo la hatari na Hassan Mwaterema, aliyevuta hatua chache na kuachia shuti kali lililopaa juu, Simba ikanusurika kufungwa. Ndilo lililokuwa shambulizi hatari pekee kwa Kagera Sugar kipindi cha kwanza.

Kichwa dhaifu kilichopigwa na Rally Bwalya dakika ya 23 kutokana na krosi ya Morrison na kuikosesha Simba bao, na dakika ya 29, Mohamed Hussein 'Tshabalala' naye alipenyezewa mpira akiwa ndani ya eneo la hatari akapiga shuti dhaifu lililombabatiza kipa Said Kipao na kuokolewa na mabeki wa Kagera Sugar waliokuwa wakiongozwa na Abdallaah Mfuko.

Dakika moja baadaye, beki mwenzake wa pembeni, Shomari Kapombe naye alikosa bao la wazi alipobaki na kipa Kipao, lakini papara au woga ulimfanya kupiga mpira nje kwa mshangao wa mashabiki wote, kwani hakuwa amekabwa.

Ugonjwa wa kukosa mabao ulimpata pia Mzamiru Yassin alipotakiwa kuugusa tu mpira wa krosi ya Morrison, lakini alipiga hewa na mpira ukaambaa nje.

Kipindi cha pili kila timu ilifanya mabadiliko, Simba ikiwatoa Morrison, Tshabalala, Joash Onyango, Bwalya na kuwaingiza Yusuph Mhilu, Meddie Kagere, Hassan Dilunga, na Erasto Nyoni, lakini haikusaidia kitu, huku Kagera Sugar ikiwaingiza Erick Kyaruzi, Kiiza, Erick Mwijage, Ngueko Tientcheu raia wa Cameroon, kuchukua nafasi za David Luhende, Ramadhani, Jackson Kabirige na Hassan Mwaterema.

Mabadiliko hayo yaliisaidia Kagera Sugar badala ya Simba ambayo iliendelea kufanya mashambulizi yaliyoishia kwenye miguu ya wenyeji wao ambao walikuwa wamekaa nyuma zaidi na kushambulia kwa kushtukiza.

Pamoja na kufungwa Simba inaendelea kushika nafasi ya pili kwa kusalia na pointi 25, lakini ikiwa imezidiwa pointi 10 na vinara Yanga, Kagera Sugar ikitoka nafasi ya 11 hadi ya tisa ikiwa na pointi 16.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >